SUPA JACKPOT
TZS.1,042,026,796
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.CO.TZ
PIGA *150*87#



UKURASA 3

**IGP** Wambura awapangua tena makamanda polisi




UKURASA 13

# Nipashe

Ijumaa Oktoba 21, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581105

MWANGA WA JAMII

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian...

# ACT yaweka kigingi Bima ya Afya kwa Wote

**YASEMA** kuna kasoro nyingi, usiharakishwe Bungeni...

*Endelea ukurasa 2*



Kiongozi wa Chama cha ACT-Wazalendo, Zitto Kabwe, akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana, kuhusu umuhimu wa muswada wa Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote kupata muda zaidi wa kujadiliwa. Kulia ni Makamu Mwenyekiti wa ACT Bara, Dorothy Semu. **PICHA: MIRAJI MSALA**

UKURASA WA 25

## LIZ TRUSS AJIUZULU UWAZIRI MKUU, KAONGOZA UINGEREZA KWA SIKU 45 TU

BAADA ya kukalia kiti cha uwaziri mkuu wa Uingereza kwa siku 45 pekee, Liz Truss ametangaza kujiuzulu nafasi hiyo baada ya kuibuka...

## Waziri Ummy abaini uchepushaji dawa malaria, uchunguzi kufanywa

UKURASA 2



Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu

# Samia: Ifanyike tathmini Sheria Ukatili Kijinsia

UKURASA 7

**MICHEZO** YANGA: FURAHA YETU NI KUMFUNGA SIMBA UK. 32

**KATUNI** UK. 6



Wavuvi wa Kisiwa cha Irugwa, Wilaya ya Ukerewe, mkoani Mwanza, wakiwa wameanika taa zao zinazotumia umeme wa nishati ya jua kwa ajili ya kutegea dagaa nyakati za usiku kisiwani humo jana. Awali wavuvi walikuwa wakitumia taa aina ya karabai zinazoelezwa kutokuwa rafiki kwa mazingira kutokana na kumwaga mafuta ya taa ziwani na kutoa moshi. **PICHA: VITUS AUDAX**

# ACT yaweka kigingi Bima Afya kwa Wote

**Na Elizabeth Zaya**

CHAMA cha ACT-Wazalendo kimependekeza Muswada wa Bima ya Afya kwa Wote usipelekwe kusomwa kwa mara ya pili kwenye Bunge la mwezi ujao, badala yake upelekwe Januari mwakani ili kuruhusu wananchi waujadili kwa upana na kuuboresha zaidi.

Chama hicho kimesema, kuna haja pia ya muswada huo kusubiri matokeo ya awali ya Sensa ya Watu na Makazi na kuuboresha kulingana na idadi hiyo ya watu ya sasa.

Kauli hiyo ilitolewa na Kiongozi wa ACT-Wazalendo, Zitto Kabwe, wakati akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana.

"Rais Samia Suluhu Hassan amuagize Waziri wa Afya ili muswada usiende kusomwa kwa mara ya pili bungeni katika mkutano unaokuja, tupate muda wa kufanya mjadala mpana wa wadau wote," alisema.

Pia, Zitto alisema haoni sababu ya kuuwahisha wakati hivi karibuni serikali itatoa matokeo ya awali ya sensa ya watu na makazi ambayo nayo itasaidia kuboresha zaidi mchakato huo wa bima ya afya kwa wote.

"Hivi karibuni tutapata matokeo ya awali ya sensa, masuala yanayohusu bima ya afya ni ya demografia, yanahusu idadi ya watu, kama yatatoka hivi karibuni, kwa nini tuharakishe muswada sasa, tusisubiri kupata takwimu za sensa ya watu na makazi kwa namba halisi," alihoji.

"Wizara ya Afya, moja ya mapungufu yake makubwa ya muswada wao, hawana namba. Mtaalamu yeyote lazima atizame namba, kwa hiyo ni vyema usiende bungeni sasa kwenye mkutano unaofuata badala yake uende Januari," alisisitiza Zitto.

"Na hili ni jambo la kawaida kwenye mabunge ya Jumuiya ya madola. Na muswada ukishasomwa kwa mara ya kwanza tayari umeshaingia bungeni na hakuna tatizo, lakini ukiupeleka kwa mara ya pili ukasomwa ndani ya bunge unaweza kujikuta ni usumbufu, Waziri akalazimika kuuondoa tena."

Alisema tayari chama hicho kimeandika barua ya wazi kwenda kwa Rais ambayo inatarajiwa kuchapishwa wakati wowote, kikiomba muswada huo usipelekwe kusomwa kwa mara ya pili bungeni, na kutoa mjadala zaidi kwa wananchi.

"Pia tumeomba kikao na wakuu wote wa mifuko ya hifadhi ya jamii, Waziri wa Afya, Waziri wa Fedha pamoja na Mkuu wa Mfuko wa Bima ya afya ili tukae, tuwape namba zetu na wao watupe namba zao ili tujadiliane tupate jawabu," alisema Zitto.

**UPUNGUFU MUSWADA**

Chama hicho kimesema muswada huo una upungufu ambao bado unapaswa kujadiliwa na wananchi na kufanyiwa kazi na mamlaka husika.

Kilitaja baadhi ya upungufu kuwa ni pamoja na njia au mfumo wa kugharimia huduma za afya, kwamba miongoni mwa mapendekezo la muswada huo la kutaka kutumia michango ya wananchi kulipia bima zao wenyewe kila mwaka kwa asilimia yote haitoi uhakika na uendelevu wa utaratibu huo wa uchangiaji kwa wananchi walio katika sekta isiyo rasmi.

Upungufu mwingine walio ubaini haujaondoa matabaka yanayoletwa na vifurushi pamoja na viwango vya uchangiaji.

"Mfano, serikali inapendekeza viwango vipya vya uchangiaji kwa kila kaya yenye watu sita kuwa ni Sh. 340,000 na kwa mtu atakayejiunga nje ya mfumo wa kaya atalipia Sh. 84,000."

"Mwaka 2021 taarifa zinaonyesha kuwa asilimia 70 ya wananchi walikuwa wagonjwa wa nje ingawa waliolazwa walikuwa milioni 1.6. Kwa hali ya kupanda kwa gharama za maisha na uwezo wa kiuchumi, wananchi hawatakuwa na mwendelezo wa kulipia malipo haya kila mwaka bila kupata misukosuko.

Pia, muswada unaeleza adhabu mbalimbali kwa watumiaji na watoa huduma watakao kiuka sheria ya bima ya afya kwa wote bila kuelezea udhibiti wa ubadhirifu wa fedha za Mfuko wa Bima ya Afya kupitia mamlaka za serikali.

"Muswada wa serikali unaweka vigezo vya mwananchi kuwa na leseni, pasi ya kusafiria, kitambulisho cha NIDA, laini za simu ndipo apate kadi ya bima ya afya. Tumejiuliza, hivi kati ya NIDA na bima kipi kinaanza? Utaratibu huu unamnyima mwananchi uhuru na haki yake ya msingi ya kupata huduma ya afya ambazo tayari anazilipia kupitia kodi na tozo mbali mbali."

"Sheria hii haitekelezeki. Serikali irudi tena mezani, ili kuja na mpango bora unaotekelezeka kuendana na uhalisia wa maisha ya kila mtanzania. Lengo letu ni kupata Bima ya Afya kwa kila mwananchi."

"Katika maelezo yake Waziri wa Afya alisema kwamba watu wasio na uwezo watatambuliwa kupitia taarifa za uanachama wa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF). Takwimu za hali ya uchumi wa taifa mwaka 2021 zinaonyesha jumla ya watu milioni 6.3 sawa na asilimia 11 ya wananchi wote walinufaika na mfuko wa TASAF. Idadi hii ni ndogo kulinganisha na hali halisi ya umaskini nchini."

Kuhusu gharama za dawa na vifaa tiba, chama hicho kilisema, muswada huo haujagusa kichocheo cha ongezeko la gharama za dawa, vifaa tiba na vipimo ambao unaamuliwa na soko la dawa.

Septemba 23, mwaka huu, serikali iliwasilisha kwa mara ya kwanza muswada kwa wote bungeni ambao unalenga kuhakikisha kila mwananchi anajumuishwa katika Mfumo wa Bima ya Afya kupitia Mifuko ya Bima ya Afya ya umma iliyopo au kampuni binafsi za bima ya afya zilizopo.

## Waziri abaini uchepushaji dawa za malaria, uchunguzi kufanyika

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

SERIKALI imebaini uchepushwaji wa matumizi ya dawa za maralia, huku ikitangaza kuweka kambi kwenye mikoa minne kwa ajili ya kuanza uchunguzi wa kina ili kubaini zinakopelekwa.

Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, aliyasema hayo jana jijini hapo alipokuwa akizindua miradi miwili ya kutokomeza malaria yenye thamani ya Dola za Marekani milioni 45 ijulikanayo kama 'Dhibiti Malaria' na 'Shinda Malaria'.

Alisema imebainika kituo kinatibu wagonjwa 20, lakini maombi ya dawa ni zaidi ya wagonjwa 1,000.

"Je, dawa hizo nyingine zinapelekewa wapi? Kuna uchepushwaji unafanywa kwa ajili ya kwenda kuziuza, mnaniletea taarifa wenyewe kwamba malaria yamepungua nchini lakini cha kushangaza matumizi ya dawa hayajapungua, mnachukua dawa idadi ile ile bila kujua zinakwenda wapi, serikali tumeshabaini hilo natunalifanyia kazi," alisema Ummy.

Alisema kutokana na hali hiyo atakwenda kupiga kambi katika mikoa ya Katavi, Mtwara, Pwani na Ruvuma ambapo miradi hiyo itatekelezwa ili kubaini dawa hizo zinapelekwa wapi na hatua kali zitachukuliwa dhidi ya watakaobainika.

Alifafanua zaidi ya kuwa malaria nchini imepungua kwa asilimia 40 na wagonjwa waliolazwa ni idadi ndogo huku wale wanaotibiwa na kurudi nao idadi imepungua.

"Tunawashukuru serikali ya Marekani kwa ufadhili huu huku akiahidi atasimamia matumizi ya fedha hizo ili ziende kwenye matumizi sahihi," alisema.

Hata hivyo, aliagiza halmashauri kuhakikisha wanasimamia hilo ili maralia yatokomezwe hadi kufikia mwaka 2030.

Alisema vita vya maralia vinapungua mwaka hadi mwaka ambapo kwa sasa katika wagonjwa 100 wanaoripoti hospitalini unakuta wagonjwa wa malaria ni 16 au chini ya hapo, jambo linaloashiria malaria inakwenda kuisha moja kwa moja.

"Hii miradi iliundwa kwa ushirikiano wa karibu wa Wizara ya Afya ya Bara na Visiwani kupitia ya Marekani kwenye Shirika lake la Maendeleo ya Kimataifa USAID kwa kushirikiana na nchi washirika," alisema.

Naye Balozi wa Marekani nchini Tanzania, Donald Wright, alisema mradi wa awali umeonyesha mafanikio makubwa sana katika mapambano dhidi ya ugonjwa huo.

Alisema tangu mwaka 2006 serikali ya Marekani imechangia Dola za Marekani Milioni 661 kupitia Mpango wa Rais wa Marekani wa Kupambana na Malaria (PMI) ili kukabiliana na maralia nchini.

Mwakilishi wa Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) anayeshughulikia Afya, Rashid Kitambulilo, alisema wamejipanga kuhakikisha wanakabiliana na ugonjwa wa malaria ili kuutokomeza ifikapo mwaka 2030.

# Panga pangua ya IGP Wambura makamanda Polisi

**Na Mwandishi Wetu**

MKUU wa Jeshi la Polisi Nchini (IGP), Camillus Wambura, amefanya mabadiliko madogo kwa baadhi ya makamanda wa polisi wa mikoa.

Hii ni mara ya tatu kufanya mabadiliko kama hayo katika kipindi cha miezi mitatu tangu alipoteuliwa kuwa IGP na Rais Samia Suluhu Hassan Julai 20, mwaka huu.

Mara ya kwanza kwa IGP Wambura kufanya mabadiliko katika jeshi hilo, ilikuwa ni Agosti 12, alipowahamisha vituo vya kazi baadhi ya makamanda wa mikoa.

Mwezi mmoja baadaye, Septemba 13, IGP Wambura alifanya tena mabadiliko madogo kwa baadhi ya makamanda wa polisi wa mikoa kwa kuwahamisha baadhi yao vituo vya kazi, huku taarifa ikieleza kuwa mabadiliko hayo yalikuwa ni katika kuongeza ufanisi wa utekelezaji wa majukumu ya jeshi hilo.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na Msemaji wa Jeshi la Polisi, David Misime, IGP Wambura amewahamisha baadhi ya makamanda wa polisi kutoka katika nafasi zao na kuwapangia sehemu nyingine.

Taarifa hiyo ilieleza kuwa katika mabadiliko Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Polisi (SACP), Ulrich Matei, amepangiwa kuwa Mkuu wa Kitengo cha Polisi Wasaidizi na Kampuni Binafsi za Ulinzi nchini, akichukua nafasi ya Kamishna wa Polisi (ACP), Isaack Katamiti.

Pia ilieleza kuwa IGP amemhamisha Kamishna Msaidizi wa Polisi (SACP), Ramadhani Ng'anzi, aliyekuwa Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mwanza kwenda kuwa Mkuu wa Kikosi cha Usalama Barabarani Nchini.

Aliyekuwa Mkuu wa Kikosi hicho, Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Polisi (SACP), Wilbroad Mtafungwa, amepangiwa kuwa Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mwanza.

Kadhalika, aliyekuwa Ofisa Mnadhimu Mkoa wa Kipolisi Rufiji, Kamishna Msaidizi wa Polisi (ACP), Protus Mutayoba, amekuwa Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Rufiji baada ya Kamanda wa Mkoa huo kuhamishiwa Mkoa wa Kipolisi Temeke hivi karibuni.




Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Puma Energy Tanzania, Lameck Hiliyai, akizungumza na waandishi wa habari, baada ya kuzindua gesi ya Liquefied Petroleum (LPG) na "App ya PumaGas", katika warsha na mafunzo kwa wafanyabiashara wake, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Rais Samia Suluhu ateua mkurugenzi mpya NIMR

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS Samia Suluhu Hassan, amemteua Prof. Said Shehe Aboud kuwa Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu (NIMR).

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu, Zuhura Yunus, Prof. Aboud ni Mhadhiri Mwandamizi na Kaimu Mkurugenzi wa Mipango, Fedha na Utawala, Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili (MUHAS), Dar es Salaam.

Alisema Prof. Aboud anachukua nafasi ya Prof. Yunus Daud Mgaya ambaye amemaliza muda wake mwezi Septemba mwaka huu na kwamba uteuzi umeanza jana.


TRA

MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA

Imethibitishwa na ISO 9001:2015

## TAARIFA KWA UMMA

## USAJILI WA NAMBA YA UTAMBULISHO WA MLIPAKODI (TIN) KWA WAAJIRIWA

***Dar es salaam, Oktoba 18, 2022***

Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) inapenda kuukumbusha umma kuhusu waajiriwa kuwa na Namba ya Utambulisho wa Mlipakodi (TIN) ikiwa ni matakwa ya Kifungu cha 22 cha Sheria ya Usimamizi wa Kodi, SURA 438 R.E 2019. Matumizi ya TIN sahihi ni muhimu katika kuweka kumbukumbu sahihi za waajiriwa na kuwezesha uwasilishaji wa ritani ya kodi za waajiriwa yaani Pay as You Earn (PAYE) kwa kutumia mfumo wa a uwasilishaji wa ritani kielekroniki (e-filing).

Ikumbukwe kuwa, Mamlaka iliagiza waajiri wote wahakikishe waajiriwa wao wana TIN na kuanza kuzitumia kikamilifu ifikapo tarehe 31 Desemba 2020. Pamoja na ukweli kwamba waajiri wengi wameonesha mwitikio chanya bado kuna kundi dogo la waajiri ambao wameshindwa kusimamia matakwa hayo ya kisheria na wamekuwa hawatumii TIN sahihi za waajiriwa au kutumia TIN 999 999 999 ambayo ilikua ni ya mfano katika kipindi cha mpito.

kufuatia hilo, Mamlaka inapenda kuwakumbushwa waajiri na waajiriwa wote kuhakikisha kuwa wanazingatia takwa hili la kisheria la kuhakikisha matumizi sahihi ya TIN. Ikumbukwe kuwa TIN hutolewa bure na Mamlaka na upatikanaji wake ni rahisi. Kwa waajiriwa wenye namba za usajili (NIN) inayotolewa na Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA), wanaweza kuomba TIN kwa njia ya mtandao kupitia mfumo wa online TIN Registration unaopatikana kwenye tovuti ya TRA (ambayo ni **www.tra.go.tz**). Waajiriwa wasio na NIN wanalazimika kutembelea Ofisi za TRA ili kufanya maombi na kupatiwa TIN.

Kwa taarifa zaidi, tembelea Ofisi za TRA zilizo Karibu nawe au tumia mawasiliano yafuatayo:

| | |
|---|---|
| **Tovuti** | **: www.tra.go.tz** |
| **Namba za Simu bila malipo** | **: 0800 750 075 / 0800 780 078 au 0800110016** |
| **WhatsApp** | **: 0744 23 33 33** |
| **Barua pepe** | **: huduma@tra.go.tz** |

**"Pamoja Tunajenga Taifa Letu"**

**Imetolewa na:**

**IDARA YA HUDUMA NA ELIMU KWA MLIPAKODI**
**TRA MAKAO MAKUU**

217098402

# GGML, Rafiki Surgical Mission zatoa magari ya wagonjwa Geita

**Na Mwandishi Wetu,** GEITA

KATIKA kuimarisha uhusiano mzuri baina ya serikali na jamii zinazoizunguka kampuni ya Geita Gold Mining Limited (GGML) na Taasisi ya Rafiki Surgical Mission kutoka Australia, wametoa msaada wa magari mawili ya kubeba wagonjwa kwa Halmashauri ya Wilaya ya Geita mkoani Geita.

Akizungumza katika hafla ya makabidhiano jana katika eneo la Nzera mkoani Geita, Mkurugenzi Mkuu wa GGML, Terry Strong alisema GGML kwa kushirikiana na Shirika la Rafiki Surgical Mission wameamua kutoa magari hayo ili kuokoa maisha ya wagonjwa wengi katika halmashauri hiyo.

"Halmashauri ya Wilaya ya Geita iliomba magari mawili ya kubebea wagonjwa kutoka GGML kwa ajili ya kusaidia jamii ya eneo hili kwa sababu baadhi ya wagonjwa walikuwa wakipata rufani kwenda Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Geita ambayo iko mbali na Nzera na maeneo mengine ndani ya Halmashauri ya Wilaya ya Geita.

"GGML na Rafiki Surgical Mission walijibu vyema ombi hilo kwa sababu ni washirika wazuri wa maendeleo ambao wanasaidia miradi ya afya katika kipindi cha miaka 20 iliyopita," alisema na kuongeza kuwa GGML na Rafiki Surgical Mission wamekuwa na ushirikiano mkubwa tangu mwaka 2000 kupitia upasuaji wa mdomo sungura na zaidi ya wagonjwa 1,700 wamenufaika na mpango huo.

Terry alisema kuwa GGML imetumia zaidi ya Sh. bilioni tano kusaidia miundombinu ya afya na usambazaji wa vifaa tiba kwa kipindi cha miaka 20 ya uendeshaji wake mkoani Geita.

Alikumbusha kuwa GGML ilisaidia ujenzi wa Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Geita, ujenzi na ukamilishaji wa vituo vya afya zaidi ya 10 katika Mji wa Geita, ujenzi wa vituo vipya vya afya vinne, uboreshaji wa Kituo cha Afya Kasota na ukamilishaji wa vituo vingine vya afya na usambazaji wa vifaa tiba vya vituo vya Katoro na Bukoli vilivyoko katika Halmashauri ya Wilaya ya Geita.

Akizungumza katika hafla hiyo kwa niaba ya serikali, Mkuu wa Wilaya ya Geita, Wilson Shimo alisema msaada wa GGML umekuja wakati mwafaka kwa sababu utaokoa maisha ya wagonjwa katika halmashauri hiyo.

Aliwaomba wadau wengine wa Halmashauri ya Wilaya ya Geita kushirikiana na serikali ili kukabiliana na vikwazo katika utoaji wa huduma za kiafya mkoani Geita.

"GGML imekuwa mshirika mzuri katika kusaidia miradi mbalimbali ya afya mkoani Geita na Tanzania kwa ujumla. Mwaka jana, GGML ilitoa hadubini mpya kabisa kusaidia mapambano dhidi ya TB katika maeneo ya madini Geita," alisema na kuongeza kuwa GGML imekuwa ikiendesha programu tofauti za afya kwa kushirikiana na serikali kutatua kero za sekta ya afya mkoani Geita.

Alisema tangu kuanzishwa kwa GGML imekuwa ikishirikiana kwa karibu na serikali, hususan Halmashauri za Wilaya na Miji ya Geita kusaidia miradi mbalimbali endelevu ya jamii mkoani Geita.




Mkuu wa Wilaya ya Geita, Wilson Shimo (katikati), akikata utepe kukabidhi magari mawili ya kubebea wagonjwa yaliyotolewa na Kampuni ya GGML na Shirika la Rafiki Surgical Mission kwa Halmashauri ya Wilaya hiyo, mkoani Geita. Wengine ni Mkurugenzi Mtendaji wa GGML, Terry Strong (kulia) na Mganga Mkuu wa Wilaya ya Geita, Dk. Modest Buchad Rwakahemula. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Ripoti kikosi kazi kutua kwa Rais leo

**Na Mary Geofrey**

RIPOTI ya kikosi kazi cha kupitia maoni ya wadau wa demokrasia, inatarajia kuwasilishwa kwa Rais Samia Suluhu Hassan leo.

Macho na masikio ya wadau wa demokrasia nchini wameelekeza kwenye kupata suluhu ya mchakato wa Katiba mpya, uhuru wa shughuli za kisiasa na tume huru ya uchaguzi.

Kikosi kazi hicho kinachoongozwa na Mwenyekiti Prof. Rwekaza Mukandala, kiliundwa na Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa ili kupitia maoni ya wadau wa demokrasia waliokutana jijini Dodoma Desemba 15 hadi 17, mwaka jana.

Kikao hicho kilifunguliwa na Rais Samia na baada ya kuundwa kilipewa jukumu la kupitia maoni 80 yaliyotolewa na wadau hao kwa siku hizo.

Machi 12, mwaka huu, Prof. Mukandala aliwaongoza wajumbe wa kikosi kazi hicho kuwasilisha taarifa yake kwa Rais Samia baada ya hapo, mkuu huyo wa nchi, alisema kuanzia wakati huo kitakuwa kikiripoti kwake.

Baada ya kukabidhi ripoti hiyo na kupewa jukumu la kukusanya maoni kutoka kwa wadau mbalimbali wakiwamo viongozi waandamizi, kimekamilisha kazi hiyo rasmi.

Mmoja wa wajumbe katika kikosi kazi hicho (jina linahifadhiwa), aliieleza Nipashe kuwa kinawasilisha ripoti hiyo mbele ya Rais Samia leo baada ya kukamilisha kazi iliyopewa.

Maeneo tisa ambayo yamepewa kipaumbele katika ripoti hiyo ni mikutano ya hadhara na ndani ya vyama vya siasa, masuala yanayohusu uchaguzi, mfumo wa maridhiano ili kudumisha haki, amani, utulivu na Umoja wa Kitaifa.

Maeneo mengine ni ushiriki wa wanawake na makundi maalumu katika siasa na demokrasia ya vyama vingi vya siasa, elimu ya uraia na rushwa.

Mapema mwezi huu, Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Mwinyi, alifungua mkutano wa majadiliano mahususi ya Zanzibar yanayohusu vyama vingi vya siasa. Dk. Mwinyi alisema lengo na madhumuni ni kuendesha shughuli za kisiasa katika hali ya amani, umoja na mshikamano.

Alisema ni imani yake timu hiyo ya watu 11 kwa uwezo wao, ubunifu na weledi waliokuwa nao, wataikamilisha kazi hiyo vyema ili serikali kupokea taarifa rasmi kutoka kwao.

Dk. Mwinyi aliwapongeza wajumbe wa kikosi kazi hicho kwa kuyafanyia kazi ya kukusanya maoni ya wadau na kuwa na mapendekezo maalum serikalini.

Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Thabit Idarusi Faina, alisema kikosi kazi hicho pia kitapitia hotuba ya Makamu wa Kwanza aliyoitoa Oktoba 6, mwaka huu, wakati akifunga mkutano huo, kupitia nyaraka mbalimbali ikiwamo Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na ya Zanzibar, sheria mbalimbali ikiwamo ya Tume ya Uchaguzi Zanzibar.

Alisema pia kitapitia ripoti na machapisho yanayohusu malengo ya mkutano huo ili kupata uelewa mzuri wa maoni na mapendekezo ya wadau yaliyotolewa katika mkutano huo.

## NHC yaanika yaliyomo kwenye sera ya ubia

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SHIRIKA la Nyumba la Taifa (NHC), limesema sera mpya ya ubia kwa kipindi cha miaka mitatu hadi mitano inatarajiwa kuwa na miradi 200 ya ubia yenye thamani ya Dola za Marekani bilioni 400.

Katika utekelezaji miradi hiyo, shirika hilo linatarajia kuvunja baadhi ya majengo yake chakavu yaliyoko katika maeneo ya katikati ya miji ili kufanyika uwekezaji wa majengo makubwa kupitia sera hiyo.

Akizungumza jana na waandishi wa habari jijini hapo, Mkurugenzi wa Maendeleo ya Uwekezaji na Biashara wa NHC, William Ngenya, alisema uzinduzi wa sera hiyo utafanyika Novemba 14, mwaka huu, Dar es Salaam na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa.

Ngenya alisema sera hiyo itaongeza ajira kupitia miradi ya ujenzi, kuongeza mandhari na miji na kuongezea serikali mapato na kwamba uwekezaji huo utaanza kwenye viwanja kati ya 60 na 70 vya shirika.

"Tunaungana na Rais Samia Suluhu Hassan kuleta wawekezaji wa ndani na nje ili uchumi ukue zaidi. Tumeboresha sera kwa kuweka vitu vinne ambapo mwekezaji ataangalia," alisema.

Alitaja vitu hivyo ni kutumia ardhi kama mtaji ambapo mbia anapata umiliki wa asilimia 40 mwishoni mwa miaka 15 ya uwekezaji na nyingine inampa asilimia 25 baada ya miaka 25 ya uwekezaji kwenye mradi.

"Nyingine ni shirika linaweka ardhi, mtaji na mbia yeye anaweka fedha tunatekeleza kwa pamoja. Hii ni kwa miradi mikubwa ambayo thamani yake inazidi Sh. bilioni 50, nyingine ni kujenga, kuuza na kugawana.

"Shirika linaweka ardhi na mbia anaweka fedha jengo linajengwa halafu linauzwa lote. Kuna nyingine shirika linatoa ardhi mbia anajenga anatumia jengo kwa kipindi kilichoko kwenye mkataba miaka 10 hadi 30 mbia atajenga baada ya mkataba kuisha, linarudi kwa Shirika la Nyumba," alisema.

"Kuna ardhi ina thamani ya juu ipo katikati ya miji kama viwanja tupu au majengo yake ambayo yamechakaa na thamani yake haikidhi thamani ya ardhi, tunakwenda kutumia ardhi hizo kama mtaji wa kuwekeza majengo makubwa yenye thamani kubwa yatakayoleta tija kwa shirika," alisisitiza.

Alitaja miongoni mwa masharti kuwa ni uwekezaji utakaofanyika uwe na thamani ya mara nne ya ardhi inayowekezwa.

Naye Meneja Habari na Uhusiano wa NHC, Muungano Saguya, alisema kumekuwa na mwitikio mkubwa wa kampuni binafsi za ndani na nje ya nchi kushiriki katika uzinduzi huo ikiwamo Diaspora na wawekezaji wa kimataifa.

"Awali tulitangaza kwamba sera itazinduliwa kesho (leo) lakini baada ya kusema tutazindua kulikuwa na maombi mengi ya kushiriki, kulikuwa na maombi ya wawekezaji wa sekta binafsi hasa wa kutoka nje wakaomba usogezwe mbele hivyo uzinduzi utakuwa mwezi ujao," alisema.

Alisema sera hiyo ilianza mwaka 1993 na kufanyiwa marekebisho ambayo yamezingatia kuvutia uwekezaji kwa maslahi ya shirika na wawekezaji.

"Tangu kuanza kwa utaratibu huu miradi 111 ilitekelezwa ikiwa na thamani ya Sh. bilioni 300 ambapo kati yake miradi 81 ya Sh. bilioni 240 imekamilika na kuanza kutumika na miradi 30 yenye thamani ya Sh. bilioni 60 inaendelea kukamilishwa," alisema.

HABARI KITAIFA

# SMZ yaahidi ushirikiano na taasisi za kitaalamu

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Mwinyi, amesema serikali ipo tayari kushirikiana na taasizi za kitaalamu kukuza usimamizi bora wa miradi inayoanzishwa ili kuongeza ufanisi na kukuza uchumi na maendeleo ya visiwa hivyo.

Rais Mwinyi aliyasema hayo kwenye ufunguzi wa mkutano wa mwaka wa Taasisi ya Kimataifa ya Usimamizi wa Miradi Tawi la Tanzania katika hotuba iliyosomwa kwa niaba yake na Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Othman Masoud Othman.

Alisema kufanikiwa kwa utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Tanzania kwa kiasi kikubwa kunategemea usimamizi bora wa miradi kwa kutumia utaalamu sahihi na uwajibikaji bora wa wataalamu wanaokuwa na dhamana ya kusimamia miradi inayoanzishwa. Rais Mwinyi alisema, kutokana na mabadiliko makubwa ya sayansi na teknolojia, kasi ya utandawazi na ongezeko la mahitaji ya miradi mikubwa ya kimaendeleo duniani kuna ulazima kwa nchi kuwa na wataalamu bora wenye ujuzi na maarifa sahihi ya usimamizi wa miradi katika ngazi ya taifa, kikanda na kimataifa ili kuongeza ufanisi kwenye utekelezaji wa miradi hiyo.

Pia amewakaribisha wataalamu mbalimbali kupitia taasisi hiyo kushirikiana na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika utekelezaji na usimamizi bora wa miradi ya maendeleo na kiuchumi kwenye sekta tofauti nchini.

Alisema ushirikiano huo unaweza kuwa kwa uwekezaji, usimamizi wa miradi ama kusaidiana kwa pamoja kuwavuta wawekezaji kutoka mataifa na nchi mbalimbali duniani kuwekeza Zanzibar.

Ametaja fursa nyingi za uwekezaji wa miradi ya kiuchumi na kimaendeleo kwenye sekta tofauti za kilimo, biashara na huduma sambamba na kuweka vivutio bora kwa wawekezaji ili kuja kuwekeza Zanzibar.

Naye Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji, Mudrik Ramadhan Soraga, alisema Serikali ya Zanzibar inafanya jitihada kutengeneza mazingira bora ya uwekezaji ikiwa ni pamoja na kuweka miundombinu bora ya kusaidia uwekezaji nchini.

Alisema, hali hiyo inatokana na mazingira bora ya kisiasa kwa kuwapo amani na utulivu jambo linalochangia jitihada za maendeleo kufanikiwa.



Kaimu Mkuu wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai wa Polisi Wilaya ya Muheza, mkoani Tanga, Teodori Njawa (kushoto) akiangalia mwili wa Zahoro Athumani (40), mkazi wa Bumbuli, wilayani Lushoto (aliyefunikwa khanga), aliyefariki wilayani Lushoto mkoani humo mapema wiki hii. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Majaliwa atoa siku 15 kampuni kukamilisha ujenzi wa barabara

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa ametoa siku 15 kwa Kampuni ya Inter Country Contractors kukamilisha ujenzi wa miradi ya barabara katika kisiwa cha Ukerewe mkoani Mwanza.

Alitoa agizo hilo jana alipokutana na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais TAMISEMI, viongozi wa wilaya ya Ukerewe na watendaji wa TARURA ofisini kwake Mlimwa, jijini Dodoma.

Alisema kuwa kampuni hiyo ilipewa kandarasi ya ujenzi wa barabara zenye urefu wa kilomita 13, kwa kiwango cha lami na changarawe katika kisiwa hicho, ambaye alipaswa kukamilisha Julai mwaka 2012.

"Serikali inatoa fedha nyingi kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo, ikiwamo ujenzi wa barabara, katika hili tumetoa kipaumbele kwa makandarasi wazawa, tunachotegemea ni uaminifu wenu na utekelezaji wa miradi hii iwe ya viwango na mkamilishe kwa wakati," alisema.

Majaliwa alisema ni vyema Meneja wa Wakala wa Barabara za Vijijini na Mjini (TARURA), mikoa na wilaya wakatekeleza majukumu yao ipasavyo, ili kuhakikisha ujenzi wa barabara katika maeneo mbalimbali nchini na ukamilika kwa wakati na kwa viwango vilivyokusudiwa.

Kwa upande wake, Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais TAMISEMI, Angellah Kairuki, alisema wamepokea maelekezo ya Waziri Mkuu na kuahidi kufanya mapitio makubwa ya mfumo wa kiutendaji wa TARURA ili kuongeza ufanisi wa utekelezaji wa miradi ndani ya taasisi hiyo.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA KATIBA NA SHERIA**

Telegramu: "LEGAL"
Simu Na.: +255 26 2310019
Nukushi: +255 26 2310056
Barua Pepe: km@sheria.go.tz
Tovuti: www.sheria.go.tz

Mji wa Serikali Mtumba,
Mtaa wa Katiba,
S. L. P. 315,
40484 DODOMA.

## TANGAZO KWA UMMA

Kufuatia taarifa ya matokeo ya wanafunzi wa Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo ya hivi karibuni, na baada ya kuibuka kwa taharuki miongoni mwa wanajamii wakiwemo wanazuoni na wadau mbalimbali wa sekta ya sheria kuhusu ufaulu mdogo wa wanafunzi katika tasnia ya Sheria, tarehe 12 Oktoba, 2022 Mheshimiwa Dkt. Damas D. Ndumbaro (Mb.), Waziri wa Katiba na Sheria aliunda Kamati Maalum ya kufanya tathmini ya mfumo wa elimu ya Sheria nchini na changamoto zinazoukabili mfumo huo ikiwa ni pamoja na namna mafunzo ya uanasheria kwa vitendo yanavyotolewa.

Pamoja na mambo mengine, Kamati hiyo imepewa jukumu la kushauri namna ya kuboresha mfumo huo ili kukidhi mahitaji ya taaluma ya Sheria kwa lengo la kuwa na ushindani wa kitaifa na kimataifa. Kamati katika utekelezaji wa majukumu yake kwa mujibu wa Hadidu za Rejea ilizopewa, itapokea maoni kwa maandishi pia kuwasikiliza wadau mbalimbali ana kwa ana.

Kwa kuwa siyo wananchi wote watapata fursa ya kufika mbele ya Kamati kutoa maoni, Mhe. Dkt. Harrison G. Mwakyembe, Mwenyekiti wa Kamati anawaalika wananchi na wadau wenye mapenzi mema na uboreshaji wa mfumo wa elimu ya sheria nchini na elimu ya uanasheria kwa vitendo, kuwasilisha maoni kwa maandishi ili kuiwezesha Kamati kupata maoni mengi kadri inavyowezekana na hatimaye kushauri ipasavyo. Mwisho wa kupokea maoni ya maandishi ni tarehe
**24 Oktoba, 2022 saa 10:00 jioni.**

*Maoni hayo yawasilishwe kupitia barua pepe ya km@sheria.go.tz, mitandao ya kijamii ya twitter: @Sheria_Katiba; Instagram @katibanasheria_ au WhatsApp kwa namba 0742 910529.*

**IMETOLEWA NA:**

**KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI WIZARA YA KATIBA NA SHERIA**
**18 Oktoba, 2022**

217105302

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Serikali inapaswa kufanyia kazi ushauri kuhusu miradi

**WATAALAMU** wa masuala ya ubunifu majengo na wakadiriaji majenzi, juzi walifanya mkutano wao wa tatu jijini Dar es Salaam ili kubadilishana uzoefu na kujadili changamoto zinazowakabili pamoja na kuzitafutia ufumbuzi.

Pamoja na mambo mengine, wataalamu hao kupitia Mwenyekiti wa Bodi ya Usajili wa Wabunifu majengo na Wakadiriaji Majenzi (AQRB), Dk. Ludogija Bulamile, walianika suala la kukithiri kwa viwango duni katika miradi ikiwamo ile ya serikali.

Bila kuuma maneno, Dk. Ludogoja alisema chanzo cha tatizo hilo ni kutokushirikishwa wataalamu wa fani husika wakiwamo wahandisi, wabunifu majengo na wakadiriaji wa gharama za ujenzi.

Licha ya kuanika tatizo hilo, Dk. Ludigija kwa niaba ya wataalamu hao, alitoa ufumbuzi wa suala hilo ikiwamo kushirikishwa kwa wataalamu wa fani mbalimbali kwenye miradi inayohitaji umakini ili idumu na kutumika kwa muda mrefu. Miongoni mwa miradi ambayo aliitaja kuwa inapaswa kuwapo wataalamu wa fani husika ni pamoja na ujenzi uwe wa barabara, majengo, usambazaji wa maji na upanuzi wa bandari.

Ni ukweli usiopingika kwamba miradi mingi imekuwa ikitekelezwa kwa kiwango duni na matokeo yake kuharibika baada ya muda mfupi na mingine kama ya maji kushindwa kutumika kabisa kwa kushindwa kutoa maji.

Kwa muda mrefu imeshuhudiwa viongozi wakiwa katika ziara za kikazi mikoani au wakati wa mbio za mwenge kukiwa na taarifa za miradi kutekelezwa kwa viwango vya chini na hata viongozi kama vile wa msafara wa mwenge wakikataa kuizindua au kuipokea kwa sababu hizo.

Mbali na miradi hiyo, mara kwa mara imekuwa ikielezwa kuwa baadhi ya majengo katika miji mikubwa, Dar es Salaam ikiwamo, yamejengwa kwa kulipuliwa au kutokukidhi viwango pamoja na ubora unaotakiwa. Yako majengo ambayo yaliwahi kuanguka kwa sababu ya vifaa vilivyotumika kutokuwa na uwiano wa majengo husika.

Wiki hii kwa mfano, Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, wiki hii alifanya ziara wilayani Namtumbo, Ruvuma na kukagua ujenzi wa hospitali ya wilaya na kuibua madudu ikiwamo milango iliyofungwa kutokuwa na ubora. Mtu aliyeulizwa kuhusu ujenzi huo ni mganga mkuu wa wilaya ambaye hahusiani kabisa na hana taaluma yoyote kuhusu ujenzi.


Kinachoonekana hapo ni kwamba aliyepewa fedha kwa ajili ya ujenzi huo ni mganga mkuu ambaye kitaaluma ni daktari kwa hiyo hata angedanganywa kuhusu vifaa vinavyotakiwa angekubali kwa sababu hana uelewa wowote kuhusu ujenzi. Laiti wangeshirikishwa wahandisi katika mchakato mzima, ni dhahiri kwamba kusingekuwa na kasoro nyingi kama zilizoibuliwa na Waziri Mkuu.

Madudu katika hospitali ya Namtumbo ni mfano mmoja tu lakini kuna miradi mingi ya maji na barabara ambayo imekuwa ikijengwa kwa viwango duni na matokeo yake kuharibika baada ya muda mfupi. Kwa mfano, ziko barabara nyingi katika mkoa wa Dar es Salaam ambazo zimejengwa na kuharibika baada ya muda mfupi na kuwapo kazi za kuziba viraka kila uchao.

Kama ilivyoshauri AQRB, ni vyema serikali ikasikiliza ushauri na kuufanyia kazi hasa kuwapo kwa wataalamu wa fani husika ambazo zinahusiana na utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Kama ni barabara, ni vyema wakawapo wahandisi, wabunifu na watu wa afya na usalama kazini badala ya kumwachia mkandarasi akaendelea na ujenzi bila kuangalia kama vigezo na masharti katika mradi vimezingatiwa.

Serikali inatumia mabilioni ya shilingi katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo, hivyo hakuna budi kuhakikisha kuna usimamizi wa kutosha pamoja na thamani ya fedha katika kazi husika badala ya kulipuliwa na kutokudumu.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Tufanye kila tuwezalo maradhi kipindupindu kiishie kiliko

Na Sabato Kasika

**KIPINDUPINDU** ni moja ya magonjwa ambayo wataalam wa afya wanasema husababishwa na aina ya bakteria aitwaye 'vibrio cholerae' na huambukizwa kwa viini vinavyoenezwa kupitia kinyesi toka kwa watu wenye ugonjwa huo.

Hapa nchini, ugonjwa huo umekuwa ukiibuka na kutoweka, huku ukiacha vilio kwenye baadhi ya familia kutokana na watu kufariki dunia, ambapo serikali kwa upande wake huhimiza umuhimu wa kuzingatia masharti ya kuuepuka.

Kwa sasa Wizara ya Afya imetoa tahadhari kuhusu kulipuka kwa ugonjwa huo nchini baada ya kubainika kuwa umetua Malawi na kuua watu 132, ambapo mikoa inayopakana na nchi hiyo imetakiwa kuwa makini.

Taarifa ya Mganga Mkuu wa Serikali Dk. Aifello Sichalwe, inabainisha kuwa mlipuko umekwishaenea katika wilaya 25 nchini humo huku watu 4,604 wakiwa wameugua na 132 kupoteza maisha kutokana na mlipuko huo.

Kutokana na mwingiliano wa shughuli za kiuchumi na kijamii uliopo kati ya watu wa Malawi na Tanzania, wizara hiyo inatoa tahadhari dhidi ya ugonjwa wa kipindupindu hususan katika mikoa na wilaya zinazopakana na nchi hiyo, ili kuudhibiti usiingie na kuenea nchini.

Ninadhani tahadhari hiyo ingepewa uzito na Watanzania wote, kwani suala la muingiliano wa Watanzania na nchi nyingine ni mkubwa, hivyo watu wasidhani kuwa wale wa mpakani ndio wanaotakiwa kuwa makini.

Lakini pia suala la kila mtu kuzingatia kuchemsha maji ya kunywa au kutibu kwa dawa maalumu na kuyatunza vizuri wakati wa matumizi ni jambo la muhimu, ingawa baadhi ya watu wamekuwa wakipuuzia.

Sio siri kwamba wapo baadhi ya watu wasiochemsha maji ya kunywa wala kuyawekea dawa, wakidai kuwa wakifanya hivyo yanakosa ladha au yanakuwa na harufu wasiyoipenda.

Vilevile, wengine hawako makini kwenye suala la usafi wa mazingira katika biashara zao hasa mamalishe na babalishe, kwani wanatupa taka ovyo na kusababisha hata mazingira wanayofanyia biashara kunuka.

Kwa mfano, katika baadhi ya maeneo ya jiji la Dar es Salaam, ni jambo la kawaida kwa wafanyabiashara hao wa chakula kumwaga mabaki ya vyakula kwenye mitaro ya maji ya mvua, hali inayosababisha yanuke.

Kwa mazingira kama hayo, ni rahisi inzi kutua na kuondoka na uchafu hadi kwenye chakula anachokula mteja, na mwisho wa siku ni kuambukizwa kipindupindu au ugonjwa wa kuhara.

Sehemu ambayo watu wanapata huduma ya chakula haipaswi kunuka, lakini baadhi ya maeneo, si jambo la ajabu kukumbana na harufu mbaya ya taka huku wateja wakiendelea kupata mlo wa mchana au jioni.

Ninadhani maofisa afya wanatakiwa kusimamia usafi wa mazingira katika maeneo yao na kuwakumbusha wananchi kuzingatia maelekezo yanayotolewa na wataalamu wa afya juu ya kujikinga dhidi ya magonjwa mbalimbali.

Ikumbukwe kwamba, kinga ni bora kuliko tiba, hivyo ni vyema jamii isisubiri ugonjwa huo uvuke mpakani mwa Malawi hadi maeneo ya mbali kama Dar es Salaam ndipo wachukue hatua.

Utiririshaji wa majitaka, kutupa taka ovyo au kuziacha kwa muda mrefu bila kuzipeleka dampo, limekuwa ni kama jambo la kawaida, lakini husababisha kuwapo kwa mazalia ya nzi hali inayoongeza kuhatarisha afya ya jamii, kwani mtindo huo ni moja ya vyanzo vya kuenea kwa ugonjwa wa kipindupindu.

Hivyo, ninadhani tahadhari iliyotolewa na Wizara ya Afya, ni muhimu kuzingatiwa, ili kuepuka kukumbwa na ugonjwa huo au kuambukiza wengine. kwa sababu ya uzembe wa kutozingatia maelekezo ya wataalamu wa afya.

# Samia: Ifanyike tathmini Sheria Ukatili Kijinsia

**Na Romana Mallya**



RAIS Samia Suluhu Hassan, ameagiza kufanyike tathmini ya sheria mbalimbali zinazowalinda wanawake na watoto, ili kuona kama zimeleta matokeo tangu zilipotungwa.

Amesema licha ya kuwapo kwa sheria hizo kwa miaka mingi bado matukio ya ukatili wa kijinsia yameendelea kutokea ndani ya jamii.

Samia aliyasema hayo jana katika kumbukumbu ya miaka 25 ya kuanzishwa kwa Shirika la Wanawake katika Sheria na Maendeleo Afrika (WiLDAF), yenye kaulimbiu ya

'Miaka 25 ya Kutumia Sheria Kuboresha Maisha ya Wanawake'.

Kwa mujibu wa Rais, tathmini ikifanyika itasaidia kubainisha upungufu wa sheria zipi zifutwe na zipi ziunganishwe.

Pia alitaka tathmini hiyo ihusishe sheria za kimila kwa kuangalia ambazo zinaendeleza ukatili dhidi ya wanawake na watoto ziondolewe na nzuri ziboreshwe.

Alitolea mfano wa Sheria ya Kujamiiana na nyingine kandamizi ambazo zinadhoofisha jitihada za kuwainua kiuchumi kundi hilo.

**SHERIA ZIANDIKWE KISWAHILI**

Rais Samia alitaka mchakato wa kubadilisha sheria ziwe kwa lugha ya Kiswahili uendelee, ili zikatumike kufundisha na kutoa elimu kwa jamii kwa sababu pamoja na kuwapo kwake, lakini makosa yanaendelea kutendeka.

Kadhalika, alisema kwa upande wa kisera na utawala bora bado wana kazi kubwa ya kufanya ili sheria zilizotungwa zifanye kazi vizuri.

Alisema serikali imeendelea kubadilisha sheria na sera ili wanafunzi wasichana watumie muda mwingi shuleni kabla ya kuolewa.

Aliwataka WiLDAF na taasisi nyingine wanapotunga mambo wahakikishe yanakwenda chini kwa wananchi kwa ajili ya kuelimisha.

Awali, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi WiLDAF, Dk. Monica Mhoja, alisema kwa miaka 25 ya shirika hilo linajivunia kuwa sehemu ya kuchangia mabadiliko makubwa ya sheria na sera zinazolenga kuleta usawa wa kijinsia na kuwatetea wanawake na watoto kutoka katika mila, desturi na tamaduni kandamizi.

Alitaja baadhi ya sheria hizo ni; ya Makosa ya Kujamiiana (SOSPA) ya mwaka 1998 ambayo imeingizwa katika Sheria ya Kanuni za Adhabu.

Nyingine ni Sheria Ardhi ya Vijijini ya mwaka 1999, Sheria ya Mtoto ya mwaka 2009, Sheria Dhidi ya Usafirishaji Haramu wa Binadamu ya mwaka 2008, Sheria ya UKIMWI ya mwaka 2008 na Sheria ya Haki za Watu Wenye Ulemavu ya mwaka 2010.

Kadhalika, alisema WiLDAF ilishiriki utungwaji wa Sera na Mipango ya Serikali ikiwamo mabadiliko ya fomu Namba 3 ya polisi maarufu PF3 na mpango wa Taifa wa Kutokomeza Vitendo vya Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto (MTAKUWWA) mwaka 2017-2022.

Alisema bado kuna changamoto nyingi katika sheria ambazo zimekuwa kikwazo kwa wanawake kupata haki zao, kumiliki mali na kushiriki shughuli za kiuchumi na kuinua Pato la Taifa.

"Tunaomba kuharakisha mabadiliko ya Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1971, ucheleweshaji umeendelea kusababisha watoto wa kike kuolewa katika umri mdogo na kukumbana na ukatili wa kijinsia, mchakato huu unachukua muda mrefu.

"Kufutwa kwa Sheria za Kimila za Mirathi, imekuwa mwiba kwa wanawake na watoto wa kike, sheria hii imesababisha wanawake kuwa maskini na tegemezi kwa mali waliyotolea jasho."

Pia alitaja sheria za kimila, kuwa bado zinaendelea kufanya kazi pamoja na kupewa miezi 12 tangu uamuzi kutolewa Machi 2, 2015 zirekebishwe.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa WiLDAF, Wakili Anna Kulaya, alisema miaka 25 mbele ya kumbukizi wanawake wategemee kuchukua nafasi zaidi za uongozi na wategemee kuwapo kwa sheria bora za kuwalinda wanawake na watoto ambazo pia zitakwenda kidigitali.

Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima, alisema wanawake ndiyo hutumika katika shughuli mbalimbali lakini kila siku wao ndio vilio.

Waziri wa Katiba na Sheria, Dk. Damas Ndumbaro, alisema kwa kushirikiana na WiLDAF wamekubaliana kuimarisha mifumo ya utoaji wa haki na kufanya mabadiliko ya baadhi ya sheria, ikiwamo na miradhi na wanaendelea na majadiliano ili Sheria ya Ukatili wa Kijinsia iweze kutungwa rasmi.

EAST AFRICAN
CRUDE OIL
PIPELINE

**OMBI LA KUONESHA NIA YA KUTOA HUDUMA ZA USAFIRI WA NDEGE KWA WAFANYAKAZI**
**KUMBUKUMBU NA: 10007995**

Kampuni ya Mafuta Ghafi ya Afrika Mashariki (EACOP) Ltd, ambayo ni Kampuni ya mafuta na gesi, inaalika kampuni au taasisi zenye uzoefu na weledi wa kutosha kuonesha nia ya kutoa huduma ya usafiri wa ndege kwenda kwenye Mradi wa bomba la mafuta ghafi la Afrika mashariki.

Mradi wa EACOP unajumuisha ujenzi na uendeshaji wa bomba la kusafirisha Mafuta lililofukiwa chini ya ardhi linalokatisha mipaka ya nchi mbili na litakalo safirisha mafuta kutoka eneo la Ziwa Albert nchini Uganda mpaka mashariki mwa pwani ya Tanzania kwa ajili ya kusafirisha Mafuta katika masoko ya kimataifa. Bomba litaanzia Kabaale katika Wilaya ya Hoima, nchini Uganda, mpaka Chongoleani, Mkoa waTanga nchini Tanzania. Urefu wa bomba ni kilomita 1,443, kati yake kilomita 1,147 zitakuwa nchini Tanzania.

**MAELEZO MAFUPI YA HUDUMA:**

Huduma za Usafiri wa Ndege:

- Sifa Husika za ndege: Ijulikanayo kitaalamu kama fixed wing, Marubani 2, Injini pacha, Iwe na injini yenye turubo ya kusukuma propela , iwe inazingatia vigezo vya Mamlaka ya Kimataifa ya Usafirishaji wa Anga.
- Viwanja vya Ndege: Dar-es salaam/Tanga au mahali pengine penye kiwanja cha ndege (Kiwanja chenye moramu).
- Ratiba: Safari 2 za Kwenda na kurudi kwa wiki kwenye viwanja vya ndege vilivyotajwa. Safari za kawaida za ndege za abiria zinaweza kuruhusiwa baadae.
- Ratiba ya kuanza: Inakadiriwa kuanza tarehe 1 Desemba 2022.
- Mshahara: Unajumuisha viwango vyote vya malipo kwa kila saa ya kuruka angani.
- Muda: Mwaka mmoja ingawa unaweza kuongezeka

**VIGEZO MUHIMU:**

Makampuni au taasisi zinzoonesha nia zanaalikwa kutuma maombi na kuambatanisha nyaraka zifuatazo:

- Uthibitisho wa usajili wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na cheti cha uthibitisho wa mlipa kodi kwa mwaka wa fedha uliopita.
- Inashauriwa kuwasilisha maombi ya usajili kwenye kanzi data ya EWURA ya Watoa Huduma ya Ugavi wa Ndani (LSSP) wakati wa konesha nia.
- Kuzingatia kanuni za watoa huduma wa ndani za mwaka 2017 na ufafanuzi wa makampuni ya ndani.
- Uzoefu, utendaji na uwezo wa kutoa huduma zilizoorodheshwa hapo juu katika kiwango kikubwa nchini Tanzania, kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.
- Uwezo wa kifedha wa kutoa huduma zinazohitajika ikiwa ni pamoja na kuwasilisha hesabu za fedha za mwaka husika.
- Uthibitisho kutoka kwenye mfumo wa Usimamizi wa QHSE, taasisi na mchakato kulingana na Viwango vya Ndani na vya Ki-Sekta vinavyotumika kwa kazi hii.
- Leseni ya biashara kutoka nchii husika inayothibitisha kufanya kazi hii.
- Vyeti vya ubora wa ndege.
- Wasifu wa marubani na marubani wasaidizi pamoja na wahudumu wengine watakaohusika katika kutoa huduma, ikiwa ni pamoja na vyeti vya lazima vya kila mhudumu, viwango vya elimu, ushahidi wa mafuzo ya mara kwa mara.
- Uthibitisho mwingine wowote wa Kampuni, vibali na leseni.
- Uthibitisho wa kukubaliana na sera za kupinga rushwa, ufisadi, na Haki za Binandamu.

Kampuni zenye nia, ambazo zina uwezo na rasilimali za kutosha kutoa huduma zilizotajwa hapo juu zinapaswa kutuma maombi na kuambatanisha nyaraka zilizotajwa hapo juu kupitia barua pepe ya **procurement.tz@eacop.com** (ukubwa wa barua pepe usizidi **20Mb**) mnamo au kabla ya Tarehe **1 Novemba 2022** saa **12:00 jioni** saa za Afrika Mashariki (EAT). Kichwa cha Barua pepe kiwe **1007995.**

Maombi yote yakuonesha nia yasizidi kurasa **10 hadi 20.**

Maombi yote lazima yawasilishwe kwa lugha ya Kingereza.

**Muhimu:** Mradi wa EACOP utapitia na kuchambua nyaraka zilizotumwa na makampuni yenye nia Kwa ajili ya kutengeneza orodha ya (Makampuni) ya awali yenye vigezo. Mwaliko wa Makampuni kutuma maombi ya zabuni utatumwa kwa makampuni ya awali yenye vigezo baada ya makampuni hayo kusaini Makubaliano ya Utunzaji waTaarifa (NDA).

217107202

# Waziri atoa mwezi tathmini mgogoro wa uwanja wa ndege

**Na Munir Shemweta,**
MWANZA

SERIKALI imetoa mwezi mmoja kuanzia juzi kufanyika tathmini ya kina kwenye eneo lenye mgogoro wa ardhi linalozunguka Uwanja wa Ndege wa Mwanza.

Mgogoro huo unahusisha wananchi na Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania (TAA) na Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ).

Agizo hilo lilitolewa juzi katika kata ya Shibula, wilayani Ilemela na Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, wakati Kamati ya Mawaziri Wanane wa Wizara za Kisekta ilipotembelea eneo hilo ikiwa ni sehemu ya ziara ya kamati hiyo kwenye mikoa mbalimbali nchini kuhusu utatuzi wa migogoro ya matumizi ya ardhi katika vijiji 975.

"Sasa tathmini ya kina itafanyika ndani ya mwezi mmoja. Tunapoondoka hapa wataalamu wa timu ya kitaifa watapita nyumba moja baada ya nyingine kwa mitaa yote kufanya tathmini ya kina tupate majibu," alisema.

Dk. Mabula ambaye ni kiongozi wa Kamati ya Mawaziri hao aliwaambia wananchi kwenye mkutano huo kuwa serikali haikutaka kuchukua uamuzi wa mwaka 2019 moja kwa moja na badala yake imerudi kwa wananchi wa maeneo hayo ili kupata ushauri wa changamoto kabla ya kutoa uamuzi.

"Lengo hapa la kuja kwa timu ya kitaifa kufanya tathmini ni kujua nani ni nani na aliingia kwa wakati gani. Yote yatapatikana ndani ya mwezi mmoja" alisema Waziri Mabula.

Kwa mujibu wa Dk. Mabula, ushauri utakaotolewa na kamati yake baada ya timu ya mkoa kujiridhisha pamoja na kamati ya wataalamu kupitia tena eneo hilo, kamati ya mawaziri itatoa taarifa yenye maslahi kwa Watanzania wote.

Aliitaka timu ya wataalamu kupewa nafasi na ushirikiano ili kufanya kinachostahili ikiwamo kuonyesha uthibitisho mbalimbali kama vile nyaraka na hatua zote za kiserikali zitafutwa.

Kumbukumbu kuhusiana na mgogoro wa ardhi eneo la uwanja wa ndege zinaonyesha kiwanja hicho kilipimwa mwaka 1987 kikiwa na ukubwa wa hekta 1,470 kwa kuzingatia eneo lililokuwa limelipwa fidia kati ya mwaka 1978 hadi 1980

Hata hivyo, mwaka 2003 hadi 2004 TAA ilijenga uzio kuzunguka eneo la kutua na kurukia ndege pamoja na miundombinu iliyopo ili kuimarisha usalama wa kiwanja. Wakati wa ujenzi wa uzio, iligundulika eneo pekee la kiwanja cha ndege lililovamiwa na wananchi lilikuwa mtaa wa Nyagungulu kata ya Ilemela.

Baada ya ujenzi wa uzio, kulitokea tafsiri potofu kwa wananchi wakidhani kuwa mwisho wa mipaka ya kiwanja cha ndege ni uzio huo na kusababisha kuanza kuvamia eneo la kiwanja ambako kuna mitaa ya Mhonze B, Kihili, Nyamilolelwa, Shibula na Bulyankhulu katika kata ya Shibula.



Meneja Masoko wa Halotel, Sakina Makabu (kulia) na Meneja Uhusiano, Stella Pius (kushoto), wakibeba moja kati ya samani walizotoa kwa Shule ya Sekondari ya Bangulo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mfumo kidijitali ufuatiliaji afya za wasafiri waimarishwa

**Na Jenifer Gilla**

SERIKALI imesema imeimarisha mfumo wa ufuatiliaji wa afya za wasafiri kwa safari za ndani ya nchi ili kuongeza ufanisi wa kubaini wasafiri wenye dalili za magonjwa kuhakikisha wanakuwa salama dhidi ya magonjwa ya kuambukiza. Taarifa iliyotolewa na Wizara ya Afya kwa wadau wa usafiri nchini, ikiwamo Mamlaka ya Anga nchini (TCAA) na Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA), ilieleza kuwa imechukua hatua hiyo kutokana na kuwapo kwa milipuko ya magonjwa mara kwa mara duniani ukiwamo wa ebola ilioanzia nchini Uganda.

"Wizara ya Afya inatekeleza afua mbalimbali za kuhakikisha watanzania wanakuwa salama dhidi ya magonjwa ya kuambukiza. Kwa sababu hiyo, Wizara imeanzisha mfumo wa kidijitali wa ufuatiliaji afya za wasafiri wa safari za ndani ya nchi," ilisema taarifa hiyo.

Aidha, taarifa hiyo ilieleza kuwa mfumo huo utamhitaji msafiri kujaza taarifa zake kabla ya safari na kuhakikiwa akiwasili katika viwanja vya ndege, bandari au mipakani ili kudhibiti kusambaa kwa magonjwa hayo ndani ya nchi.

Septemba 28, mwaka huu, Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu alitoa tahadhari ya kuwapo kwa ugonjwa wa ebola katika Wilaya ya Mubende nchini Uganda, umbali wa kilometa 230 hadi Mutukula mkoani Kagera kupitia Masaka.

Ummy alisema uchambuzi uliofanywa na wizara hiyo umeonesha mikoa iliyo hatarini kupata maambukizi ya ugonjwa huo ni Kagera, Mwanza, Kigoma, Geita, Mara, Dar es Salaam, Arusha, Kilimanjaro, Songwe, Mbeya na Dodoma kutokana na mwingiliano wa kibiashara na kijamii.

Kwa mujibu wa taarifa ya waziri huyo, dalili za ugonjwa huo ni homa kali, degedege, kutapika matapishi yenye damu, kuharisha na kutokwa damu machoni. Uchunguzi wa kimaabara umethibitisha kuwapo kwa ugonjwa wa ebola anuai aina ya Sudan (Ebola-Sudan strain).

Aidha, wizara inachukua hatua mbalimbali kuzuia ugonjwa kuingia nchini ikiwamo kuelimisha na kuhamasisha jamii kuchukua tahadhari dhidi ya ugonjwa huo na kuimarisha uchunguzi wa wasafiri katika mipaka hasa yenye mwingiliano mkubwa na nchi ya Uganda.

# Sekondari Bangulo yapata msaada vifaa vya masomo

**Na Mwandishi Wetu**

SHULE ya Sekondari Bangulo jijini Dar es Salaam imepewa msaada wa vifaa mbalimbali vya masomo ili kupunguza tatizo linazowakabili wanafunzi na walimu.

Akitoa msaada huo wa kompyuta, printa, meza, viti na vifaa vya masomo, Mkuu wa Kitengo cha Bidhaa na Mawasiliano wa Kampuni ya Simu ya Halotel, Sakina Makabu, alisema wameamua kusaidia vifaa hivyo kutokana na changamoto zinazoikabili shule hiyo.

Alisema mpango huo ni kuunga mkono juhudi za serikali za kuhakikisha shule zote nchini zinapata mahitaji na vifaa muhimu vitakavyowezesha wanafunzi kupata elimu katika mazingira bora ili kukuza kiwango cha ufaulu wa wanafunzi hao na kupunguza uhaba wa vifaa vya elimu kwa shule zote nchini.

"Halotel tumeamua kutoa msaada huu wa vifaa ambavyo ni meza na viti vya walimu, kabati la vitabu na mafaili, desktop mbili na printer ikiwa ni mojawapo ya mwitikio wa kampuni yetu wa kuitikia juhudi za serikali za uboreshaji wa mazingira na upatikanaji wa vifaa vya ufundishaji na kujifunzia ili kuongeza ufanisi wa kufundishia na kujifunzia katika mfumo wa nadharia na vitendo," aliongeza Sakina.

Kadhalika, alisema inatoa huduma bure ya kimasomo ijulikanayo kama 'Halostudy" ya kujisomea mtandaoni inayowawezesha wanafunzi kusoma mitaala ya masomo mbalimbali nchini kwa njia ya mtandao (TEHAMA) inayopatikana kwenye simu za mkononi na kwenye kompyuta.

Vile vile, alisema kwa sasa wana mpango mpya wa kuboresha zaidi sekta hiyo kidigitali kwa ngazi ya wanafunzi wa vyuo vikuu nchini huduma itakayowawezesha wanafunzi wote vya vyuo vikuu nchini kuwekewa vocha yenye thamani ya Sh. 1,500 kila mwezi.

Kwa upande wake Mkuu wa sekondari hiyo, Hussein Mwamtuya, alisema wamefarijika kupokea msaada huo na kuendelea kuwa karibu na jamii.

Pia kwa kuunga mkono jitihada za kuisaidia sekta ya elimu nchini. "Ninaamini kabisa vifaa hivi vitawasaidia walimu na wanafunzi hapa shuleni katika kuboresha namna ya ufundishaji na kujifunza kwa ujumla".

Kampuni ya Halotel, ilisema itaendelea kushirikiana na serikali pamoja na wadau wengine wa elimu kuhakikisha na kufanikisha kusonga mbele sekta ya elimu ikiwa ni pamoja na kutengeneza wanafunzi bora wanaosoma masomo ya sayansi hasa kuelekea ukuaji wa uchumi wa viwanda.

## Wakazi Fukayosi wafurahia majisafi

**Na Julieth Mkireri,** BAGAMOYO

BAADHI ya wakazi wa Kijiji cha Fukayosi Wilaya ya Bagamoyo, wamesema kukamilika kwa mradi wa maji ni fursa kimaendeleo kwa kuwa wataanzisha bustani na shughuli nyingine zilizokwama kutokana na ukosefu wa maji.

Mradi huo umetekelezwa na Wakala wa Majisafi na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA).

Tabia Ramadhani mkazi wa kijiji hicho, akizungumza na Nipashe alisema, awali kabla ya mradi huo kuna wakati walikuwa wanashinda bila kula kutokana na kukosa maji ya kupikia, nguo chafu za watoto ambazo zilisababisha wakati mwingine kukwama kwenda shule.

Tabia alisema maji waliyokuwa wanategemea yalikuwa yanakatika mara kwa mara na wakati mwingine kutopatikana kwa wiki mbili na zaidi na hivyo kutumia maji ya kwenye lambo ambayo hayakuwa salama kwa afya.

Kibibi Athumani, aliishukuru RUWASA kwa kujenga mradi huo ambao umewaondolea vikwazo walivyokuwa wakikumbana navyo ikiwamo cha kuchelewa kukamilisha kazi za nyumbani na watoto kushindwa kula kwa wakati.

Mwenyekiti wa kijiji hicho, Rajab Mkecha, alisema maji waliyokuwa wanatumia awali ni ya Wakala wa Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA) ambayo yalikuwa yakikatika muda mrefu.

Alisema kutokana na hali hiyo wananchi walilazimika kununua dumu la lita 20 kwa Sh. 500 ambayo hata hivyo yalikuwa hayakidhi mahitaji.

Mkecha alisema mradi huo wa RUWASA umefanikisha ujenzi wa vituo vinne vya kuchotea maji ambavyo vinatoa muda wote na ni karibu na makazi ya wengi.

Meneja wa RUWASA Wilaya ya Bagamoyo, Mhandisi James Kionaumela, alisema chanzo chake ni maji kutoka bomba la DAWASA na kwamba fedha za mradi huo ni kutoka katika Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano dhidi ya UVIKO-19.

Mhandisi Kionaumela alisema gharama za mradi huo ni Sh. 350,344,596 na kwamba wanafanyakazi ya kuhudumia wananchi 2,242 sawa na kaya 374 kwa umbali usiozidi mita 400.

**Mwenyekiti wa kijiji hicho, Rajab Mkecha, alisema maji waliyokuwa wanatumia awali ni ya Wakala wa Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA) ambayo yalikuwa yakikatika muda mrefu.**

# Kongamano la Azaki kujadili mabadiliko ya tabianchi

**Na Mary Geofrey**

WASHIRIKI 500 kutoka mashirika 28 ya ndani na nje ya nchi, wanatarajia kushiriki kongamano la Wiki ya Asasi za Kiraia (AZAKI), mkoani Arusha, kujadili mambo mbalimbali ikiwamo mabadiliko tabianchi.

Mkurugenzi Mtendaji wa FCS, Francis Kiwanga, akizungumza na waandishi wa habari juzi jijini Dar es Salaam, alisema kwenye kongamano la Wiki ya AZAKI 2022, litafanyika kuanzia Oktoba 24 hadi 28, mwaka huu.

Alisema watajadili pia ajenda fursa na changamoto za maendeleo kijamii na kutoa msaada wa kisheria kwa wananchi, ushauri na kupokea maoni kwa makundi ya wanawake, vijana na wazee.

Alisema kaulimbiu ya mwaka huu 'Maendeleo ya Watu na Simulizi za Watu', inalenga kubadilisha uzoefu, kubaini fursa na kusikiliza changamoto kutoka kwa wananchi ikiwamo kutafuta mbinu za kukuza uchumi.

"Kupitia mkutano huu tutaangazia mbinu, mikakati na fursa za watu, tutazumgumza na watu pamoja na ajenda nyingine pia tutajadili mabadiliko ya tabianchi ambayo husababisha ukame katika maeneo mbalimbali duniani," alisema Kiwanga.

Mkurugenzi Mkazi wa Shirika la Norwegian Church Aid (NCA), Berte Marie Ulveseter, alisema kwa kipindi cha miaka 10 iliyopita shirika hilo, limetoa zaidi ya mikopo 5,000 ya kijamii kwenye vikundi vilivyo na watu 100,000.

Alisema wametoa ruzuku zaidi ya Dola za Kimarekani 21,000 (Sh. bilioni 50), na kuwawezesha wazalishaji 500 wanaoongeza mnyororo wa thamani wa bidhaa za ufugaji na mboga kutoka wilaya 10, Tanzania.

Naye Mratibu wa Wiki ya AZAKI 2022, Dk. Shirley Mushi, alisema usajili wa ushiriki mwaka huu ulifanyika kwa njia ya mtandao na hadi sasa asilimia 90 wanaotarajia kushiriki walikuwa wamejiandikisha.

Dk. Mushi alisema, ajenda ya Wiki ya AZAKi 2022 itaelekezwa katika kuhakikisha watendaji wa sekta mbalimbali wanaimarisha ushirikiano na uhusiano unaolenga kuleta maendeleo.




Wafanyakazi wa gari la kuzoa taka wakifanya shughuli zao katika eneo la Makumbusho, Manispaa ya Kinondoni, Dar es Salaam hivi karibuni, bila ya kuvaa vifaa vya kujikinga mikononi 'gloves' kitendo kinachoweza kuhatarisha usalama wa afya zao. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Mkemia Mkuu akabidhi kemikali za maabara vifaa, vitabu Handeni

**Na Mary Geofrey**

MAABARA ya Mkemia Mkuu wa Serikali (GCLA), imekabidhi msaada wa kemikali za maabara na vitabu 786 vya masomo ya sayansi ya kidato cha tano na sita, wilayani Handeni mkoani Tanga.

Lengo la vitabu hivyo ni kuwezesha wanafunzi kufanya vyema kwenye masomo ya sayansi na kemia, katika kuendana na kasi ya dunia ya sayansi na teknolojia.

Mkuu wa Wilaya ya Handeni, Siriel Mchembe, akipokea msaada huo jana katika Shule ya Sekondari Mkata, wilayani humo, aliwataka wanafunzi kujitahidi kusoma masomo ya sayansi kutokana na dunia kuendeshwa na mapinduzi ya sayansi na teknolojia.

"Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali imetupatia msaada huu, ili kuhakikisha wanafunzi wetu wanajifunza na kupenda masomo ya sayansi na kuendana na maendeleo ya dunia ya sasa ambayo inaendeshwa kwa mabadiliko ya kila siku ya sayansi na teknolojia," alisema Mchembe.

Aliwataka wazazi kuhamasisha watoto kusoma masomo ya sayansi ikiwamo biolojia, fizikia, kemia na hisabati kwa lengo la kuinua kiwango cha elimu katika masomo ya sayansi na kutengeneza kizazi cha wataalamu wengi wa sayansi kwa nchi.

Naye Mkemia Mkuu wa Serikali, Dk. Fidelice Mafumiko, aliwakumbusha wanafunzi hao kuwa, sayansi na teknolojia ndiyo zinaleta maendeleo na jukumu la serikali ni kuwajengea madarasa, kupanga walimu na vifaa vya kusomea.

"Tuna matumaini vitabu hivi vya sayansi na kemikali za maabara vitaisaidia shule hii kujenga wataalamu wa sayansi hasa ukizingatia serikali inaweka juhudi ili nchi yetu kufikia uchumi wa juu katika sayansi na teknolojia.

Aidha, ni muhimu kuwekeza katika rasilimali watu na kujenga Watanzania wenye weledi. Nasi tutaendeleza lengo letu ambalo ni kuendelea kuwezesha vijana kufikia malengo yao kupitia elimu," alisema.

## TANGAZO

BancABC part of atlasmara

# UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA KWA UMMA

## IMETOLEWA CHINI YA KANUNI YA 7 NA YA 8 YA KANUNI ZA MABENKI NA TAASISI ZA FEDHA (UONESHAJI) YA MWAKA 2014

### WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 30 SEPTEMBA 2022 (Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo Mwaka ya /Mwaka wa sasa 30-Sep-22 | Robo Mwaka/Mwaka uliopita 30-Jun-22 |
|---|---|---|---|
| **A** | **MALI** | | |
| 1 | Fedha Taslimu | 4,611 | 5,460 |
| 2 | Salio Katika Benki Kuu ya Tanzania | 12,194 | 13,727 |
| 3 | Uwekezaji Katika Amana za Serikali | 40,023 | 43,355 |
| 4 | Salio Katika Benki Nyingine na Taasisi za Fedha | 9,759 | 10,854 |
| 5 | Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | 59 | 41 |
| 6 | Miamala Baina ya Matawi | - | - |
| 7 | Bili Zilizoafikiwa | - | - |
| 8 | Dhima za Wateja Zilizokubalika | - | - |
| 9 | Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | 98,523 | 95,419 |
| 10 | Uwekezaji Katika Amana Nyingine | - | - |
| 11 | Mikopo Halisi Iliyopo | 128,241 | 129,371 |
| | | - | - |
| 12 | Mali Nyingine | 28,051 | 26,707 |
| 13 | Uwekezaji wa Hisa | 1,000 | 1,000 |
| 14 | Akaunti za udhamini | - | - |
| 15 | Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 2,450 | 2,602 |
| **16** | **JUMLA YA MALI** | **324,911** | **328,537** |
| **B** | **DHIMA** | | |
| 17 | Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | 67,330 | 66,812 |
| 18 | Amana za Wateja | 139,084 | 142,008 |
| 19 | Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | - | - |
| 20 | Amana Maalumu | - | - |
| 21 | Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | - | - |
| 22 | Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | - | - |
| 23 | Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | - | - |
| 24 | Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | - | - |
| 25 | Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | - | - |
| 26 | Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitakazolipwa Baadae | (0) | - |
| 27 | Dhima Nyingine | 2,185 | 3,749 |
| 28 | Madeni | 90,840 | 89,996 |
| **29** | **JUMLA YA DHIMA** | **299,439** | **302,565** |
| **30** | **MALI/(DHIMA) HALISI (16 kutoa 29)** | **25,472** | **25,972** |
| **C** | **FEDHA ZA WANAHISA** | | |
| 31 | Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 122,954 | 122,954 |
| 32 | Akiba ya Mtaji | 2,163 | 2,163 |
| 33 | Mapato Yaliyobakizwa | (99,334) | (99,334) |
| 34 | Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | (1,300) | (800) |
| 35 | Akaunti Nyingine za Mtaji | 988 | 988 |
| 36 | Stahiki ya Wenyehisa Chache | - | - |
| **37** | **JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **25,472** | **25,972** |
| 38 | Dhima Zisizo Dhahiri | 413 | 351 |
| 39 | Mikopo Chechefu | 18,247 | 18,678 |
| 40 | Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 11,856 | 11,856 |
| 41 | Mali Nyingine Chechefu | - | - |
| **D** | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| (I) | Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 7.84% | 7.91% |
| (ii) | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 13.03% | 13.23% |
| (iii) | Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 67.87% | 67.63% |
| (iv) | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 39.47% | 39.38% |
| (v) | Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 46.40% | 46.34% |
| (vi) | Ongezeko la Amana | -1.15% | 0.65% |
| (vii) | Ongezeko la Mali | -1.10% | -5.85% |

### TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 30 SEPTEMBA 2022 (Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo ya Mwaka sasa 30-Sep-22 | Robo ya mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita 30-Sep-21 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 30-Sep-22 | Limbikizo la Mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) 30-Sep-21 |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Mapato ya Riba | 10,161 | 10,246 | 30,327 | 30,311 |
| 2 | Gharama za Riba | (4,889) | (5,190) | (14,764) | (14,976) |
| **3** | **Mapato Halisi ya Riba (1kutoa 2)** | **5,271** | **5,057** | **15,563** | **15,335** |
| 4 | Madeni Viza Yaliyofutwa | 536 | 206 | - | 319 |
| 5 | Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | - | - | 1,160 | - |
| **6** | **Mapato Yasiyo ya Riba:** | **1,856** | **1,163** | **4,697** | **3,454** |
| 6.1 | 6.1 Faida /(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | 266 | 192 | 652 | 699 |
| 6.2 | 6.2 Ada na Kamisheni | 304 | 249 | 856 | 682 |
| | 6.3 Gawio | - | 35 | - | 35 |
| 6.3 | 6.4 Mapato Mengine | 1,285 | 687 | 3,189 | 2,038 |
| **7** | **Gharama Zisizo za Riba:** | **(8,032)** | **(7,961)** | **(22,524)** | **(22,496)** |
| | 7.1 Mishahara na Mafao | (2,760) | (2,510) | (7,920) | (7,608) |
| | 7.2 Ada na Kamisheni | - | - | - | - |
| | 7.3 Gharama Nyingine | (5,272) | (5,451) | (14,604) | (14,888) |
| **8** | **Faida /(Hasara) ya Uendeshaji** | **(369)** | **(1,535)** | **(1,104)** | **(3,388)** |
| 9 | Tengo la Kodi ya Mapato | (131) | - | - | - |
| **10** | **Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **(500)** | **(1,545)** | **(1,300)** | **(3,511)** |
| 11 | Mapato Mengine Yaliyojumuishwa (bainisha) | - | - | - | - |
| **12** | **Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa mwaka** | **(500)** | **(1,545)** | **(1,300)** | **(3,511)** |
| 13 | Idadi ya Waajiriwa | 178 | 168 | 178 | 168 |
| 14 | Mapato kwa Hisa | (0.20) | (0.63) | (0.13) | (0) |
| 15 | Mapato yaliyopatikana kwa Kushiriki | - | - | - | - |
| 16 | Idadi ya Matawi | 6 | 6 | 6 | 6 |
| | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | | | |
| (I) | Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | -0.61% | -0.62% | -0.53% | -2.11% |
| (ii) | Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | -7.77% | -5.62% | -6.74% | -19.15% |
| (iii) | Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 112.69% | 128.72% | 111.17% | 119.96% |
| (iv) | Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | 2.92% | 0.96% | 2.87% | 2.92% |

### TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA ROBO/MWAKA ULIOISHIA 30 SEPTEMBA 2022 (Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo Mwaka ya sasa 30-Sep-22 | Robo Mwaka iliyopita 30-Jun-22 |
|---|---|---|---|
| **I** | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji:** | | |
| | Mapato/(Hasara) Halisi | (369) | (163) |
| | Marekebisho kwa Ajili ya: | - | - |
| | - Hasara Katika Mali | 758 | 815 |
| | - Badiliko Halisi Katika Mikopo | 1,130 | 243 |
| | - Faida/Hasara Kwenye Mauzo ya Mali | - | - |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Amana | (2,406) | 1,350 |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi Zilizoafikiwa | 3,332 | 907 |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | (1,564) | (10,355) |
| | -Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | (1,362) | (1,479) |
| | - Kodi Iliyolipwa | (131) | - |
| | - Mengineyo (bainisha) | - | - |
| | **Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji** | **(613)** | **(8,682)** |
| **II** | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji:** | - | - |
| | Gawio Lililopokewa | - | - |
| | Ununuzi wa Mali za Kudumu | (605) | 2,708 |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | - | - |
| | Ununuzi wa Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - |
| | Mengineyo (bainisha) | - | - |
| | **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji** | **(605)** | **2,708** |
| **III** | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Kifedha:** | | |
| | Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | - | - |
| | Gawio Lililolipwa kwa Fedha Taslimu | - | - |
| | Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | 844 | (11,243) |
| | Mengineyo (bainisha) | - | - |
| | **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Kifedha** | **844** | **(11,243)** |
| | | - | - |
| **IV** | **Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu:** | - | - |
| | Ongezeko / Punguzo Halisi Katika Fedha taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu | (373) | (17,217) |
| | Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Robo Mwaka/Mwaka | 125,461 | 142,677 |
| | **Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Robo Mwaka/Mwaka** | **125,087** | **125,461** |

### TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA 30 SEPTEMBA 2022

| | Mtaji wa Hisa | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato Yaliyobakizwa | Ziada ya Kisheria | Tengo la Ziada ya Jumla | Mengineyo | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Mwaka wa sasa** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | **122,954** | **-** | **(99,334)** | **2,163** | **0** | **989** | **26,972** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | (1,300) | - | - | - | (1,300) |
| Hisa za upendeleo | - | | | | | | |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | - | - | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **122,954** | **-** | **(100,633)** | **2,163** | **0** | **989** | **25,472** |
| | - | - | - | - | - | - | (0) |
| **Mwaka Uliopita** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | **122,954** | **-** | **(89,329)** | **1,715.64** | **0** | **989** | **36,329** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | (9,357) | - | - | - | (9,357) |
| Hisa za upendeleo | - | - | - | - | - | - | |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | (447) | 447 | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **122,954** | **-** | **(99,334)** | **2,163** | **0** | **989** | **26,972** |

| | Jina | Sahihi | Tarehe |
|---|---|---|---|
| Ofisa Mtendaji Mkuu | I. John | | 21-Oct-22 |
| Mkuu wa Fedha | H. Kharbush | | 21-Oct-22 |
| Mkaguzi Mkuu wa Ndani | J. Kilato | | 21-Oct-22 |

Sisi, tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi, tunathibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi, na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na Viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006, na zinaonesha hali halisi

| | Jina | Sahihi | Tarehe |
|---|---|---|---|
| 1 Mkurugenzi | P. Ishengoma | | 21-Oct-22 |
| 2 Mkurugenzi | Mr.R. Dave | | 21-Oct-22 |

217107102



# Neema wakulima, tani 100 za mbolea zikiwasili nchini

**Na Godfrey Mushi,** ARUSHA

WAKULIMA wanaozalisha mazao ya chakula na biashara katika mikoa ya Arusha na Kilimanjaro, wamepata ahueni ya viuatilifu, baada ya tani 100 za mbolea kutoka nchi jirani ya Kenya kuwasili nchini.

Kwa miaka kadhaa sasa wakulima wa Tanzania wamekuwa wakilalamikia tatizo la kupaa kwa bei kiholela na kuwapo kwa urasimu wa upatikanaji wa mbolea.

Mbolea hiyo itakayosambazwa na kuwafikia wakulima vijijini wakati wowote kuanzia sasa, ni matokeo ya makubaliano yaliyofikiwa hivi karibuni, kati ya Rais Samia Suluhu Hassan (Tanzania) na William Ruto (Kenya), ya kuondoa vikwazo 14 vya kibiashara vilivyokuwa vikidhoofisha ukuaji wa maendeleo ya kiuchumi katika mataifa hayo mawili.

Jana, Kaimu Meneja wa Kampuni ya Mbolea nchini (TFC), Kanjeli Mroba, alisema ujio wa mbolea hiyo unalenga zaidi kuwasaidia wakulima kuongeza tija ya uzalishaji wa mazao yao na kuwasogeza kiuchumi kutokana na nafuu ya mbolea.

“Hii mbolea itakuwa inauzwa kwa bei nafuu, mkulima atakuwa na uwezo wa kumudu gharama. Huu ni mwanzo tu wa utekelezaji wa makubaliano ya viongozi wetu hao wawili. Kwa pamoja walikubaliana kuondoa vikwazo hivyo, vilivyochangia kurozotesha biashara baina ya pande zote mbili. “TFC matamanio yetu ni kumuona mkulima akinufaika kupitia sekta ya kilimo, na ndiyo maana tukaona tuangalie fursa kutoka sehemu nyingine, ambapo tutapata mbolea kwa urahisi zaidi na mkulima wetu kuweza kuimudu gharama zake.”

Katika taarifa yake, Kanjeli, ameeleza kuwa licha ya serikali kutoa ruzuku ya zaidi ya Sh. bilioni 150 ili kuwezesha unafuu wa mbolea, TFC waliona ni vyema kutafuta mbolea ambayo inaweza kutumika kwa kazi zaidi ya moja. Mbolea hiyo kutoka nchini Kenya, ni mahususi kwa ajili ya kupandia na kukuzia mazao.

Alisema tayari mbolea hiyo tani 30 zimeshapelekwa Mkoa wa Mbeya na kuanza kusambazwa kwa wakulima, ili kuongeza chachu ya kufikiwa kwa mapinduzi makubwa ya sekta ya kilimo nchini.

Mkurugenzi wa Kampuni ya Mbolea ya SBL kutoka nchini Kenya, Joe Kariuki, alisema kampuni hiyo imelenga kuwainua wakulima wa Tanzania, kwa kuwauzia mbolea hiyo kwa gharama nafuu ili kupunguza gharama za uzalishaji.

“Ni matumaini yetu kuwa tunapoenda kuuza mbolea kwa gharama nafuu, hata wakulima watapunguza gharama kwenye uzalishaji nikimaanisha hata mazao yataenda kuuzwa kwa bei nafuu tofauti na ilivyo kwa sasa,”alisema.

Mkurugenzi huyo alieleza kuwa kwa sasa mazao yamekuwa yakiuzwa kwa bei ghali, kutokana na mbolea kuuzwa bei ya juu, ndiyo maana kampuni hiyo imekuja na suluhisho la tatizo hilo kwa wakulima.

# Waliopisha ujenzi nyumba za askari Babati walilia fidia

**Na Allan Isack,** BABATI

WANANCHI wa Bagara Ziwani katika Wilaya ya Babati, mkoani Manyara, wamesema wanasubiri kauli ya serikali kuhusu malipo yao ya fidia ya ardhi waliyotoa kwa ajili ya kupisha ujenzi wa makazi ya nyumba ya askari wa Jeshi la Polisi.

Kilio cha wananchi hao kilitolewa jana, wilayani humo kupitia barua yao ya wazi kwenda kwa Mkuu wa Mkoa huo, Makongoro Nyerere.

Akifafanua zaidi kuhusu barua hiyo, kiongozi wa wananchi hao wanaodai fidia, Fita Giderege, alisema wameamua kupaza sauti hiyo, kwa sababu sasa ni muda mrefu umepita tangu walipotoa mashamba yao kupisha ujenzi huo.

“Sisi tulitoa ardhi yetu, baada ya Halmashauri ya Mji wa Babati, kutusihi kutoa mashamba yetu ili kupisha ujenzi makazi ya askari wa Jeshi la Polisi Mkoa wa Manyara.

“Ndiyo maana tunakumbushia, tukiiomba serikali kusikia kilio chetu na wahakikishe tunalipwa haki zetu, kwa kuwa tulitoa mashamba kwa makubaliano watulipe fidia kupisha ujenzi wa makazi ya nyumba za askari polisi,” alisema.

Kwa mujibu wa wananchi hao, hivi sasa wamezuiwa na serikali kutumia maeneo hayo kama kufanya shughuli za kilimo na ufugaji, kwa kuwa tayari ni ardhi iliyotengwa kwa shughuli za serikali.

Alipoulizwa kuhusu madai hayo, Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa huo, John Konki, alisema walifanya jitihada ya kufikisha maombi hayo kwa halmashauri hiyo, bila ya kupata mafanikio yoyote.

“Mimi kama kiongozi wa mtaa huu kwa kushirikiana na wananchi wangu tulipeleka maombi yetu kwa halmashauri lakini hadi sasa hakuna mafanikio yoyote, hivyo tunaiomba serikali iingilie kati tulipwe madai yetu,” alisema.

Akizungumzia madai hayo kwa njia ya simu, Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Mji wa Babati, Anna Fisso, alisema serikali imejipanga kuwafidia wananchi hao, hivyo aliwataka kuwa wavumilivu kwa kuwa suala hilo linafanyiwa kazi.

BancABC part of atlasmara

## MINIMUM DISCLOSURES OF BANK CHARGES AND FEES


| | PRICING (TZS) | PRICING (US $ / EUR) | PRICING (GBP) |
|---|---|---|---|
| **PERSONAL BANKING** | | | |
| **SAVINGS ACCOUNT** | | | |
| **IZZE** | | | |
| Account Opening Fee | Free | NA | NA |
| Opening balance | Free | NA | NA |
| Minimum Operating Balance | NIL | NA | NA |
| Minimum Interest Bearing Balance | TZS 10,000.00 | NA | NA |
| Monthly Service Fee | Free | NA | NA |
| **FAHARI** | | | |
| Account Opening Fee | Free | Free | Free |
| Opening balance | TZS 10,000.00 | $ 50.00 | £ 50.00 |
| Minimum Operating Balance | TZS 10,000.00 | $ 50.00 | £ 50.00 |
| Minimum Interest Bearing Balance | TZS 50,000.00 | $ 100.00 | £ 100.00 |
| Monthly Service Fee | TZS 1,500.00 | $ 2.00 | £ 2.00 |
| **MWANGAZA JUNIOR ACCOUNT** | | | |
| Account Opening Fee | Free | Free | Free |
| Opening balance | TZS 20,000.00 | $ 50.00 | £ 50.00 |
| Minimum Operating Balance | TZS 20,000.00 | $ 50.00 | £ 50.00 |
| Minimum Interest Bearing Balance | TZS 20,000.00 | $ 500.00 | £ 500.00 |
| Monthly Service Fee (1 free w/drawal per quarter) | Free | Free | Free |
| Extra fee for more than 1 w/drawal per quarter | TZS 5,500.00 | $ 2.00 | £ 2.00 |
| **WEKEZA SAVINGS ACCOUNT (BALANCE BUILD UP)** | | | |
| Account Opening Fee | Free | Free | N/A |
| Opening balance | Free | Free | N/A |
| Minimum Operating Balance | NIL | NIL | N/A |
| Minimum Interest Bearing Balance | TZS 100,000.00 | $ 25.00 | N/A |
| Monthly Service Fee* | Free | Free | N/A |
| **CURRENT ACCOUNT** | | | |
| **AMANA** | | | |
| Account Opening Fee | Free | N/A | N/A |
| Opening balance | TZS 20,000.00 | N/A | N/A |
| Minimum Operating Balance | TZS 3,000.00 | N/A | N/A |
| Minimum Interest Bearing Balance | N/A | N/A | N/A |
| Monthly Service Fee* | TZS 3,000.00 | N/A | N/A |
| **MARIDHAWA** | | | |
| Account Opening Fee | Free | Free | Free |
| Opening balance | TZS 25,000.00 | $ 25.00 | £ 25.00 |
| Minimum Operating Balance | TZS 6,000.00 | $ 5.00 | £ 5.00 |
| Minimum Interest Bearing Balance | NA | NA | N/A |
| Monthly Service Fee* | TZS 10,000.00 | $ 10.00 | £ 10.00 |
| **PREMIUM** | | | |
| Account Opening Fee | Free | Free | Free |
| Opening balance | TZS 35,000.00 | $ 30.00 | £ 30.00 |
| Minimum Operating Balance | NIL | NIL | NIL |
| Minimum Interest Bearing Balance | NA | NA | NA |
| Monthly Service Fee* | TZS 15,000.00 | $ 10.00 | £ 10.00 |
| **SME BANKING** | | | |
| **AMANA BIZ ACCOUNTS** | | | |
| Account Opening Fee | Free | Free | Free |
| Opening balance | TZS 50,000.00 | $ 50.00 | £ 50.00 |
| Minimum Operating Balance | TZS 50,000.00 | $ 100.00 | £ 100.00 |
| Minimum Interest Bearing Balance | NA | NA | NA |
| Monthly Service Fee* | TZS 15,000.00 | $ 15.00 | £ 15.00 |
| **SME TIERED CURRENT ACCOUNT** | | | |
| Account Opening Fee | Free | Free | NA |
| Opening balance | TZS 100,000.00 | $ 100.00 | NA |
| Minimum Operating Balance | TZS 1,000,000.00 | $ 1,000.00 | NA |
| Minimum Interest Bearing Balance | TZS 5,000,000.00 | $ 5,000.00 | NA |
| Monthly Service Fee* | TZS 20,000.00 | $ 15.00 | NA |
| **JAMII CURRENT ACCOUNT** | | | |
| Account Opening Fee | Free | Free | Free |
| Opening balance | Free | Free | Free |
| Minimum Operating Balance | TZS 100,000.00 | $ 100.00 | £ 100.00 |
| Minimum Interest Bearing Balance | TZS 5,000,000.00 | $ 50,000.00 | £ 50,000.00 |
| Monthly Service Fee* | Free | Free | Free |
| **CORPORATE BANKING** | | | |
| **CORPORATE CURRENT ACCOUNTS** | | | |
| Account Opening Fee | Free | Free | Free |
| Opening balance | TZS 500,000.00 | $ 250.00 | £ 250.00 |
| Minimum Operating Balance | NIL | NIL | NIL |
| Minimum Interest Bearing Balance | NA | NA | NA |
| Monthly Service Fee* | TZS 25,000.00 | $ 20.00 | £ 15.00 |
| **CORPORATE CALL ACCOUNTS** | | | |
| Account Opening Fee | Free | Free | Free |
| Opening balance | TZS 10,000,000.00 | $ 10,000.00 | £ 10,000.00 |
| Minimum Operating Balance | TZS 10,000,000.00 | $ 10,000.00 | £ 10,000.00 |
| Minimum Interest Bearing Balance | TZS 1.00 | $ 1.00 | £ 1.00 |
| Monthly Service Fee* | TZS 20,000.00 | $ 20.00 | £ 15.00 |
| **CORPORATE TIERED INTEREST ACCOUNTS** | | | |
| Account Opening Fee | Free | Free | NA |
| Opening balance | TZS 500,000.00 | $ 250.00 | NA |
| Minimum Operating Balance | NIL | NIL | NA |
| Minimum Interest Bearing Balance | TZS 50,000,000.00 | $ 100,000.00 | NA |
| Monthly Service Fee* | TZS 25,000.00 | $ 20.00 | NA |
| **GENERAL CHARGES** | | | |
| Bankers Cheque | TZS 50,000.00 | $ 25.00 | N/A |
| DISHONORED/UNPAID CHEQUE | | | |
| Fund related | TZS 120,000.00 | $ 50.00 | N/A |
| Technical | TZS 30,000.00 | $ 50.00 | N/A |
| **Cheque book Processing Fee:** | | | |
| 25 leaves | TZS 15,000.00 | $ 15.00 | £ 15.00 |
| 50 leaves | TZS 25,000.00 | $ 20.00 | £ 20.00 |
| 100 leaves | TZS 50,000.00 | $ 35.00 | £ 35.00 |
| Uncollected cheque book after 3 months | TZS 15,000.00 | $ 15.00 | £ 15.00 |
| 3rd party encashment (with 3rd party indemnity) | TZS 25,000.00 | 1% Per Cheque + $20 | 1% Per Cheque +$20 |
| Stop Payment Charges | TZS 30,000.00 | $ 25.00 | £ 25.00 |
| **TRANSACTIONAL SERVICE FEES** | | | |
| **With banks via Standing Orders** | | | |
| Standing Order - internal same customer ( set up fee - once off) | Free | Free | Free |
| Standing Order - internal other customers ( per transaction) | Free | Free | Free |
| Standing Order - Other local bank | TZS 20,000.00 | $ 10.00 | £ 10.00 |
| Amendment | Free | Free | Free |
| **DEPOSIT/WITHDRAWAL TRANSACTIONS:** | | | |
| Cash Deposit at Branch | Free | Free | Free |
| Cash Deposit at Branch coins above 100,000 | 5% Min 10,000 | NA | NA |
| Cash Deposit at Branch small denominations less than 50USD (USD 1,2,5,10,20) equal and above USD 500 | NA | 3% of FCY currency value | 3% of FCY currency value |
| With Account Transfers (Internal) | Free | Free | Free |
| Cheque deposit | Free | Free | Free |
| Cash withdrawal Personal Banking ( over the counter) up to 2m | TZS 3,500.00 | 1% Min 5 | 1% min 5 |
| Cash withdrawal Personal Banking ( over the counter) btn 2m to 20m | TZS 4,000.00 | 1% Min 5 | 1% min 5 |
| Cash withdrawal Personal Banking ( over the counter) above 20m | 0.15% Max 50,000 | 1% Min 5 | 1% min 5 |
| Cash withdrawal SME ( over the counter) | 0.15%Min 3,000 Max 20,000 | 1% Min 5 | 1% min 5 |
| Cash withdrawal Corporate Banking | 0.15%Min 3,000 Max 100,000 | 1% Min 5 | 1% min 5 |
| Deposit charges - Financial Institution. | Free | Free | Free |
| Deposit charges - Financial Institution - small denominations | Free | 3%On small denominations above $500 | 3%On small denominations above $500 |
| Account Closure | TZS 10,000.00 | $ 10.00 | £ 10.00 |
| Dormant Account Reactivation | NIL | NIL | NIL |
| Dormant Account monthly fee | NIL | NIL | NIL |
| Premature/cancellation fixed deposit fee | 50% Accrued Interest is Forfeited. Breaking 1st month all interest forfeited | 50% Accrued Interest is Forfeited. Breaking 1st month all interest forfeited | 50% Accrued Interest is Forfeited. Breaking 1st month all interest forfeited |
| Monthly statements | Free | Free | Free |
| Interim Statements (per page) | TZS 2,000.00 | $ 1.00 | £ 1.00 |
| Search fee documents (after 3 months) | TZS 80,000.00 | $ 40.00 | £ 40.00 |
| Audit confirmation | TZS 75,000.00 | $ 50.00 | £ 50.00 |
| Balance Certificate | TZS 50,000.00 | $ 30.00 | £ 30.00 |
| Reference Letter | TZS 50,000.00 | $ 30.00 | £ 30.00 |
| Inter Account Transfers | Free | Free | Free |
| T T Outward local - TISS | TZS 11,800.00 | $ 10.00 | N/A |
| T T Outward local - EFT | TZS 3,000.00 | N/A | N/A |
| T T Inward local TISS | Free | Free | N/A |
| Salary processing (per entry) | TZS 1,500.00 | $ 1.00 | £ 1.00 |
| International Outward T T | N/A | $50 + Other overseas bank chrges | $50 + Other overseas bank chrges |
| International Inward T T | N/A | Free | Free |
| Travellers Chq. Deposit | N/A | N/A | N/A |
| Foreign BankDrafts | N/A | $ 50.00 | £ 30.00 |
| Outward Cheque for Collection | N/A | N/A | N/A |
| Outward Bills for collection | N/A | 0.25% min 50 + $ 50 (courier charge) | 0.25% min 50 + $ 50 (courier charge) |
| Inward Bills for Collection | N/A | 0.25% MIN 50 | 0.25% MIN 50 |
| Advising fee (Inward Bill & LCs ) | N/A | $ 200.00 | £ 200.00 |
| Travellers Chq. (Issue) | N/A | N/A | N/A |
| Letters of Credit | N/A | 1% per qtr + $ 50 (total min $250) | 1% per qtr + $ 50 (total min $250) |
| Bank Guarantees | 1% Per Qtr Min $ 200 | 1% Per Qtr Min $ 200 | 1% Per Qtr Min $ 200 |

**AGENCY BANKING FEE**

| | |
|---|---|
| !"#$%&'( | Free |

**Withdrawal Fees**

| Transaction tiers | BancABC Fees | Government Levy | Total Fees |
|---|---|---|---|
| 100-2999 | 300 | 10 | 310 |
| 3,000-3,999 | 300 | 14 | 314 |
| 4,000-4,999 | 300 | 27 | 327 |
| 5,000-6,999 | 500 | 54 | 554 |
| 7,000-9,999 | 500 | 56 | 556 |
| 10,000-14,999 | 600 | 102 | 702 |
| 15,000-19,999 | 600 | 195 | 795 |
| 20,000-29,999 | 600 | 306 | 906 |
| 30,000-39,999 | 700 | 351 | 1,051 |
| 40,000-49,999 | 800 | 419 | 1,219 |
| 50,000-99,999 | 900 | 573 | 1,473 |
| 100,000-199,999 | 1,000 | 707 | 1,707 |
| 200,000-299,999 | 1,100 | 821 | 1,921 |
| 300,000-399,999 | 1,200 | 838 | 2,038 |
| 400,000-499,999 | 1,200 | 982 | 2,182 |
| 500,000-599,999 | 2,000 | 1,245 | 3,245 |
| 600,000-699,999 | 2,000 | 1,532 | 3,532 |
| 700,000-799,999 | 2,000 | 1,700 | 3,700 |
| 800,000-899,999 | 2,000 | 1,500 | 3,500 |
| 900,000-1,000,000 | 2,000 | 1,776 | 3,776 |
| 1,000,001-2,000,000 | 2,300 | 1,875 | 4,175 |
| 2,000,001-3,000,000 | 2,500 | 1,875 | 4,375 |





## Prof. Mkenda aagiza fedha za jimbo kununua mashine kurudufu mitihani

**Na Anjela Mhando,** ROMBO

WAZIRI wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda, amesema fedha za mfuko wa Jimbo la Rombo, lililoko mkoani Kilimanjaro, zitumike kununua mashine ya kunakilisha maneno na kudurufu mitihani ya Shule ya Sekondari Mawanda.

Alitoa agizo hilo jana alipokuwa akizungumza na wananchi wa Mawanda waliofika katika shule hiyo. Pia aliahidi kuchangia mifuko 20 ya saruji kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu yake.

"Nimeguswa kuisaidia shule hii yenye mchepuo wa sayansi na sanaa, kuwa na vifaa hivyo ambavyo ni mashine ya kunakilisha na mashine ya kudurufu ili kuboresha ufaulu na kuwapa motisha walimu kufanya kazi katika mazingira wezeshi,"alisema.

Aidha, Prof. Mkenda, aliagiza Idara ya Elimu ya Halmashauri ya Wilaya ya Rombo, kuchangia Sh. 100,000 za ununuzi wa vifaa hivyo, kwa kuwa shule hiyo ya Mawanda inatakiwa kufanya vizuri kama shule nyingine.

"Endapo shule hii itapata mashine hizo kwa ajili ya kuchapishia mitihani, itasaidia kwa sababu inawezesha shule kufanya mitihani mingi na mazoezi ya kila wakati, jambo ambalo litawasaidia kuongeza ufaulu kwa wanafunzi wengi," alisisitiza.

Mkuu wa Shule hiyo, Konsolata Tesha, alimweleza Waziri Mkenda kwamba, shule hiyo pia haina jengo la utawala, nyumba za watumishi mabweni, bwalo na stoo ya kuhifadhia chakula.

Akiwa eneo hilo Waziri Mkenda, alielezwa na Ofisa Elimu Sekondari wa Wilaya hiyo, Petronila Wakurila, kwamba Halmashauri ya Wilaya ya Rombo, inalifahamu tatizo la shule hiyo na serikali itaunga mkono utatuzi wake.

Tesha aliwashauri wanafunzi kuendelea kusoma kwa bidii ili waweze kufikia ndoto zao pamoja na kutengeneza taifa lililo bora na lenye wasomi wengi zaidi.

Mwakilishi wa wazazi shuleni hapo, Jackob Asenga, aliwataka wazazi wenzake pamoja na walezi kuendelea kutoa michango ya chakula ili kuwezesha wanafunzi kusoma wakiwa na afya bora.

# Bodi ya Maji yaagizwa kubadilisha bomba kumaliza kero ukosefu maji

**Na Mwandishi Wetu,** SIHA

MWENYEKITI wa Halmashauri ya Wilaya ya Siha mkoani Kilimanjaro, Dancan Urassa, ameiagiza Bodi ya Maji ya Magadini/Makiwaru Water Supply, kuiandikia barua Wizara ya Maji, kuomba kuongezwa kwa ukubwa wa bomba la kupitisha maji kwenda kwa wananchi ili kumaliza kero ya ukosefu wa maji.

Urassa alieleza juzi, namna asivyofurahishwa na mwenendo huo wakati wa kikao cha dharura cha bodi hiyo, kilichokutana kwa ajili ya kujadili upungufu wa maji iliojitokeza na kuutafutia ufumbuzi.

"Naliona tatizo na kuna haja ya kuongeza ukubwa wa bomba ili maji yaweze kuongezeka na kupunguza usumbufu kwa wananchi, hasa vijiji vya tambarare.

"Kitu cha kwanza, lazima serikali ipate taarifa kwamba maji tunayopata ni kidogo, hayatoshelezi. Kwa sababu mradi huu ulianzishwa mwaka 2002, ukilenga kuhudumia kwa watu wasiopungua 80,000. Hivi sasa kuna watu 200,000 na tunapata lita 15 kwa sekunde na bomba linaloleta maji ni la inchi nane. Kwa takwimu hizo, inatosha kuonyesha kwamba maji ni kidogo." Alisema Urassa.

Zaidi alisisitiza: "Katika eneo letu maji hayatoshelezi na watu wanapata maji kwa mgawo. Hata hivyo tusiishie kuitegemea serikali peke yake, tunaweza kuongeza na wafadhili wakiwamo Taasisi ya Punchimin."

Hata hivyo, katika taarifa iliyoandikwa na Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijiji (RUWASA), kumekuwapo na malalamiko ya wateja wanaohudumiwa na Skimu ya Maji ya Gararagua, kukosa maji hasa maeneo ya ukanda wa tambarare.

Vijiji vinavyotishiwa na uhaba wa maji ni Mlangoni, Magadini, Mawasiliano, Kandashi, Mkombozi, Orkolili, Sanya Juu na Ormelili. Zimo pia shule pamoja na nyumba za ibada.

Akielezea hali ilivyo, Mwenyekiti wa Bodi ya Maji ya Magadini/Makiwaru Water Supply, Oscar Kilawe, alikiri kuwapo kwa malalamiko ya wananchi, huku akisisitiza wanahitaji kupata taarifa za ukubwa wa tatizo hilo katika kila kijiji.

"Tenga muda wako wewe ni mjumbe wa eneo hilo, maji hakuna mjulishe fundi wako. Piga simu muite kwa nini maji hakuna. Tukifanya hivyo, tutakuwa tumewasaidia wananchi wetu kujua tatizo, badala ya wananchi kupiga simu ngazi za juu, wakati nyie mpo hapo," alisisitiza Kilawe.

Mjumbe wa Bodi hiyo na Mwenyekiti wa Kamati ya Maji ya Kijiji cha Orkolili, Anton Mwega, alisema hali ni mbaya na wananchi wanalazimika kuhemea maji katika kata za jirani zinazohudumiwa na Mradi wa Maji wa Lawate/Fuka Water Supply.



Wajumbe wa Kamati ya Uchumi ya Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Jiji la Tanga, wakikagua ujenzi wa jengo la zahanati ya Mtaa wa Kisimatui, Kata ya Pongwe, jijini humo juzi. Kulia ni Diwani wa Kata ya Marungu, Mohammed Mambea na (mwenye kitabu) ni Ofisa Mawasiliano wa Halmashauri hiyo, Musa Laban. **PICHA: BONIFACE GIDEON**

# RC aona ombwe la viongozi kuchepusha fedha za lishe

**Na Mary Mosha,** MOSHI

MKUU wa Mkoa wa Kilimanjaro, Nurdin Babu, amesema analiona 'ombwe' la viongozi wenzake, kujitwalia madaraka yasiyo ya kawaida ya kuchepusha fedha zinazotengwa kwa ajili ya masuala ya lishe, huku wakijua kufanya hivyo ni kukiuka maelekezo ya serikali.

Kutokana na hali hiyo, ameagiza Halmashauri sita za Mkoa huo, ambazo ni Manispaa ya Moshi, Halmashauri ya Wilaya ya Moshi, Hai, Siha, Rombo, Mwanga, Same, kuhakikisha fedha zilizotengwa kwa mwaka huu, zinatumika kama zilivyokusudiwa na siyo vinginevyo.

Babu alionyesha kukerwa na uchepushaji wa fedha za lishe na mafungu yake kuelekezwa katika matumizi mengineyo, wakati hafla ya utiaji sahihi mkataba wa usimamizi wa shughuli za lishe.

"Leo (jana) ofisi yangu na wakuu wote wa wilaya tunatia sahihi mikataba ya lishe. Sitaki kusikia tena kuna wilaya imechepusha fedha kwenda kwenye miradi mingine badala ya lishe. Ninyi ni mashahidi kwamba Mkoa wa Kilimanjaro, hivi sasa unashika nafasi ya 21, kati ya mikoa 26 katika suala la lishe.


"Tumeshuhudia katika mwaka wa fedha 2021/2022, zipo baadhi ya halmashauri zimekuwa zikitumia fedha za lishe kwenye mambo mengine ambayo hayana uhusiano na masuala ya lishe. Sasa kwa mwaka wa fedha 2022/2023, sitakubali kuliona hili tena."

Kwa mujibu wa Babu, kwa sasa Mkoa umekuja na mkakati wa kuhakikisha unaondoka kwenye nafasi hiyo na kuingia katika 10 bora. Alitaja mmoja ya mkakati ni kuhakikisha fedha zinazotengwa kwa ajili ya lishe, zinatumika kama zilivyokusudiwa.

Pia aliagiza halmashauri hizo kuhakikisha fedha zilizotengwa kwa ajili ya shughuli za lishe zinatolewa na kutumika kwa wakati.

Alisisitiza kuwa matumizi ya fedha za lishe, yanapaswa kuzingatia bajeti na mpango wa matumizi, huku akiagiza Mkaguzi wa Ndani wa Hesabu za Serikali mkoani humo, kufanya ukaguzi wa matumizi ya fedha za lishe, kila baada ya robo mwaka na taarifa hiyo ifikishwe kwa Katibu Tawala Mkoa huo.

Katibu Tawala Mkoa huo, Willy Machumu, akizungumza baada ya utiaji saini mikataba hiyo, alisema ili kujenga taifa lenye maendeleo, suala la lishe ni jambo la msingi katika jamii.




Ukurasa 17

Tuwe makini na ndimi zisiponze vichwa



# BUFE

IJUMAA OKTOBA 21, 2022
Nipashe

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA

**Mafanikio ya machinga mwenye ulemavu wa kutembea, ageuka gumzo 'mama wa mfano'**

Ukurasa 16

# Wakili 'mtata' wa Kenya atua, baada kutimuliwa akidumu miaka 5 Canada

MIGUNA Miguna, ni wakili Mkenya aliyekimbia nchi yake akielekea Canada mwaka 2018.

Katika uwanja huo, Miguna alilakiwa jana na umati mkubwa wa wafuasi, mwenyewe akielezea furaha ya kurejea nyumbani baada ya takriban miaka mitano ughaibuni.

Alitimuliwa nyumbani, baada ya kudaiwa kusimamia kiapo cha kiongozi wa upinzani Raila Odinga, muda mfupi baada ya upinzani kususia marudio ya uchaguzi wa mwaka 2017.



Wakili Miguna Miguna, baada ya kuwasili na ndege jijini Nairobi, jana. **PICHA: MTANDAO**

**SAFARI ALIKOPITIA**

- Mwaka 2007; alikuwa kiungo wa timu ya kampeni ya chama cha upinzani Kenya, ODM wakati wa uchaguzi mkuu wa 2007 na aliteuliwa kuwa Mshauri Mkuu wa wakati huo Waziri Mkuu Raila Odinga, kabla ya kudaiwa kuwa na utovu wa nidhamu na alisimamishwa kazi bila malipo. Adhabu hiyo iliondolewa baadaye, lakini Miguna alikataa kurejea kuendelea na kazi yake.
- Mwaka 2010, baadhi ya wanachama kutoka chama tawala PNU walimshtumu kwa kuwa raia wa kigeni akimiliki hati ya kusafiria ya Canada, kwa sababu wakati huo sheria za Kenya hazikutambua uraia wa nchi mbili. Hata hivyo, Miguna alihalalisha kitendo chake kwa kusema kwamba "Wakati mtu anapotoroka utawala wa kidikteta, mtu hutumia njia yoyote.
- Mnamo 2012; alizindua kumbukumbu yake ya kwanza iliyoitwa 'Peeling Back the Mask: Quest for Justice in Kenya'. Kitabu hicho kilimkosoa sana Raila Odinga na kuzua maandamano kutoka kwa wafuasi wa Odinga huko Ahero kaunti ya Nyanza. Vilevile alishambuliwa alipokuwa akizindua kitabu hicho katika hoteli moja mjini Mombasa na kulazimika kuokolewa na polisi.
- Mnamo 2016; Miguna akatangaza angewania nafasi ya Ugavana Nairobi kama mgombea huru na akazindua manifesto akiiahidi uongozi unaozingatia uadilifu, sera za mabadiliko zilizo wazi na za kimaendeleo, programu na dhamira ya utoaji huduma, uundaji wa ajira na maendeleo ya miundombinu. Hata hivyo alishika nafasi ya nne.
- Mwaka 2017: Katika uchaguzi wa urais mwaka huu, kiongozi wa upinzani nchini Kenya Raila Odinga na wafuasi wake walidai ushindi wa Uhuru Kenyatta ulikumbwa na udanganyifu na baada ya upinzani kupinga matokeo ya uchaguzi huo mahakamani. Mahakama ilibatilisha matokeo. Miguna, alikuwa katika safu ya watetezi wa Odinga.
- Mwaka 2018, katika hafla ya kuapishwa kwa dhihaka, Miguna alimwapisha Raila Odinga, aliyejitangaza 'Rais wa Watu', serikali ilijibu kwa kuzima matangazo yote ya televisheni na redio na kuwakamata Miguna na wakili mwingine (T J Kajwang') walioshuhudia hafla hiyo. Miguna alifikishwa mahakamani na ikaamriwa na Mahakama Kuu iliamuru Miguna aachiliwe kwa dhamana. Pasipoti ya Miguna ya Kenya ilichukuliwa na akatimuliwa nchini humo.
- Machi 2018, Miguna alijaribu kurejea Kenya, lakini, alipowasili katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Jomo Kenyatta jijini Nairobi kwa ndege kutoka Dubai na alipotaka apewe nafasi ya kuingia kwa mujibu wa amri nyingi za mahakama, serikali ilikataa kumruhusu kuingia nchini. Akarudishwa kwa lazima Dubai alikotoka.
- Machi 2018; Taasisi ya Human Rights Watch ilitoa taarifa ikitaka Miguna aachiliwe. Shirika hilo lilisema kwamba "Mamlaka za Kenya zinapaswa kutii kwa haraka amri."
- Desemba 2018; Mahakama Kuu Kenya ilitoa hukumu dhidi ya serikali kwa kukiuka kwa kiasi kikubwa haki za kikatiba na msingi za Miguna kama vile uraia wa kuzaliwa.
- Desemba 2019; Miguna alitangaza hadharani nia ya kurejea Kenya kupitia akaunti yake ya Twitter ikiwa ni jaribio lake la tatu, akirejea agizo la mahakama lililotolewa mnamo Desemba 2018 kumruhusu kurejea.
- Septemba 22, 2022: Miguna akaahidi angeondoka Canada Oktoba 25 na kutua katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Jomo Kenyatta (JKIA) usiku wa Jumanne, Oktoba 25, 2022. Baada ya kutangaza mabadiliko, akisema angewasili Kenya Oktoba 20, 2022 (jana), saa 12 asubuhi.

Kabla ya ndege yake kutua uwanja wa JKIA, Miguna alikuwa amewaarifu wafuasi wake kwamba amealikwa kwenye sherehe za mashujaa na baadaye ataungana na Rais William Ruto na Mkewe Rachel Ruto kwa karamu ya bustani Ikulu.

- *Kwa mujibu wea BBC.*

UCHUMI

# Pata historia ya mkonge nchini na simulizi Baba Taifa alivyoinyanyua

## • Unajua ilivyowahi kubeba nusu ya bajeti?

**Na Ester Bhoke**

INAPOZUNGUMZIWA historia ya mkonge nchini ni kati ya mazao ya kimkakati kitaifa, nyuma yake kukiwepo umaarufu na historia ndefu, mojawapo haiwezi kutenganishwa na Rais wa kwanza Mwalimu Julius Nyerere, ambaye Ijumaa iliyopita iliadhimishwa miaka 23 tangu kifo chake.

Ikirejewa historia kabla na baada ya uhuru, kuna maeneo kama vile wilaya ya Kilosa na maeneo mengine ya mkoa Morogoro, pia Pwani na Tanga, kulitikisa zaidi katika kilimo chake.

Katani au mkonge, ni zao lililokuwa juu sana sokoni, moja ya bidhaa zake ni magunia na kamba za katani ambazo zilikamata sana soko la dunia.

Pia mashamba yake yanakumbukwa kukamata soko kubwa la ajira, watu kufunga safari kwenda kuajiriwa huko, kutoka ndani na nje ya nchi, hali hiyo inajidhihirisha sana mkoani Tanga, penye mashamba hayo.

Mkonge likiwa zao la biashara kwa sasa linasimamiwa na Bodi ya Mkonge Tanzania (TSB), ikawa na majukumu ya kukuza na kuendeleza zao hilo tangu mwaka 1997 bodi hiyo ilipoanzishwa.

**ULIVYOINGIA NCHINI**

Kihistoria katani imeingia nchini kutoka Mexico, katika kisiwa cha Yucatan, ambako ni Marekani ya Kusini, ambako ndiko kwenye chanzo cha neno katani.

Aliyeleta nchini anatajwa kwa jina, Richard Hindorf, Mjerumani mtafiti wa masuala ya kilimo, akitafiti katika maeneo ya Amani – Derema, mkoani Tanga miaka ya 1890.

Mtafiti huyo (Hindorf) alienda huko kwa mambo yake ya kitafiti na akaliona zao la mkonge na mazingira yanayolimwa kule Mexico, akayaona ni rafiki kwa Tanganyika, hivyo akaja na miche 62 kati ya 1,000 aliyotoka nayo nchini Mexico.

Aliporudi nchini, mtaalamu huyo wa kilimo, akaipanda miche katika kijiji cha Kikokwe wilayani Pangani, Tanga kwenye shamba la kwanza Afrika, lililoitwa Bushiri, ambalo kwa sasa linaitwa Mwera (Mwera Sisal Estate).

Kuanzia miaka hiyo ya 1890, mashamba hayo yaliendeshwa na Wajerumani hadi mwaka 1967 baada ya Azimio la Arusha, ndipo Mwalimu Nyerere akahamishia



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa akifafanuliwa jambo na aliyekuwa Waziri wa Wizara ya Kilimo, Omar Mgumba, katika kituo cha utafiti wa zao la mkonge TARI Mlingano, akiwa katika ziara yake mkoani Tanga, Juni, 2020.

uendeshaji mashamba hayo mikononi mwa serikali.

Ni katika miaka hiyo, ambayo zao la mkonge likawa linaongoza uzalishaji na masoko, kwa sasa kuna jumla ya tani 43,594 zimezalishwa katika mwaka wa fedha 2021/23 na lengo ni kufika tani 120,000 ifikapo mwaka 2025.

**WASIMAMZI MKONGE**

Olivo Mtung'e, ni Mkurugenzi wa Maendeleo ya Zao la Mkonge wa Bodi ya Mkonge, akiwa na majukumu ya kusimamia maendeleo yake, anasema Mwalimu Nyerere alianzisha uwezeshaji wananchi kuendesha zao la mkonge.

Huo ni mpito unaobeba historia kuanzia na waanzishaji wake Wajerumani, baadaye wakafuata Waingereza mwaka 1945, ikiwa ni baada ya ile vita vya pili vya dunia.

Anasema, mashamba makubwa nchini yalikuwa yametapakaa sehemu kubwa ya mkoa Tanga, Dar es Salaam (wakati huo ukiwa mkoa mmoja na Pwani ), Kilimanjaro, Morogoro na Ukanda wa Juu.

"Kwa hiyo, sasa yeye (Mwalimu) alisema, mashamba makubwa yataifishwe, ili kwamba yamilikiwe na serikali na yaongozwe na watu weusi hasa wazawa wa Tanzania, kwa hiyo huo ni uwekezaji wa kwanza.

"Katika kipindi hicho hicho cha Mwalimu, ndipo mkonge ulipewa kipaumbele kwa kiwango kikubwa, ndiyo maana ukiangalia noti au nembo ya Benki Kuu ya Tanzania (BoT) utaona kuna picha ya zao la mkonge. Kwa hiyo Mwalimu alilithamini sana zao la mkonge," anasema Mtung'e.

Anaeleza katika uongozi, Mwalimu Nyerere akaeleza kwamba, katika bajeti ya serikali takriban asilimia 50 ilitokana na chanzo cha zao la mkonge na ndiyo maana, bajeti kadhaa za serikali za bunge lilijadili likiwa Tanga ambako ni kitovu cha uzalishaji wake.

"Katika miaka hiyo ya utawala wa Mwalimu (Nyerere), ndiyo hapo sasa tumeendelea na wazawa kujiona kwamba tunaweza kujiendesha wenyewe. Mpaka sasa hivi tunategemea hadi kufikia 2025 siyo wazawa tena, bali wakulima wadogo wa kawaida kabisa wachangie asilimia 50 ya uzalishaji wote wa mkonge nchini," anasema.

Mtung'e anafafanua kwamba, lengo la sasa ni kuifanyia kazi uzalishaji unaofanywa na wakulima wadogo, baada ya mwaka 2025 ufike ikiwezekana wastani wa asilimia 90.

"Kwa hiyo, tunajivunia sana uanzishwaji na ubunifu wa Mwalimu katika zao la mkonge, kwa kuwaingiza, Watanzania wazawa waweze kulima zao la mkonge," anasema Mtung'e.

**OFISI HADI UINGEREZA**

Ni katika kipindi cha utawala wake, inaelezwa pia mwalimu akaona haja ya kufunguliwa njia ya masoko kimataifa na mkonge



Mkonge ukiwa katika hatua ya uzalishaji kuandaa kamba.
**PICHA ZOTE: MTANDAO**

uuzike kirahisi duniani, akafungua tawi la ofisi ya masoko nchini Uingereza.

Mtung'e anasimulia mafanikio hayo, kwamba Rais Nyerere alikuwa mtu anayeona mbali na haja ya kuendeleza Idara ya Masoko, isikae Tanzania pekee, bali na tawi nchini Uingereza.

Anaueleza mtazamo huo, mzizi wake ni kwamba malipo ya mkonge yafanywe na Watanzania, pia waende wakakae huko ambako mkonge unatumika.

"Mwalimu akafungua ofisi ya masoko Uingereza, ambapo mtu aliyekuwa anafanya kazi ya masoko ya mkonge wote wa Tanzania kwa wazawa wenyewe, kwa maana ya Mamlaka ya Mkonge na baadaye Bodi ya Mkonge ambayo kwa sasa haimiliki tena hizo nyumba za masoko kule Uingereza.

"Kipindi chote cha Mwalimu, alianzisha ile idara ya masoko kule Uingereza kwa ajili ya kuuza Mkonge Ulaya na maeneo mengine. Hayo yote, Mwalimu alifanya ili tuwe na soko la uhakika la mkonge," anasema, akifafanua imelenga haja ya kuwa na masoko ya uhakika duniani.

Mtung'e anasema, kwa sasa wanaendeleza alipoishia Mwalimu Nyerere, Watanzania wenyewe waweze kuuza nje ya nchi, kupitia kampuni zinazomilikiwa na wazawa, hali kadhalika za nje.

Anafafanua kwa sasa kampuni za nje za kuzalisha mkonge, moja ya Kichina an nyingine Uingereza, hali kadhalika viwanda vinavyozalishaji bidhaa za mkonge viko sita, kati yake vitano vinamilikiwa na wenyeji na moja cha kigeni.

"Kwa hiyo, hapo unaweza ukaona viwanda vyote katika sita vinavyomilikiwa na wazawa ni vitano kwa hiyo ni hatua ambayo imepigwa kuanzia mwaka 1967 hadi leo," anaeleza.

Pia Mtung'e kwa upande wa mashamba, amataja kati ya 38 yaliyoko, ni matano tu ndiyo yanamilikiwa na wageni, 33 yaliyobaki yanamilikiwa na kampuni za wazawa, zikiwa na hisa za aserikali.

"Kwa hiyo, unaweza kuona hapo akili na busara aliyotumia Mwalimu Nyerere, aliyatoa mashamba kwa wakoloni akayarudisha serikalini na serikali ikayatoa kwa wananchi.

"Kwa hiyo tunapomkumbuka Mwalimu Nyerere tunamkumbuka kwa haya aliyoanzisha na sisi tunaendeleza pale alipoishia," anahitimisha Mtung'e.

BIASHARA

# Wenye ulemavu wafunguka ya kwao, wanakokwama, kufanikisha biashara

**Na Shaban Njia, KAHAMA**



Waalikwa vijana wenye ulemavu wa ngozi mjini Kahama, wakiwa kwenye shughuli inayowahusu.

JAMII imekuwa ikilitizama kundi la watu wenye ulemavu kuwa ni tegemezi kwenye jamii na familia wanazotoka, jambo ambao sio kweli, kwani nao wana uwezo wa kufanya kazi kama yalivyo makundi wengine na kuwaingizia kipato, kukua kiuchumi na kuendesha maisha yao.

Kundi hilo, pia katika kujishughulisha na shughuli mbalimbali za kujiingizia kipato, bado wanakutana na changamoto nyingi kutokana na aina ya ulemavu wao, ikiwamo kushindwa kuwasiliana wenyewe au na watu wasiokuwa na ulemavu, ili kujikwamua katika masuala ya kuinua vipato vyao.

Baadhi yao wamekuwa na uwezo wa kufanya kazi, lakini inategemea ni wakati gani. Kwa wenye ulemavu wa ngozi, huwa na uwezo wa kufanya kazi za kuwaingizia kipato wawapo juani na kulazimika kuzifanya kwa muda mfupi, hususani ama asubuhi au jioni ili kuepuka kupata saratani ya ngozi wanapopigwa na jua kali.

Kwa kuona kundi hilo halibaki nyuma katika uzalishaji mali, serikali kupitia halmashauri zake nchini imekuwa ikitenga fedha asilimia mbili ya mapato yake ya ndani kwa ajili ya kundi hilo, ili kukuza mitaji yao katika shughuli wanazofanya, hali inayowafanya wasiendelee kudharaulika na kuonekana ombaomba.

Wengi waliofanikiwa kuzipata fedha hizo wamejikita kwenye biashara ndogo na wanaendesha maisha yao vema, wanasomesha watoto, kulipa kodi wanasaidiana wenyewe, lengo ni kuondokana na dhana ya kudharaulika kuwa ni tegemezi kwenye jamii.

**WAPATA MRADI**

Mwenyekiti wa Chama cha Watu Wenye Ualbino (TAS) wilayani Kahama Mkoa wa Shinyanga, Nisha Phabiani, anasema, walipata mradi jumuishi kwa watu wenye ualbino wa Sh. milioni 90 na Shirika lisilo la kiserikali la Karagwe Community Based Rehabilitation Program (KCBRP) na kutoa elimu kwenye jamii.

Anasema, mradi huo walitekeleza katika Halmashauri ya Msalala kwa kipindi cha miaka mitatu kuanzia mwaka wa fedha 2017/2018 hadi mwaka wa fedha uliopita, 2020/2021 na kila mwaka walikuwa wakipewa Sh. milioni 30 na jamii ilipata elimu.

Lingine, mradi huo umewawezesha wenye ulemavu wa ngozi kupata elimu ya ujasiriamali, elimu kwenye jamii kuhusu ulemavu wa ngozi na kutoka Mfuko wa Bima ya Afya wa CHF, ulioboreshwa kwenye kaya 30 zenye walemavu wa ngozi wasiojiweza kwa muda wa mwaka mmoja, hali iliyowawezesha matibabu ya bure katika vituo vya afya.

Nisha anasema, kila mwaka wakati wa utekelezaji wa mradi huo, walikuwa wakipewa Sh. milioni 30 na shirika hilo na waliutekeleza kwa kuelimisha jamii ilipata namna ya kushirikiana na wenye ulemavu wa ngozi katika shughuli mbalimbali za kiuchumi na matokeo ni kwamba, wamenufaika wote kupitia mradi huo.

"Tuliifikia jamii nzima ya Msalala hususani wale wanaoishi pembezoni na kuendekeza mila potofu juu yao, kwamba wanaposhikana mikono au kusalimia na mtu mwenye ilemavu wa ngozi ni mkosi na hawezi kupata mali, jambo ambalo sio kweli na tulikemea ipasavyo," anaeleza Nisha.

**KIKWAZO JUA**

Kwa mujibu wa Nisha, moja ya sababu inayowafanya kushindwa kujishughulisha ipasavyo katika uzalishaji mali, ni uhalisia wa kushindwa kukaa juani kwa muda mrefu, kutokana na ngozi zao kuharibiwa na mionzi ya jua hali inayofanya kufanya kazi kwa muda mfupi sana.

Anasema, wakati wa msimu wa kilimo huwa wanalazimika kulima kuanzia majira ya saa 12 hadi saa tatu asubuhi, kabla ya jua kuanza kuwa kali, kwani ngozi zao hazina uwezo wa kuhimili jua katika harakati za uzalisha mazao ya chakula na biashara kwa uwingu unaofanana na wengine.

Nisha anaeleza licha ya hali hiyo, bado hawabagui kazi yoyote kulingana na udhaifu wao na badala yake wamekuwa wakifanya kila kazi za kuwaingizia kipato. Changamoto inatajwa ni miili yao inayowafanya kufanya kazi kwa muda mfupi, hata kukwaza malengo yao ya kiuchumi kwa wakati.

"Kuna wenzetu wengi wamefanikiwa kama vile Haji Sunday Manara (kiongozi wa soka) na Abdallah Possi, ambaye kwa sasa ni Balozi nchini Ujerumani, wamekuwa msaada mkubwa kwetu kwa kutusaidia vitu mbalimbali, lakini kutokana na kundi kuwa kubwa, baadhi yetu walio karibu wananufaika kupitia viongozi hao," anasema.

**KILIMO WENYE ULEMAVU**

Katibu Msaidizi wa Shirikisho la Watu Wenye Ulemavu Kahama (SHIVYAWATA), Edward Charles, anaeleza kwamba Manispaa ya Kahama, iwapatie pembejeo za kilimo bure, ili kuzalisha zaidi mazao ya chakula na biashara kama wanavyowapatia wakulima vijana wenye uwezo wa kulima ekari tano na kuendelea.

Anasema, manispaa imekuwa na utaratibu wa kutenga fedha kila mwaka wa fedha kutoka katika vyanzo vyake vya mapato, kununua pembejeo na kuzigawa bure kwa vijana jinsi zote wenye uwezo wa kulima mazao ya chakula na biashara nao wana haki ya kupata mkopo huo.

Naye Tatu Nalimi, mkulima na mkazi wa Nyandeka anasema, wana maeneo makubwa ya kulima mazao ya biashara, lakini wanakosa fedha za ununuzi wa pembejeo za kilimo na kwamba wakipata wataongeza uzalishaji kwa wingi.

Kwa upande wake, William Joseph, anasema wengi wao wamepitiliza umri wa ujana, hivyo hawawezi kufanya ujasiriamali wowote, isipokuwa wanaweza kulima na kumuomba Ofisa Kilimo, baada ya kuwakopesha wawapatie elimu ya kulima kisasa, hata kuangukia mavuno ya kutosha.

**DED & OFISA JAMII**

Anderson Msumba, Mkurugenzi wa Manispaa ya Kahama, anasema wamekuwa wakitenga fedha kila mwaka fedha na kununua pembejeo za kilimo na kuzigawa bure kwa wakulima na vijana bila ya kujali hali zao za kimaumbile na mazao wanayoyapata wao.

Anasema, mwaka uliopo wa fedha 2022/2023 wametenga Sh. milioni 84 ukilinganisha na vipindi vilivyopita, hivyo wanatakuwa kujitokeza na kujiorodhesha katika ofisi za kata wanazotoka na kukaguliwa mashamba yao kwa ajili ya kupata pembejeo hizo bure.

Naye Ofisa Maendeleo ya Jamii, Robert Kwela, anasema, manispaa imetenga Sh. milioni 147.8 kwa ajili ya kutoa mikopo isiyokuwa na riba, kwa watu wenye ulemavu ili kukuza mitaji yao, kujikwamua kiuchumi na kuondokana na utegemezi ndani ya familia na jamii wanazotoka.

Aidha, anasema katika mwaka wa fedha uliopita, walitoa mikopo isiyokuwa na riba kwenye vikundi 20 vya watu wenye ulemavu wa Sh. milioni 64.2, hali ambayo mpaka sasa vikundi vinaendelea na urejeshaji mkopo huo na kuvipatia vingine fursa ya kukopa.



Mazingira ya kibiashara, Manispaa ya Kahama ambako wenye ulemavu wana nafasi. **PICHA ZOTE: MAKTABA.**

BIASHARA

# Mafanikio ya machinga mwenye ulemavu wa kutembea, ageuka gumzo 'mama wa mfano'

## • Kuzunguka kwa baiskeli, alivyopata mtaji...

**Na Mary Mosha, MOSHI**

HUJAFA hujaumbika, ndivyo unavyoweza kusema ukitaka kumuelezea Editha Malya (28), mwanamama kijana ambaye ni mfanyabiashara mdogo, maarufu 'machinga' alivyogeuka gumzo katika stendi kuu ya mabasi mjini Moshi, kutokana na kuuza bidhaa mbalimbali kwa kutumia kiti mwendo.

Editha, ambaye ni mlemavu wa miguu hutumia kiti mwendo kutembeza bidhaa zake katika maeneo mbalimbali ya stendi kuu Mjini Moshi, ili kujipatia kipato.

Safari yake ya kujitafutia riziki huanza kila siku saa 12 asubuhi kwa kukodi bodaboda inayompeleka katika kituo cha daladala kwa ajili ya kuanza safari ya kuisaka shilingi.

Hapo ni hatua inayomgharimu shilingi 1000, kufika kituoni hapo na baadaye hutumia shilingi 1500, kupanda daladala ili kumfikisha kwenye Stendi Kuu ya Mabasi Mjini hapo.

Editha anasema, kila anapofika eneo lake la kazi, humlazimu kufuata kiti mwendo katika ofisi za kuhifadhia mizigo (booking) zilizopo mjini hapo, kwa ajili ya kuanza safari yake ya mzunguko, ambapo hatua hiyo inatokana na matatizo anayopitia kwenye daladala

" Kwenye daladala hawataki niingie na kiti mwendo, wanadai kuwa nachukua nafasi kubwa kwa hivyo inanibidi nilipie shilingi 500 kwa ajili ya kuhifadhiwa kiti changu kwenye ofisi ya kuhifadhi mizigo. Nikifika mjini, ndipo naenda kukichukua, "

Anasema muda ndio kitu cha msingi na anachozingatia katika kazi yake, akifafanua kwamba hufika kwake eneo la kazi mapema, ili aanze mizunguko akiwa mwenye nguvu, hatimaye ashuhudie ufanisi.

"Asubuhi saa moja nakuwa nimeshafika stendi, naanza kutembeza mzigo wangu ikifika saa nane nakua nimemaliza naanza safari ya kurudi, nawahi kazini, kwani jua likiwa kali nashindwa kutembeza bidhaa zangu,

"Kwa siku naingiza shilingi 30,000, biashara ikiwa mbovu naweza kupata shilingi 20,000, fedha hiyo inaniwezesha kumsomesha binti yangu, usafiri, kulipia pango na kujikimu kimaisha,"



Mfanyabiashara Editha Malya akiwa katika stendi ya mabasi Moshi mkoani Kilimanjaro akitembeza bidhaa zake. **PICHA: MARY MOSHA**

Anasema, kipato hicho anachopata kinamuwezesha kulipia pango la nyumba anakoishi, kumsomesha mtoto wake, pamoja na kuweza kumudu mahitaji yake binafsi.

Editha anasema, ulemavu huo wa kupooza miguu aliupata mwaka 2009, akitokea mkoani Morogoro baada ya gari walilokuwa wamepanda kugongana uso kwa uso na lingine dogo na baadhi ya abiria walipoteza maisha katika ajali hiyo

"Nilikuwa nafanya kazi kwenye mgahawa mmoja huko Morogoro, ilifika wakati nikaondoka, nikiwa njiani kurejea Moshi tulipata ajali ndipo nilipata ulemavu huu, miguu yangu ilipooza baada ya ajali.

" Kwetu tumezaliwa watoto nane na yeye akiwa ni mtoto wa saba, ambako wazazi walitengana na kusababisha kukosa upendo wa familia," anasema.

Anasema kuwa baada ya mgogoro wa wazazi uliopelekea mama na baba kuachana na kila mmoja kuanza maisha na mwenza mwingine hajawahi kupata upendo kutoka kwa wazazi wake.

Huku akishindwa kujizuia Editha anasema kuwa baba mzazi alimkataa ambapo baba huyo alioa mke mwingine, huku mama yake akiolewa na mume mwingine na hivyo kukosa upendo kutoka kwa wazazi wote wawili ambapo aliishia kulelewa na bibi.

Anaeleza kuwa baada ya kukataliwa bibi ndiye alichukua jukumu la kumlea hadi alipomaliza darasa la saba mwaka 2006, ambapo bibi huyo alifariki mwaka 2007 na ndipo maisha yalipozidi kuwa magumu.

" Baada ya baba kunikataa bibi alinichukua, lakini nilipomaliza darasa la saba bibi akafariki, alipofariki bibi nilifukuzwa kwa bibi, nikaanza maisha ya kutanga tanga, nikaanza kutafuta kazi kwa watu mpaka hii leo nipo najitafutia riziki hapa stendi"

### ALIVYOANZA BIASHARA KWA KUKOPA BIDHAA

Editha anasema kuwa aliianza biashara yake ya kutembeza soksi na bidhaa nyingine katika maeneo ya stendi mjini hapa baada ya maisha kuwa magumu huku akitakiwa kutoa matunzo kwa mtoto mmoja aliyejaliwa.

"Mwaka 2010 niliolewa na bwana mmoja, huko machame lakini alifariki 2011, akiniacha na ujauzito wa miezi miwili nililea ujauzito nikajifungua mtoto ambaye sasa ana miaka 11, kutokana na kuwa na mambo mengi yanayonihitaji nilitafuta biashara ambayo itaniwezesha kujipatia kipato".

> **" Kwenye daladala hawataki niingie na kiti mwendo, wanadai kuwa nachukua nafasi kubwa kwa hivyo inanibidi nilipie shilingi 500 kwa ajili ya kuhifadhiwa kiti changu kwenye ofisi ya kuhifadhi mizigo. Nikifika mjini, ndipo naenda kukichukua, "**

Ilinibidi nije mjini kwenye duka moja la mfanyabiashara wa jumla nikamweleza shida yangu, nilimuomba anikopeshe bidhaa sikuwa na hela ya kulipia, nashukuru Mungu alinisaidia, nikapewa mzigo na nikaanza kuutembeza maeneo ya stendi nilipomaliza nikamrudishia pesa yake, kwenye ile faida niliyopata ndiyo nikaitumia kama msingi wa biashara yangu"

### ASHAURI WENYE ULEMAVU

Editha anawashauri wenye ulemavu kutoibeba hali hiyo kama tatizo na badala yake waichukulie kama hali ya kawaida ili waweze kufikia ndoto zao.

" Kwa wenye hali kama yangu ninawasihi wasiibebe hali hii kama tatizo, waone ni hali ya kawaida wafanye kazi kwa bidii, kwani wakiamua wanaweza, " Anafafanua kuwa juhudi zake zimelenga kuhakikisha anapata ofisi kwa ajili ya kuuzia bidhaa zake ili biashara anayoifanya kwa sasa matatizo mengi kutokana na ulemavu alionao yapungue.

"Natamani niwe na ofisi yangu ya kuuzia bidhaa zangu, kutembea na kiti mwendo unachoka sana, misuli inakaza lakini hakuna namna inanibidi nifanye ili niweze kumtunza mtoto niliye naye na kujikimu mwenyewe, "

### WAKAZI WA MOSHI WANAVYOMZUNGUMZIA

akiwemo Fredrick Lusian ambaye ni mfanya biashara katika eneo la stendi kuu Mjini hapa wanasema kuwa binti Editha amekua kielelezo kizuri kwa wanawake kutokana na juhudi zake katika kuisaka shilingi.

" Huyu binti yupo tofauti na wengine, kila siku tunapita na kuona walemavu wengine wamekua omba omba wengine wakionekana kuwa na nguvu ya kufanya kazi , lakini kwa Editha ameonyesha juhudi ndio maana watu wanamuunga mkono kwa kununua bidhaa zake, "

Veronica Mallya anasema hii ni hatua kubwa kimaisha kwa binti huyu anatafuta kipato ambacho kinamsaidia asiwe tegemezi kwenye jamii na familia yake.

### APONGEZA JUHUDI ZA SERIKALI KUWAJALI WENYE ULEMAVU

Editha anasema kuwa licha ya kutokuwa mnufaika wa mikopo isiyokuwa na riba inayotolewa na Halmashauri hapa nchini bado wapo wanaosaidika kutokana na mikopo hiyo.

" Mimi nilishindwa kujiunga kwenye kikundi kwa sababu sikuwa na kiti mwendo cha kunisaidia kufika sehemu yoyote, nashukuru msamaria mwema alinisaidia cha mama yake ambaye alifariki, baada ya kupata kiti hiki ndipo nikaanza kuzunguka kutembeza bidhaa zangu, "


Anasema kuwa endapo serikali itaboresha masharti ya mikopo hiyo na kufikia hatua ya kupatiwa mtu mmoja mmoja hasa kwa walemavu itakuwa msaada kwani imekuwa changamoto kuwaweka walemavu kwenye kundi la watu watano au zaidi ndipo waweze kupatiwa mkopo.



Stendi kuu mjini Moshi anakofanya biashara. **PICHA: MAKATBA.**

TAFAKURI YA MLALAHOI

# Tuwe makini na ndimi zisiponze vichwa







**NA JOSEPH KULANGWA**
Simu: +255 713 410008
barua pepe: kulangwasos@gmail.com


MIONGONI mwa nahau au semi tulizokuwa tukifundishwa shuleni tangu madarasa ya awali na kuendelea, ni ile isemayo 'ulimi uliponza kichwa'.

Hizi ni baadhi ya lugha za picha zinazofananisha vitu mfupa, ni kuvipa nafsi ya uwezo kufanya au kutenda na hata kusema kufikiri na kuona, lakini hata kusikia.

Ukiambiwa kwa mara ya kwanza, utajiuliza ulimi unawezaje kuponza kichwa, wakati havina mawasiliano ya kuzungumza! Lakini, ukishajifunza kwa kufafanuliwa, utaelewa kinachoendelea.

Utaelewa kwamba ulimi ni kiungo ndani ya kichwa kinachotumika pamoja na kumezea chakula na kinywaji, lakini kina jukumu zito la kuzungumza mtu akaeleweka.

Ukikatwa ulimi, ujue ni mwisho wa kuzungumza au hata kugeuza chakula kinywani. Wenye matatizo ya ulimi, ndio unasikia wanaitwa wenye ulemavu wa kuzungumza au bubu.

Hivyo, dhana ya ulimi kuponza kichwa, ni pale unapotoa kauli tata au zinazoudhi na mwenye ulimi kuadhibiwa, hivyo adhabu huwa ni za kupigwa makwenzi.

Hapo ndipo unaposikia ulimi ulimponza kichwa akapigwa, kwa sababu tu ulitoa kauli tata au ya maudhi. Kwa upande mwingine ni kuamsha hasira, hivyo adhabu kutolewa kwa asiyehusika, yaani kichwa. Ndio kuponzwa kunapojiri.

Vichwa vingi vilishaponzwa na ndimi, licha ya kumiliki na kuhifadhi ndimi hizo. Na mara nyingi, kuponzana kuko zaidi kwenye siasa ambako kauli za maudhi ni kama zimezoeleka.

Kauli hizo huwa ni kama kumimina mafuta ya petroli kwenye moto unaowaka na hivyo kukuza mambo na kuharibu kabisa. Ipo mifano mingi, lakini hii michache inaonesha jinsi ulimi usivyo na staha.

Hivi karibuni katika mikoa ya Dar es Salaam, Mbeya na Arusha, kuna viongozi walitumia ndimi zao, naweza kusema vibaya au kwa bahati mbaya, kutoa kauli zilizotaka kuponza vichwa vyao.

Viongozi hao ni wa chama cha kisiasa, waliotoa kauli tofauti kwa nyakati na maeneo tofauti lakini kwenye muktadha wa uchaguzi wa viongozi ndani ya chama hicho.

Kwa Dar es Salaam, wilayani Temeke, kiongozi wa vijana wa chama hicho, alikaririwa akisema kazi ya umoja huo ni kuharibu halafu chama chenyewe kinawajibika kurekebisha mambo kwa kuomba radhi na yakaisha.

Eti mtu akizingua tunamwagia maji, halafu tutarudi kuomba radhi. Kazi ya Vijana ni kuharibu na kazi ya chama ni kutuombea radhi. Akafafanua kuwa wanaokuja kuomba radhi na kurekebisha mambo baada ya Vijana kuharibu ni jumuiya ya wazee na kinamama katika chama.

Wa Mbeya pale mjini, yeye akasimama na kuwaambia wafuasi wa chama hicho, kwamba mtu akisimama na kukosoa au kuwa sema vibaya viongozi wa chama hicho au serikali, basi vijana 'wanyooke' naye!

Wakati watu wakilalamikia kauli hiyo iliyotoka kwa mtu mzito kweli kweli katika Taifa hili, Arusha akaibuka kiongozi mwingine wa Vijana naye kwa kauli yake akajitambulisha akiomba kura.

Kwamba yeye alikuwa kwenye kundi la 'chinjachinja' na hivyo kuomba achaguliwe ili andelee kupambania chama chake. Kauli hizi zilizusha si tu gumzo, bali mijadala katika vijiwe, vyombo vya habari na mitandao ya kijamii.

Watu waliojadili wakawa wanahusisha kauli hizo na maagizo au maelekezo ya kutaka watu wadhuriane kisiasa, hata kama ni kwa kupokonya maisha. Hiyo ndiyo dhana ya ulimi kuponza kichwa.

Hizi kauli hazina ubishi kwamba zilitolewa na baadhi ya watoaji wakarudi kujitetea na kufafanua kuwa hawakuwa na maana hiyo, huku wengine wakisimamia kauli zao kuwa hivyo ndivyo na ni maoni yao hasa.

Jambo la kutafakari hapa si kutafsiri sisisi tu, bila kuangalia muktadha, lakini pia kubeba uzito wa misimu. Misimu ni maneno ambayo huibuka katika jamii na kukaa kwa muda mfupi na kutoweka kama msimu unavyokuja na kutoweka.

Mathalan, huyu wa Arusha mimi naweza kumtetea, kuwa hakumaanisha alikuwa katika kikosi cha kuchinja watu, kilichomponza ni msimu wa vichinjio wakati wa uchaguzi.

Kwamba wakati huo, kitambulisho cha mpiga kura kiliitwa kichinjio cha kuchinjia wapinzani kwenye sanduku la kura, na katika uchaguzi kunakuwa na vikosi maalumu vya kampeni na uhamasishaji wa nani achaguliwe.

Hivyo, kijana wa Arusha alikuwa katika moja ya vikosi vilivyofanya kampeni ya kuhakikisha wapinzani 'wanachinjwa' kwa kunyimwa kura, lakini si kwa kushika kisu na kuchinja mtu. Namtetea.

Hawa wengine waTemeke na Mbeya Mjini kwa kweli walistahili wakalishwe chini wafafanue walikuwa na maana gani ya kuharibu na chama kuja kurekebisha na kuomba radhi na hiyo ya kunyooka nao. Alamsiki!

FEDHA

## NAIBU WAZIRI AKOSHWA...

# Wanawake katika kasi ya kuwapiku wanaume fani uhasibu leo ‘50/50’

**Na Joseph Mwendapole**

WANAWAKE wameonekana kushika kasi kwenye nafasi za masomo ya uhasibu kwa kuongoza kwenye masomo hayo kiasi cha kuwapita wanaume kwenye fani hiyo.

Kwa mujibu wa takwimu za hivi karibuni za Bodi ya Taifa ya Uhasibu na Ukaguzi (NBAA), wanawake wengi wameonekana kuchangamkia fani hiyo na hivyo kufanya idadi yao kuongezeka maradufu, uwiano ukifika asilimia 50 kwa 50.

Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na Mipango, Lawrence Mafuru, hivi karibuni alihudhuria mahafali ya 44 ya Bodi ya Taifa ya Uhasibu na Ukaguzi (NBAA) na kwenye nasaha zake kwa wahitimu hao, akasema serikali inafurahishwa na idadi kubwa ya wanawake wanaojitokeza kusomea fani ya uhasibu, sasa wakiwa kwenye idadi sawa na wanaume.

Anasema, kwa miaka mingi fani hiyo ilikuwa imetawaliwa na idadi kubwa ya wanaume, lakini inafurahisha kuona kwa sasa wanawake wengi wamechangamkia na kuwa ‘50/50’.

Katika wahitimu 1,155 wa mahafali ya 44 ya NBAA ya hivi karibuni kati ya wahitimu hao wote wanawake ni 577 sawa na asilimia 49.9 na wanaume ni 578 sawa na asilimia 50.04.

“Takwimu ambazo nimetajiwa hapa zinaonyesha kwamba sasa wanawake wengi wameamua kwa dhati kabisa kuchangamkia fani hii ambayo kwa muda mrefu tuliona ikihodhiwa na wanaume pekee,” anasema Mafuru

Mafuru anasema, jitihada zilizochukuliwa kuwahamasisha wanawake kusomea fani hiyo zinapaswa kuwa endelevu ili kuhakikisha idadi inaongezeka hata ikiwezekana kuwapita wanaume.

Dk. Neema Kiure, Mwenyekiti wa Chama cha Wanawake Wahasibu Tanzania (TAWCA), anajinasibu kwamba wao kuongoza kwenye fani ya uhasibu, hawajaanza leo kwani muda mrefu wamekuwa wakiongoza.

Anasema kwa muda mrefu wanawake wameonekana kuchangamkia fani hiyo, hali ambayo imesababisha kuwa ‘nusu kwa nusu’ na wanaume na kuwaasa wengine wajitokeze zaidi kusomea fani hiyo.

“Nitoe wito kwa wasichana waendelee kujitahidi kwenye masomo ya uhasibu na hii haina maana kwamba tunawaacha watoto wa kiume bali tunasema hivyo kwa sababu baadhi ya wasichana wanaona masomo haya ya hesabu ni ya wanaume,” anasema



Sehemu ya wahitimu wa NBAA, katika mahafali ya 44. **PICHA ZOTE: MPIGAPICHA WETU.**

Anasema, kupitia Chama cha Wanawake Wahasibu Tanzania (TAWCA), wamekuwa wakiwahamasisha wasichana kusomea fani ya uhasibu na kuondokana na dhana kwamba fani hiyo ni ngumu .

“Wakati TAWCA inaanza mwaka 2005 wanawake wenye CPA tulikuwa asilimia 20, lakini tumekwenda tukiongezeka na kufika nusu kwa nusu,” anasema Dk. Kiure ambaye ni msomi wa ngazi ya juu ya uhasibu CPA.

Anasema, TAWCA inaendesha programu ndogo za kuwasaidia wanawake wajasiriamali wadogo wadogo, ili wakuze mitaji yao na kuwasaidia masuala ya fedha.

Anasema, wamekuwa wakizungumza na wanafunzi wa shule za sekondari hasa wasichana kuwahamasisha kusomea masomo ya uhasibu na waachane na dhana potofu kwamba masomo ya hesabu ni kwa wanaume.

“Huwa tunawahamasisha wasichana wasilegee wasirudi nyuma na wasifikiri kwamba hawawezi kuwa wahasibu, tunataka mwanafunzi wa kike aone kwamba yeye anaweza kufika wengine walikofika,” anasema

Dk. Neema mbia wa Kampuni ya Ukaguzi wa Hesabu ya Ernest& Young, pia ni mwakilishi wa Tanzania katika Bodi ya Kitunga Viwango vya Kutunza Hesabu katika sekta ya umma, ambayo makao makuu yake yako Toronto Canada.



Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na Mipango, Lawrence Mafuru, hivi karibuni alihudhuria mahafali ya 44 ya Bodi ya Taifa ya Uhasibu na Ukaguzi (NBAA), Dar es Salaam.

Naibu Waziri Mafuru, kwenye mahafali ya 44 ya NBAA, anaipongeza NBAA kwa kuendeleza taaluma ya uhasibu kwa weledi na ubunifu wa hali ya juu, licha ya changamoto mbalimbali wanazokabiliana nazo ikiwemo rasilimali watu.

“Kwa miaka miwili iliyopita tulipata shida ya UVIKO 19 na katika hali ya kawaida ungetarajia mitihani isimame, lakini waliendelea online na kuzalisha CPA nawapongeza sana. Zipo taasisi zilizosimamisha shughuli sababu ya Covid, lakini hapa tunajifunza kwamba katika changamoto tunapaswa kufikiri zaidi,” anasema

Anafafanua kuwa serikali inahitaji wahasibu wengi wenye viwango vinavyotakiwa watakaofanya kazi kwa weledi na kwa kufuata maadili ya taaluma zao.

Anaitaja fani ya uhasibu ni iliyotukuta, hivyo wanapaswa kulinda taswira yake kwa jamii kwa kuacha kufanya mambo ambayo yataifanya idharauriwe kama vile kuandaa ripoti za kihasibu za ‘ujanja ujanja’.

“Kuna wahasibu wanakula njama na wateja wao kwenye kuandaa hesabu tofauti tofauti, anaandaa hesabu ya kupeleka TRA, hesabu ya kupeleka benki kwa ajili ya kupata mikopo, sasa ukigundulika ni wewe umefanya unapoteza sifa yako na unaweza kupokonywa cheti na NBAA,” anatahadharisha.

“Ukitaka kujua kwamba hii ni fani muhimu na yenye heshima ya kipekee angalia idadi ya Watanzania na idadi ya wahasibu waliopo tangu kuanzishwa kwa NBAA mwaka 1972.

“Nimeambiwa hapa na Mkurugenzi wa NBAA kwamba mpaka sasa mko 12,000 kati ya watanzania milioni 60 hivyo lazima mheshimu fani yenu,” anasema

Pia, anawataka wasibweteke, bali wajiendeleze kielimu kwani dunia inakwenda kwa kasi sana na mambo yamekuwa yakibadilika badilika kila mara.

Mafuru anaitaka NBAA kuendelea kutoa mafunzo hayo kwa kuzingatia viwango vya kimataifa ili kuwawezesha wahitimu wa bodi hiyo kushindana kimataifa na kupata fursa mbalimbali zinazotangazwa duniani.

Anatoa wito kufanyike jitihada mbalimbali kuhakikisha watu wengi zaidi wanahamasishwa kujiunga na fani hiyo ili kukidhi mahitaji ya wataalamu wa masuala ya fedha wa ngazi mbalimbali.

“Uchumi wetu unafunguka na unakuwa kwa kasi sasa tunapoendelea kuvutia wawekezaji sekta binafsi tukumbuke kwamba watahitajika wataalaumu wa fedha sasa haitakuwa vyema tunavutia wawekezaji halafu watuambie hakuna wataalamu wa fedha,” alisema.

FEDHA

## WIKI YA WAWEKEZAJI DUNIANI

# UTT AMIS yaainisha njia zake miaka 16 ikiwekeza kwa ushindi kwa umma

**Na Frank Monyo**

KILA ifikapo Oktoba 3 hadi 9 kila mwaka, hufanyika Maadhimisho ya Wiki ya Wawekezaji Duniani, lengo ni kuongeza uelewa kuhusu umuhimu wa elimu kwa umma na ulinzi wa maslahi ya wawekezaji, kwa kuangazia jitihada zinazofanywa na mamlaka za usimamizi wa masoko ya mitaji.

Maadhimisho hayo, ni kampeni ya kimataifa inayohimizwa na Taasisi ya Kimataifa inayohusika na Usimamizi na Utoaji wa Viwango vya Kimataifa vya Masoko ya Mitaji Duniani, yaani International Organization of Securities Commissions (IOSCO) kuongeza uelewa kuhusu umuhimu wa elimu na ulinzi wa wawekezaji.

Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA) ndiyo yenye jukumu la kuendeleza, kuratibu na kusimamia masoko ya mitaji nchini kisheria.

Wiki ya Wawekezaji Ulimwenguni inahusisha Mamlaka za Usimamizi wa Masoko ya Mitaji zilizo chini ya IOSCO pamoja na wanachama wengine wa IOSCO katika mabara sita, kukifanyika shughuli mbalimbali, ikiwamo kuzindua njia za mawasiliano na huduma zinazomlenga mteja.

Aidha, kuna hoja za kukuza ushindani wenye tija unaoongeza wigo wa mikakati ya kutolewa elimu ya wawekezaji, kuandaa warsha na makongamano, pamoja na kutumia mamlaka zao kuendesha kampeni za kitaifa.

Maadhimisho ya mwaka huu yalikuwa na mkakati wa kukabiliana na changamoto za maisha kiuchumi, kuzingatia hali ya uchumi na kulinda uwekezaji wa muda mrefu, huku ukimpa msingi thabiti mwekezaji wa kudhibiti dharula za kifedha na kuwa mwekezaji shupavu.

Taasisi ya UTT AMIS katika maadhimisho ya mwaka huu, imejinasibu kuendelea kutoa elimu kwa umma ya uwekezaji kwenye mifuko ya uwekezaji wa pamoja ya kampuni hiyo ikiamini kuwa ni njia thabiti ya kupambana na majanga au dharura kwa mwekezaji.




Ofisa Masoko na Uhusiano Mwandamizi, Grace Ngailo akitoa maelezo ya mifuko ya uwekezaji katika moja ya maonyesho hivi karibuni. **PICHA: FRANK MONYO**

**WANENAVYO WENYEJI**

Ofisa Mwandamizi wa Masoko na Uhusiano wa UTT AMIS, Rahim Mwanga, anaitambulisha UTT AMIS, kuwa taasisi ya kiserikali chini ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa zaidi ya miaka 17, ikitoa fursa Watanzania kuwekeza katika mifuko yake.\

Anaitaja mifuko hiyo ni; Umoja, Mfuko wa Watoto, Hatifungani, Jikimu, Wekeza Maisha na Mfuko wa Ukwasi ili kutunza thamani ya fedha, kukuza mitaji yao na kupata gawio.

Mwanga anawakumbusha wananchi kuwa na tabia na utamaduni wa kufanya uwekezaji wa muda mrefu kwani utamuwezesha kukabiliana na majanga pindi yanapotokea.

"Mwekezaji yeyote anahitaji njia sahihi za kupunguza hatari za uwekezaji na kukabiliana na majanga, ili kuendelea kutunza mtaji na kupata faida za ushindani, anahitaji utaalumu, gawio, uwazi, urahisi wa kuweka na kutoa fedha zake na gharama nafuu za uendeshaji, vyote vinaweza kupatikana kwenye mifuko yetu ya uwekezaji wa pamoja." anasema Mwanga

Ofisa Masoko - Mwanga, anaielezea Nipashe, namna mifuko ya UTT AMIS inavyofanya kazi huku ikiacha faida lukuki kwa mwekezaji, akianza na namna taasisi hiyo imepewa leseni kutoka Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA), kukusanya amana kutoka kwa wawekezaji na kuziwekeza.

"Tukishapata hizo fedha tunaenda kuwekeza katika masoko ya fedha na mitaji kulingana na waraka wa toleo la mfuko. Faida inayopatikana inarejeshwa na kugawanywa kwa wawekezaji na sehemu ya uwekezaji wao katika mfuko, ndio inafahamika kama kipande," anafafanua.

Mwanga anasema, masoko ya mitaji ni fedha inayohusisha dhamana za uwekezaji zaidi ya mwaka mmoja, akifafanua: "Mfano kuna kuwekeza kwenye Hisa ambazo zimeorodheshwa na Soko la Hisa la Dar es Salaam (DSE). Pia, kuna kuwekeza kwenye hati fungani za serikali za muda mrefu na hati fungani za kampuni."

Mwanga anasema, faida ya kuwekeza inajumuisha nafasi ya kupata faida shindani sokoni, akiendelea: "Mifuko ya uwekezaji inawezesha wawekezaji wadogo kupata fursa za kuwekeza kwenye masoko ya fedha na mitaji kwa viwango vidogo vya fedha tena mara kwa mara.

"Pia, wanapata fursa ya kuwekeza kwenye dhamana, ambazo katika hali fulani mwekezaji mmoja mmoja inakuwa ni ngumu au ghali kuweza kupata dhamana hizo."

"Kampuni ya UTT AMIS, imekuwa ikitoa elimu ya fedha mara kwa mara kwa makundi tofauti juu ya faida na jinsi ya kuwekeza katika mifuko yao, kwa malengo ya muda mfupi hadi mrefu." Anafafanua Mwanga

**MFUKO WA UMOJA**

Mwanga anaeleza, Mfuko wa Umoja uko wazi na wenye uwiano sawa wa uwekezaji, ukiwa na ubora kwa wenye uwekezaji kiwango cha kati.

Hapo anafafanua, kunawekezwa kiwango kisichozidi asilimia 50 ya fedha zake kwenye hisa zilizoorodheshwa DSE na asilimia 50 zilizobaki zinawekezwa kwenye masoko mengine ya fedha na mitaji yenye sifa tofauti.

Sera ya uwekezaji kwa upande mmoja, ni mpango uliowekwa na mfuko kutawanya rasilimali zake. Pia, ni mpango mkakati na kinga, endapo eneo moja la uwekezaji linafanya vibaya.

Mwanga anaueleza kuwa ni uwekezaji kwenye hisa ulio kwa kiwango cha chini, ikilinganishwa na eneo lenye mapato ya kudumu (fixed Income).

Anataja thamani ya kipande kwa sasa imeongezeka kwa Sh. 104.0 na kufikia Sh. 740.0 kwa kila kipande, sawa na faida ya asilimia 16.6 kwa mwaka ulioishia Juni 2021.

Kimsingi, anasema, Mfuko wa Umoja ni wa kwanza kuanzishwa na UTT AMIS mwaka 2005 na umeendelea kufanya vizuri kwa miaka 16 mfululizo, ukiwalenga wawekezaji wenye malengo ya muda mrefu, pia wa kati.

**MFUKO WA UKWASI**

Mwanga anasema, madhumuni ya mfuko huo ni kutoa njia mbadala ya uwekezaji, kwa wanaotaka kuweka fedha kwa kipindi cha muda mfupi na mrefu. Hatari yake, inatajwa kuwa na athari kidogo katika uwekezaji na ukwasi wa hali ya juu, ndio dhumuni hasa la mfuko huu.

Anaeleza Sera ya Uwekezaji kuwa ni kiwango cha chini cha uwekezaji katika masoko ya fedha, itakuwa asilimia 50 na fedha inayobaki itawekezwa katika Dhamana za Serikali. Huo ni mfuko usiowekeza kwenye hisa.

"Chaguo la mpango wa Uwekezaji wa Mfuko huu; unatoa fursa ya kukuza mtaji. Pia mwekezaji anaweza kutoa fedha zake wakati wowote bila gharama yoyote," anafafanua.

**RUKSA YA KUWEKEZA**

Nani anaruhusiwa kuwekeza? Mfuko kisheria uko wazi kwa kila Mtanzania aliye ndani au nje ya nchi, ikihusisha mtu binafsi (ikijumuisha watoto), asasi kama mifuko ya pensheni, benki, taasisi za serikali, vyombo vya ulinzi na usalama, asasi zisizo za kiserikali na mashirika mengineyo.

Anaueleza Mfuko wa Ukwasi,

INAENDELEA UK. 20

UCHUMI

# UTT AMIS yaainisha njia zake miaka 16 ikiwekeza kwa ushindi kwa umma

INATOKA UK. 19

umeongezeka ukubwa wa Sh. bilioni 103.1 sawa na asilimia 91.4. Hapo inamanaisha, ni kutoka Sh. bilioni 112.8 Juni, 2020 hadi Sh. bilioni 215.9 Juni 30,2021.

Mwanga anaeleza, katika kipindi hicho thamani ya kipande iliongezeka kwa Sh.37.5 sawa na faida ya asilimia 15.3 kwa mwaka.

"Faida ya Mfuko wa Ukwasi kwa kipindi cha mwaka mmoja ni asilimia 15.3 ikilinganishwa na faida ya asilimia 15.1 ulionakiliwa mwaka uliopita 2020. Faida ya asilimia 15.3 ni tafsiri ya ongezeko kwenye mtaji wa mwekezaji aliyewekeza kwa mwaka mmoja," anasema Migangala

**MFUKO WATOTO**

Mwanga anaufafanua ni mpango unaokusudia kukuza mtaji kwa muda mrefu, kupitia uwekezaji wa mseto, kwa kuwekeza kwenye hisa zilizoorodheshwa kwenye soko la hisa na dhamana, walengwa ni Watanzania wote wa umri chini ya miaka 18, pia watu binafsi, kampuni, taasisi, asasi za kiraia, mlengwa mkuu akiwa mtoto.

Anaeleza, kwa kipindi cha Juni, 2020 hadi kipindi kama hicho mwaka jana, thamani ya kipande iliongezeka hadi kufikia Sh. 455.2 kutoka Sh. 380.9 mwaka jana, akisema ukubwa wa mfuko huo ni Sh. bilioni 4.2, ikilinganishwa na Sh. bilioni 3.5 ya Juni 30,2020.



Wawekezaji wakijaza fomu za kujiunga na mifuko ya uwekezaji. **PICHA: FRANK MONYO**

**MFUKO WA JIKIMU**

Mwanga anasema, lengo la Mfuko wa Jikimu ni kukuza na kutoa gawio kutokana na mapato ya ziada kwa vipindi tofauti, pia kumkuzia mwekezaji mtaji.

Anasema, mfuko unatoa fursa mbili za uwekezaji, mapato ya robo mwaka, pia mwaka mzima, kwa kuambatanisha na ukuaji wa vipande.

Kiwango cha chini cha uwekezaji katika mfuko huo kwa Mpango wa Mapato ya Robo Mwaka, unatajwa ni Sh. milioni 2 na Sh. milioni 1 kwa Mpango wa Gawio kwa Mwaka; pia Sh. 5,000 kwa Mpango wa Ukuaji Mtaji kwa mwaka.

"Kiwango cha chini cha uwekezaji wa nyongeza au unaofuata (additional investment) ni Sh.15, 000 kwa mpango wowote wa gawio na Sh.5, 000 kwa mpango wa ukuaji mtaji kwa mwaka, hakuna ukomo wa kiwango cha kuwekeza," anafafanua.

Anataja faida nyinginezo katika Mfuko wa Jikimu kwa mwaka wa fedha ulioisha Juni 30, 2021, ulilipa gawio lenye thamani ya Sh. bilioni 1.2 sawa na Sh. 12.0 kwa kila kipande.

"Hadi kufikia Juni 30, 2021 rasilimali za mfuko zilifika shilingi bilioni 17.9 ikilinganishwa na shilingi bilioni 17.6 mwaka uliopita," anasema na kuongeza kuwa;

"Faida ya Mfuko wa Jikimu iliendelea kuimarika na kuongezeka kutoka asilimia 15.6 katika mwaka wa fedha uliopita (2019/2020) hadi asilimia 18.8 katika mwaka wa fedha ulioisha Juni 30,2021."

**HATI FUNGANI ILIVYO**

Mwanga anaeleza Mfuko wa Hatifungani kwa mwaka wa fedha ulioishia Juni 30,2021 faida ilikuwa asilimia 15.7 ikilinganishwa na asilimia 16.2 mwaka uliotangulia.

"Mfuko wa Hati Fungani umelipa gawio la shilingi 1.0 kila mwezi sawa na shilingi 12.0 kwa muda wa mwaka mmoja," anasema

**MFUKO WEKEZA**

Mwanga anautaja kuwa Mfuko Wekeza Maisha, una zaidi ya miaka 10 sasa, ukiambatanishwa na faida za bima. Mwekezaji katika mfuko huo, ana lengo la kiasi anachotaka kuwekeza katika muda wa miaka 10, kiwango cha chini ni Sh. milioni moja. Ni hiari yake kuwekeza kwa mkupuo au awamu.

"Mtu akichagua kuwekeza kiasi hicho (Sh. milioni moja) kila mwezi atahitajika kuwekeza kiasi cha Sh. 8,340 tu ili kukamilisha mpango wake wa uwekezaji.

"Zaidi ya asilimia 99 ya fedha za mwekezaji huwekezwa na chini ya asilimia moja hutumika kugharamia bima," anasimulia, akitaja aina ya bima hizo ni za maisha, ulemavu wa kudumu na ajali.

Mwanga anatoa mfano binafsi, baada ya miaka 10 alifungua kiwanda kidogo cha kutotoa mayai ya kuku na kuuza vifaranga na mayai, akiwa na maelezo ya kijivuna: "Niliweza kununua mashine (incubator) kwa sasa kipato changu kimeongezeka sana."

Anaeleza kuwa, mfuko huo kwa sasa umeongezeka kwa Sh. milioni 400 (ziada 28.6%) hadi shilingi bilioni 1.8 kutoka shilingi bilioni 1.4 mwaka 2020.

"Thamani ya kipande kwa muda wa mwaka mmoja ulioishia Juni 30,2021 iliongezeka kwa shilingi 125.8 (25.6%) hadi kufikia shilingi 617.3 kwa kila mwaka." anasema


---

Dondoo: Kulia
1. miti inayozaa Kakau
7. nyanyuka
8. hutumika kulalia
9. kabumbu
14.nchi yenye mlima mrefu Afrika
15.utukutu 16.mia moja
17.jina la kale la Thailand
18.husaidia mnyama kufukuza wadudu 19.Vientiane ni mji mkuu
20.sehemu ya kitu 21.nasaba
22.mwezi wa tano

Chini:
1. miti inayozaa makungu
2. kiungo kitoacho nyongo
3. ona mtu ufikapo mahali fulani
4. neno la kukanusha 5. soka
6. kampala ni mji wake mkuu
9. dawa ya mzizi fulani wa mti inayoponya mshipa 10.zumari
11.nchi ya pili kwa uzalishaji wa mafuta Afrika 12.dhamira
13.mtu tajiri barani Afrika
14.tolewa maneno machafu
18.mja

## CHEMSHABONGO NA -00 15 00-


Na Felix Magezi
felixmagezi@gmail.com




Kamilisha jedwali kwa kujaza maneno yafuatayo:

TAMATI
TIMAMU
MAMBO
ADABU
MIMEA
MUASISI
SHANGA
MKATABA
MBIO
UBINI
INGAWAJE
ISHA
MAUAJI
BANJA

IDI
TAO
ABE
TIA
KINA
OAA
INUA
DINI
DUA
ITU
UTU
BI




Majibu toleo lililopita



| | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | M | A | A | N | A | N | I |
| | | | | A | | I | | G | | B |
| | | | | K | U | N | G | U | R | U |
| | | | | I | Z | A | R | A | | K |
| T | A | M | A | N | I | | U | | | I |
| U | | | N | D | O | A | N | A | | K |
| T | A | N | G | A | | S | E | T | L | A |
| U | R | D | U | | K | I | T | A | | |
| M | I | A | K | A | | L | I | M | A | |
| U | | N | A | B | I | I | | I | S | I |
| A | S | I | | U | | A | S | A | A | |

| | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| U | P | A | R | A | | O | N | E | A |
| P | A | N | A | M | A | | | | H |
| I | K | A | B | U | | | C | H | E |
| N | U | S | A | | M | D | H | | R |
| Z | A | A | | R | A | H | A | | A |
| A | | | | A | L | A | M | A | |
| N | G | O | N | J | E | R | A | | |
| I | A | S | I | | N | A | N | G | A |
| | M | L | A | N | G | U | Z | I | |
| F | U | O | | | O | | I | A | N |





## ‘Wawekezaji njooni mwekeze katika shughuli za uzalishaji’

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

SERIKALI mkoani Mbeya, imewataka wawekezaji kutoka katika maeneo mbalimbali ya ndani na nje ya mkoa huo kwenda kuwekeza kwenye shughuli za uzalishaji ili kuzalisha ajira kwa wananchi na kuongeza kipato kwa wananchi na taifa.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, aliyasema hayo juzi alipofanya ziara kwenye kiwanda cha kuzalisha vinywaji vikali cha Pan Master kilichoko katika eneo la SIDO jijini humo ambacho kinamilikiwa na mzawa.

Homera alisema Serikali imeweka mazingira rafiki kwa wawekezaji ikiwa ni pamoja na kuandaa maeneo ya kujenga viwanda, mashamba kwa ajili ya kilimo na maeneo ya machimbo kwa ajili ya madini hasa dhahabu.

Homera alisema viwanda vinasaidia kuongeza thamani ya mazao ya wananchi pamoja na kuzalisha ajira kwa makundi mbalimbali ya wananchi na hivyo akawataka wananchi wenye uwezo kuendelea kuwekeza.

“Nawashukuru sana Pan Master kwa kuanzisha kiwanda hiki, hapa mmezalisha ajira nyingi sana na familia za watu hawa zina uhakika wa kuishi kwa sababu ya fedha ambazo wanapata kupitia kazi hii,” alisema Homera.

Mwakilishi wa Mkurugenzi wa Kiwanda hicho, Dk. Mussa Leonard, alisema kiwanda hicho mpaka sasa kimeajiri zaidi ya wafanyakazi 350 wanaofanya shughuli mbalimbali ikiwamo za uzalishaji na shughuli zingine.

Alisema kiwanda hicho kinatarajiwa kuongeza ajira kutokana na mahitaji ya vinywaji wanavyozalisha kuzidi kuongezeka kwenye maeneo mbalimbali ya ndani na nje ya nchi.

Hivyo, aliishukuru serikali kwa kuwawekea wawekezaji mazingira rafiki ya kufanyia shughuli zao ikiwamo kuwaandalia maeneo ya kuwekeza ndani ya mkoa huo.

# Wananchi 54,300 Mbeya hawajui kusoma, kuandika

**Na Nebart Msokwa,** KYELA

WANANCHI 54,300 mkoani Mbeya wamebainika kuwa hawajui kusoma na kuandika jambo ambalo linaashiria kuanza kuongezeka kwa kundi la wajinga na kushuka kwa kiwango cha elimu mkoani humo. Hayo yalibainishwa na Mkufunzi Mkazi wa Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima Mkoa wa Mbeya, Thomas Mbuba wakati wa maadhimisho ya Wiki ya Elimu ya Watu Wazima, kusema zinahitajika jitihada za kukabiliana na tatizo hilo.

Alisema idadi hiyo ilibainika kupitia utafiti uliofanywa na taasisi hiyo kati ya mwaka 2020 na 2021 na kwamba tatizo kubwa lipo kwa vijana wenye umri wa kati ya miaka 18 na 35.

Mbuba alisema idadi hiyo ni kubwa na inailazimu taasisi hiyo kubuni mbinu mbadala za kuhakikisha kundi hilo linajifunza stadi hizo pamoja na kupata maarifa mengine kupitia elimu hiyo ya watu wazima.

“Kupitia maadhimisho haya ni lazima tutafakari namna ya kuwawezesha watu hawa kujua kusoma, kuandika na kuhesabu, lakini pia ni lazima tuangalie namna ya kuyashirikisha makundi mbalimbali kukabiliana na hali hii,” alisema Mbuba.

Alisema watashirikisha makundi mengine yakiwamo ya watu wenye ulemavu katika kukabiliana na tatizo la watu wazima kutojua kusoma na kuandika.

Hata hivyo alisema kupitia utaratibu wa kuwarejesha shuleni wasichana ambao walikatishwa masomo kwa sababu mbalimbali ikiwamo kupata ujauzito, katika Mkoa wa Mbeya wameshawarejesha wasichana 468 ambao wanasoma kwenye shule mbalimbali.

Mbuba alisema utaratibu huo utawasaidia wasichana hao kufikia ndoto zao ambazo zilikuwa zimeanza kufifia kutokana na kuwa nje ya mfumo wa elimu.

Mwenyekiti wa Maofisa Elimu wa Mkoa wa Mbeya, Mwalimu Thomas Mwanga, alisema Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima inashindwa kutekeleza vizuri baadhi ya majukumu yake kutokana na ufinyu wa bajeti zinazotengwa na halmashauri.

Alisema taasisi hiyo inahitaji fedha kwa ajili ya kuandaa vifaa vya kufundishia kwa vitendo na hivyo akaiomba serikali kuisaidia taasisi hiyo kutenga bajeti kwa ajili ya vitu hivyo.

Ofisa Elimu wa Mkoa wa Mbeya, Malimu Ernest Hinju, aliagiza halmashauri zote za mkoa huo kutenga bajeti kila mwaka kwa ajili ya kugharimia elimu ya watu wazima ili kuhakikisha tatizo hilo la watu kutojua kusoma, kuandika na kuhesabu linamalizwa.

Aliagiza pia halmashauri zote kuandaa mashindano ya stadi za kusoma, kuandika na kuhesabu kwa wanafunzi wa shule mbalimbali na kutoa zawadi kwa washindi ili kuhamasisha watoto kujifunza kwa nguvu stadi hizo.

Mwalimu Hinju aliagiza pia kuongeza ushirikiano kati ya maofisa elimu wa halmashauri na wadau wengine wa elimu katika kukabiliana na tatizo hilo la watu wazima kutojua stadi hizo.

“Nawaagiza maofisa elimu wa wilaya zote kuhakikisha mnaandaa mashindano ya mara kwa mara ya kusoma, kuandika na kuhesabu, tutawaandikia pia barua wakurugenzi ili kulipa uzito zaidi jambo hili,” alisema Hinju.

Aliipongeza Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima kwa kuendelea kupambana na tatizo la watu kutojua kusoma na kuandika na akasisitiza kwamba iendelee kushughulika na jambo hilo.



Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Dk. Rashid Chuachua (kulia), akipokea moja ya mifuko ya saruji 180 kutoka kwa Mhifadhi Mkuu wa Shamba la Miti la Kiwira, Thadeus Shirima, kwa ajili ya kusaidia ujenzi wa kituo cha polisi Kata ya Igoma, juzi. **PICHA: NEBART MSOKWA**

## Operesheni kuwaondoa waliovamia vyanzo vya maji, misitu kufanyika

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

SERIKALI wilayani Mbeya imewataka wananchi wote wanaofanya shughuli za kibinadamu kwenye vyanzo vya maji na hifadhi za misitu ndani ya wilaya hiyo, kuondoka kwa hiari kabla hatua za kuwaondoa kwa nguvu hazijaanza.

Aidha, imetangaza kuanza operesheni ya kuwaondoa kwa nguvu kuanzia wiki ijayo na kwamba mbali na kuondolewa pia watachukuliwa hatua kali za kisheria.

Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Dk. Rashid Chuachua, alitoa kauli hiyo juzi wakati akipokea mifuko 180 ya saruji ambayo imetolewa na Wakala wa Huduma za Misitu nchini (TFS) kupitia Shamba la Miti la Kiwira kwa lengo la kuwasaidia wananchi wa Kata ya Igoma kukamilisha ujenzi wa Kituo cha Polisi.

Wananchi wa kata hiyo wamejenga Kituo cha Polisi kwa nguvu zao kwa lengo la kusogeza huduma za ulinzi na usalama kwenye eneo lao, wanadai kuwa wamekuwa wakiipata huduma hiyo umbali wa zaidi ya kilomita 50.

Mbali na mifuko hiyo ya saruji, pia wakala huo ulikabidhi madawati 120 kwa ajili ya Shule ya Sekondari Itala iliyoko katika Kata ya Ulenje wilayani humo.

Dk. Chuachua alisema shughuli zinazofanywa na wananchi hao zinaharibu vyanzo vya maji pamoja na kuharibu rasilimali zingine zilizoko kwenye misitu hiyo na hivyo kuwa chanzo cha mabadiliko ya tabianchi.

Alisema serikali haitakubali misitu hiyo iharibiwe na hivyo lazima iendeshe operesheni ya kuwasaka wanaolima, kuchungia mifugo kwenye maeneo hayo pamoja.

“Hii misitu ni muhimu kwa ajili ya kizazi cha sasa na kijacho, kwa hiyo nawahakikishia kwamba wiki ijayo tutaendesha operesheni ya kuwasaka na kuwaondoa kwa nguvu wale wote wanaoharibu maeneo haya, ondokeni ili mtupishe tuendelee kuhifadhi,” alisema Dk. Chuachua.

Aliushukuru uongozi wa TFS kwa kuamua kuwasaidia wananchi hao vifaa hivyo kwa maelezo kuwa wananchi walitakiwa watumie rasilimali zao kuvitafuta.

Mhifadhi Mkuu wa Shamba la Miti la Kiwira, Thadeus Shirima, alisema waliamua kuwasaidia wananchi hao ili kuimarisha ujirani mwema baina yao.

Alisema wananchi hao wamekuwa wakishirikiana na wakala huo kwenye ulinzi wa msitu huo ikiwa ni pamoja na kufanya shughuli za upandaji.

“Lengo letu ni kuwaonyesha wananchi kwamba shughuli ambazo huwa wanatusaidia, matunda yake ndio haya na tutaendelea kusaidiana nao kwenye shughuli mbalimbali,” alisema Shirima.

Madiwani wa Kata za Ulenje na Igoma ambao maeneo yao yamenufaika na msaada huo, waliushukuru wakala huo kwa misaada hiyo na wakaomba waendelee kushirikiana kwenye shughuli mbalimbali za maendeleo.

Diwani wa Kata ya Igoma, Andrew Mwaipopo alisema waliomba msaada wa kusaidiwa kwenye ujenzi wa kituo cha polisi kutokana na nguvu ya wananchi kuwa ndogo.

Alisema uongozi wa wakala huo uliridhia kusaidia saruji kwa sababu na wenyewe unahitaji kituo hicho kwa ajili ya ulinzi wa raslimali zao kwenye eneo hilo.





# Wizara ya Afya yasaini mkataba kuimarisha huduma za kibingwa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WIZARA ya Afya imesaini mkataba wa saba wa mahusiano na nchi rafiki ili kuimarisha ushirikiano katika masuala ya afya kwenye maeneo sita ikiwamo huduma za ubingwa bobezi.

Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Prof. Abel Makubi, aliyasema hayo jana jijini hapo kwenye hafla ya kuingia makubaliano kati ya Tanzania na Taasisi ya Alameda ya nchini Misri.

Alibainisha makubaliano mengine waliyoingia ni pamoja na Hospitali ya MIOT ya nchini India, Hospitali ya Sheba nchini Israel, mikataba ya pande mbili na nchi za Uturuki, Kenya, Burundi na Rwanda.

Alitaja maeneo yanayolengwa kwenye makubaliano hayo ni kuimarisha mahusiano katika mafunzo kwa watumishi wa afya kwenye nyanja ya ubingwa na ubingwa bobezi, wataalamu zaidi ya 20 watanufaika kila mwaka kwa gharama nafuu.

"Pia kubadilishana wataalamu ambapo wataalamu wa hapa nchini watapata fursa ya kwenda kujifunza nje ya nchi pia wa nje ya nchi watakuja kufanya kazi na wataalamu wetu hapa nchini,"alisema.

Alisema pia kutakuwa na ushirikiano wa kikanda katika masuala ya udhibiti wa magonjwa ya dharura mipakani, masuala ya utafiti wa tiba na kinga, kuimarisha huduma za tiba mtandao na mifumo ya TEHAMA.

Alisema eneo lingine la ushirikiano ni uwekezaji wa huduma za tiba na viwanda vya dawa na vifaa tiba.

Alisema hati za makubaliano 15 zipo katika hatua mbalimbali kusainiwa na wizara.

"Wizara ya Afya itaendelea kushirikiana na jumuiya za kimataifa katika kusimamia na kutekeleza vipaumbele vyake na kufikia malengo yaliyowekwa na serikali,"alisema.

Prof. Makubi alisema wizara hiyo inaendelea kujipanga katika kuimarisha ushirikiano na jumuiya za kimataifa kwa faida ya Watanzania.

Akizungumzia makubaliano yao na ALAMEDA, katibu huyo alisema nchi ya Misri ni miongoni mwa nchi zilizofanikiwa sana kwenye sekta ya afya ikiwa ni pamoja na bima ya afya kwa wote.

Alisema ushirikiano huo hadi sasa umezaa matunda kwenye Taasisi ya Jakaya Kikwete na Hospitali ya MOI, wataalamu wa ndani walijengewa uwezo huduma za kibingwa ikiwamo za matibabu ya moyo.

Alieleza kuwa kutokana na Tanzania kuendelea kuimarisha huduma za kibingwa baadhi ya hospitali zinapokea wagonjwa kutoka nchi nyingine na kuwatibu.

Mkurugenzi Mtendaji wa ALAMEDA, Neeraj Mishra, alisema hospitali hiyo inatambulika hadi Marekani kwa ubora wa huduma na kwamba mafanikio ya sekta ya afya Misri yanatokana na utashi wa kisiasa.



Makamu Mwenyekiti wa Soko la Sabasaba, Kombo Kombo (kulia), akizungumza na wachuuzi wa mboga wa eneo la stendi ya daladala ya Sabasaba, jijini Dodoma jana, akiwaomba kuondoa bidhaa zao kwenye eneo hilo, lililopigwa marufuku kwa biashara ya aina yoyote. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# LSF: Watanzania milioni saba wafikiwa na wasaidizi wa sheria

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

MKURUGENZI Mtendaji wa Shirika la Legal Services Facility (LSF), Wakili Deogratias Bwire, amesema katika kipindi cha mwaka jana wananchi zaidi ya milioni saba walifikiwa na wasaidizi wa sheria, kutatua migogoro 88,000.

Aliyasema hayo jana jijini hapo alipokuwa akifungua mkutano uliowashirikisha wadau zaidi ya 400 kutoka kwenye mashirika yanayotoa huduma za msaada wa kisheria na wasaidizi wa kisheria takribani 200 wanaopokea ruzuku kwa ajili ya utekelezaji wa programu ya upatikanaji wa haki nchini.

Alisema kati ya idadi hiyo ya migogoro, 65,000 ilitatuliwa na wasaidizi wa kisheria.

Bwire aliwapongeza wasaidizi wa sheria kwa kazi wanayoifanya kwa kuiwezesha jamii hususani wanawake na watoto wa kike kupata haki zao.

Alisema mkutano huo unalenga kujadili na kutathmini utekelezaji wa upatikanaji wa huduma za msaada wa kisheria na wasaidizi wa kisheria nchini, mafanikio, matatizo, fursa na mipango mikakati kwa ajili ya utekelezaji wa programu ya upatikanaji wa haki nchini katika kipindi cha mwaka mmoja ujao 2022/23.

Wakili Bwire alisema kwenye mkutano huo watatoa mrejesho wa utekelezaji wa shughuli za msaada wa kisheria, kubadilishana uzoefu na kujifunza mbinu mbalimbali kwa ajili ya kujijenga na kujiimarisha kwenye masuala yote yanayohusu huduma za msaada wa kisheria.

"Hii ni muhimu kwetu kama wasimamizi wa ruzuku tunazozitoa kutoka kwa wadau wetu wakubwa ambao ni Shirika la Kimataifa la Maendeleo la nchini Denmark (DANIDA) ili kujenga jamii iliyowezeshwa kisheria," alisema Wakili Bwire.

Akiongea kwa niaba ya Msajili wa Huduma za Msaada wa Kisheria Wizara ya Katiba na Sheria, Wakili wa Serikali, Agnes Mkawe, aliwapongeza LSF kwa kuandaa warsha hiyo muhimu kwa mustakabali na ustawi wa wadau wa sekta ya msaada wa kisheria na huduma.

# Uongozi Soko la Sabasaba waanza kuwaondoa machinga

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

UONGOZI wa Soko la Sabasaba jijini Dodoma umeanza kutekeleza agizo la Jiji la kuwahamisha wafanyabiashara zaidi ya 1,000 ambao walikuwa wanafanya shughuli zao katika stendi ya daladala ndani ya eneo hilo.

Akizungumza na waandishi wa habari jana wakati wa kuwaondoa wafanyabiashara hao, Makamu Mwenyekiti wa soko hilo, Kombo Adam, alisema wamefanya hivyo kutokana na eneo hilo la stendi kutokuwa salama kwao.

Alisema uongozi wa Jiji ulitoa agizo hilo Septemba 6, mwaka huu, kwamba uliagiza wafanyabiashara wanaofanya shughuli zao katika eneo la stendi ndani ya soko hilo kuondolewa mara moja.

Alisema wafanyabiashara hao kuendelea kufanya shughuli zao katika eneo hilo ni hatari kwao kutokana uwapo wa magari mengi hali inayosababisha wakati mwingine bidhaa zao kukanyagwa.

"Hili eneo ni kwa ajili ya daladala lakini wafanyabiashara hawa wamekuwa wakipanga bidhaa zao chini hali ambayo inawalazimisha kuhamisha bidhaa zao kila wakati kukwepa magari,"alisema.

Alisema lengo la kuwahamisha wafanyabiashara hao ni kuwatafutia eneo salama kwao pamoja na wateja ili kuwapunguzia adha wanayoipata sasa.

Kombo alisema tayari wameshapa eneo kwa ajili ya kuwahamishia wafanyabiashara na kipaumbele chao kitakuwa kwa wale ambao wameondolewa katika eneo la stendi.

"Mimi kama kiongozi wenu niwahakikishe kuwa wale ambao mlikuwa stendi ya daladala ndiyo mtakuwa wa kwanza kupata maeneo, hapa ndipo wengine watapata kwa hiyo msiwe na wasiwasi wowote,"alisisitiza Kombo.

Mmoja wa wafanyabiashara waliohamishwa, Karim Godwin, aliwataka viongozi wa soko hilo kuharakisha mchakato wa kuandaliwa kwa eneo la kufanyia biashara ili waendelee na shughuli zao bila kuathiri biashara zao.

"Tunaomba eneo liwekwe vizuri ili watu tuendelee na kufanya biashara zetu lakini pia wale ambao ni waathirika wa kuondolewa pale stendi ndiyo tupewe kipaumbele, viongozi wanatakiwa kulisimamia hili kwa makini zaidi," alisema.

Mfanyabiashara mwingine Lucy Mdanga, alisema kutokana na kuhamishwa ameshindwa kufanya biashara kwa muda wa wiki mbili, hali ambayo imempa ugumu wa maisha kutokana na kutegemea kazi hiyo kwa ajili ya kupata riziki na familia yake.



## Ufugaji nyuki kusaidia mageuzi uzalishaji asali

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WIZARA ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo imesema mradi shirikishi wa ufugaji wa nyuki ni muhimu kusaidia kuleta mageuzi makubwa ya uzalishaji wa asali na kuingia katika soko la kimataifa.

Hayo yalisemwa jana na waziri wa wizara hiyo, Shamata Shaame Khamis, wakati alipowakabidhi vifaa vya kufuga nyuki vikundi 13 ikiwamo mizinga pamoja na mabomba ya moshi na nguo za kujilinda wakati wa kuvuna asali.

Alisema serikali imejipanga kuyafikia makundi yote yanayofanya shughuli zao kwa njia ya kazi za ujasiriamali na kujikwamua kiuchumi.

Alisema katika fedha za ahuweni kupambana na ugonjwa wa UVIKO-19, serikali imetenga Sh. milioni 680 kwa ajili ya kuwafikia wafugaji wa asali, Unguja na Pemba.

Alisema soko la asali hivi sasa lipo kubwa ndani na nje ya nchi kutokana na kuimarika kwa sekta ya utalii nchini na wafugaji wanatakiwa kutumia mbinu za kisasa kupata kipato kikubwa.

"Vifaa hivi tunavyowakabidhi wafugaji asali lengo lake kubwa kuongeza uzalishaji wa asali na kutumia mbinu mpya za kisasa ambazo zitasaidia kuvifikia viwango vya kimataifa," alisema.

Naye Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Seif Shaamban Mwinyi, alisema matumizi ya vifaa vya kisasa vya kufuga nyuki ndiyo vitakavyoleta mageuzi makubwa kwa wafugaji kupata kipato kikubwa.

Alisema jumla ya vijiji 16 vyenye msitu wa kufugia nyuki vitafaidika na vifaa hivyo katika utekelezaji wa mradi wa kufuga nyuki kwa kutumia mbinu za kitaalamu zaidi.

Alisema utafiti uliofanywa na wizara kwa kushirikiana na Kamisheni ya Utalii Zanzibar unaonesha soko la asali lipo kubwa katika sekta ya utalii ambalo halijatumiwa vizuri.

Kwa upande wao walengwa wa vifaa hivyo walisema watahakikisha wanavitunza na kuvitumia ipasavyo ili kuongeza uzalishaji wa asali na kupata tija zaidi.

# Mabadiliko tabianchi hatari namba 1 uchumi wa bahari

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

KATIBU Mkuu Wizara ya Uchumi wa Buluu, Aboud Suleiman Jumbe, amesema mabadiliko ya tabianchi ni hatarishi namba moja katika uchumi endelevu wa bahari.

Alisema ongezeko la joto katika bahari, uchumi wa buluu huathirika kupitia kilimo cha mwani na kuongezeka kwa kina cha bahari utalii pia huathirika.

Aliyasema hayo mjini hapo, wakati akiwasilisha mada katika mafunzo ya waandishi wa habari kuhusu dhana ya uchumi.

Alisema mabadiliko ya tabia ya kikemia ya bahari, husababisha kufa kwa matumbawe, kupotea bayoanuai na upotevu wa mikoko, nyasi za baharini na fukwe.

Alisema uvuvi wa bahari ndogo Zanzibar, umeshaathirika na mabadiliko ya tabianchi na umesababisha kuwapo kwa mavuno madogo ya samaki.

Alisema asilimia 70 ya sayari ya dunia imefunikwa na maji na 50 ya hewa safi inayovuta binadamu inatokana na bahari ambayo mpaka sasa inazalisha kiasi cha faida chenye usawa wa dola trilioni tatu kila mwaka.

"Kama bahari ingekuwa nchi, ingekuwa ni nchi ya saba ulimwenguni kwa nguvu za kiuchumi," alisema Jumbe.

Kadhalika, alisema watu bilioni 2.4 wanaishi ndani ya kilomita 100 ya ukanda wa bahari ambao ni zaidi ya robo ya watu wanaoishi ulimwenguni.

Aidha, watu milioni 600 ulimwenguni wanaishi katika maeneo hatarishi ya bahari ambayo hayazidi usawa wa bahari wa mita 10 na katika maeneo hayo baadhi ya maeneo ya Zanzibar yapo katika hatari kwa sababu ya mabadiliko ya tabianchi.

Alisema ukanda wa magharibi mwa Bahari ya Hindi ina uwezo wa uchumi wa bahari inayofikia Dola za Kimarekani bilioni 330.

Alisema nchi zote 10 za ukanda wa Bahari ya Hindi, uwezo wao wa uchumi haufiki Dola bilioni 2.7 kwa mwaka.

Hata hivyo, alisema bahari ni kama kiumbe kinaishi, kinaumwa na kiathirika, pia bahari ya karne ya 21 tija yake sio sawa na ya karne ya 15 kwa sababu ulimwengu ulikuwa na watu kidogo, lakini imeathirika kwa sababu ya matumizi makubwa.

Alisema lazima kuwa na matumizi sahihi ya bahari na endelevu ambayo matokeo yake yanaweza kuwa na tija zaidi.

Vile vile, mpango wa maendeleo wa Zanzibar shabaha yake ifikapo mwaka 2026 uchumi wa buluu uwe umefikia kuchangia asilimia 60 ya pato la taifa.

Alisema ili kufikia huko kuna kazi ya kuimarisha mifumo ya kisera, kisheria na kimipango, kuanzisha mpango wa matumizi ya bahari na diplomasia ya uchumi wa buluu ili kuinyanyua Zanzibar kiuchumi.

Kadhalika kuna changamoto ndani ya mazingira ikiwamo, uelewa, ufahamu, ubunifu, maarifa, usawa wa kijinsia na nafasi za sekta binafsi katika uchumi wa buluu.

Mwandishi nguli visiwani humo, Salim Said Salim, aliwataka waandishi wa habari kuwa mabalozi wazuri kulinda na kuhifadhi rasilimali za bahari.

Alisema waandishi wa habari wana nguvu kubwa ya kuihabarisha jamii katika kuyalinda na kuyahifadhi mazingira ili kuepukana na athari za mabadiliko ya tabianchi yanayosababishwa na shughuli za kibinadamu ikiwamo uvuvi haramu.



Sehemu ya washiriki wa kikao cha mrejesho wa matokeo ya utafiti wa uvuvi wa mtando wakimsikiliza Waziri wa Uchumi wa Buluu, Masoud Suleiman Makame (hayupo pichani), wakati akifungua kikao hicho, kilichoandaliwa na Taasisi ya Utafiti ya Uvuvi na Maliasili za Bahari, Maruhubi, Mjini Zanzibar jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Usimamizi uvuvi unaozingatia mahitaji kijamii muhimu

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi, Masoud Suleiman Makame, amesema usimamizi wa rasilimali za uvuvi unaozingatia mahitaji ya kijamii na kiuchumi ya wavuvi wadogo ni muhimu kwa uvuvi endelevu.

Alisema, aina za uvuvi hubadilika kila wakati ili kuongeza ufanisi katika uvunaji wa samaki, kujiongezea kipato na pia kulinda ajira kwa jamii za wavuvi.

Aliyasema hayo jana mjini humo, katika taasisi ya utafiti wa uvuvi na maliasili za bahari wakati wa kikao cha kutoa mrejesho wa matokeo ya utafiti wa uvuvi wa mtando (Ring net) ili kukuza uelewa wa uvuvi huo.

Alisema uvuvi wa mtando umejiri kwa watu wengi Tanzania, hususan visiwa vya Zanzibar.

Kwa upande wa kisiwa cha Unguja, uvuvi huo hufanyika katika ukanda wa Kaskazini Magharibi na Kusini (Kizimkazi) na wavuvi hupata mavuno ya haraka na kipato kikubwa hali inayohamasisha idadi kubwa ya wavuvi kuwekeza kwenye uvuvi huo.

Hata hivyo, alisema madhara yatokanayo na uvuvi huo kwenye mazingira ya bahari, yakiwamo maeneo yenye nyasi bahari na matumbawe, ambayo ni mazalia, malisho na makuzi ya samaki, hayafahamiki vizuri.

"Ni jukumu la utafiti kutuonesha ni madhara yapi yanayoweza kutokana na aina hii ya uvuvi kwa mazingira ya bahari na rasilimali zake kwa ujumla," alisema waziri huyo.

Aidha, alisema matokeo ya utafiti huo yatasaidia kuweka misingi itakayoimarisha nia ya kuwa na uvuvi endelevu utaozingatia uhifadhi wa rasilimali za bahari.


Mkurugenzi wa Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi na Maliasili za Baharini, Zakaria Ali Khamis, alisema uvuvi wa mtanda ni maarufu Zanzibar na hufanywa zaidi na wananchi wa jumuiya ya Wakojani na utafiti umebaini kuwa una tija kubwa kwa jamii.

Alisema ukifanywa kinyume na sheria unaathari kubwa kwa maeneo ya mazingira ya bahari na hutakiwa kuvuliwa katika kina kikubwa cha maji ya bahari kisichopungua mita 30.

"Unaweza kufanyika uvuvi huu usilete athari, lakini katika maeneo maalum ya bahari na haipendezi uvuvi huu kufanyika katika maeneo ya uhifadhi wa bahari," alisema.

Akitoa muhtasari wa matokeo ya utafiti huo, Mkuu wa Idara ya Utafiti, Ali Said Ali, alisema lengo la utafiti huo ni kuwahabarisha wadau wa uvuvi na maliasili za baharini, kugundua athari zipi zinazopatikana katika uvuvi huo na kupata mapendekezo ya pamoja kuendelea kuleta tija bila ya kuathiri mazingira ya bahari.

Alisema utafiti umebaini kuwa wavuvi wengi wanafanya shughuli za uvuvi huo katika maji madogo ambayo ni ya hifadhi yenye matumbawe na kuathiri mazalia ya samaki maeneo ambayo hupenda kupata chakula kwa ajili ya makuzi yao.





# Wasomi elimu watu wazima waomba vifaa kujifunzia

**Na Vitus Audax**

BAADHI ya wanafunzi wa elimu ya watu wazima mkoani Mwanza wameiomba serikali kuboresha miundombinu pamoja na vifaa vya kujifunzia vitakavyo wawezesha kusoma kwa vitendo.

Wanafunzi hao ni wale wanaojifunza ujuzi mbalimbali ikiwamo ufundi wa umeme, nguo, thamani, ubunifu pamoja na masomo ya muda mfupi yanayomwezesha kujiunga na elimu rasmi.

Walitoa ombi hilo wakati wa maadhimisho ya elimu ya watu wazima na kueleza kuwa tatizo la vifaa ni kikwazo kwao katika kusoma.

Mmoja wa wanafunzi hao, Peter Boniface kutoka Chuo cha Ufundi Sengerema alisema licha ya kupokea mafunzo ya fani mbalimbali chuoni hapo bado wanaupungufu wa vifaa vya kujifunzia ikiwamo magari, cherehani, umeme wa kuaminika, vyumba vya kujifunza kwa vitendo havijakarabatiwa kukidhi mahitaji yao.

Mwanafunzi mwingine Japheth Magoti, ambaye anasomea ufundi wa ujenzi na ukarabati wa mitumbwi kutoka Kijiweni Sengerema aliiomba serikali kuweka utaratibu wa kuwatafutia vyuo vya teknolojia mpya ya ufundi wa mitumbwi ya kisasa inayotumia vyuma na kuwasaidia kuhama kutoka kwenye teknolojia ya mbao iliyopitwa na wakati.

Wakieleza umuhimu wa elimu ya watu wazima baadhi ya wadau na viongozi wa taasisi za elimu hiyo mkoani Mwanza walisema suala la kujifunza halina mwisho, hivyo mtu yeyote anaweza kujifunza kwa wakati wowote ili kuongeza ujuzi na maalifa.

Mkurugenzi wa Chuo Kikuu Huria mkoani Mwanza, Dk. Ansfirida Prosper, alieleza kuwa kupitia chuo hicho kila mtu anaweza kuongeza elimu bila kujali umri wake na eneo analotokea ikiwa kupitia mfumo huo watu wanaweza kusoma wakiwa nyumbani ili kuepusha usumbufu wa mtu kuacha shughuli zake na kufunga safari kwenda kuifuata elimu nje ya eneo lake.

Alisema elimu ya watu wazima inahusisha elimu ya ujuzi na utaalamu katika fani mbalimbali kwa wale walioshindwa kuendelea na elimu rasmi kutokana na matatizo mbalimbali.

Mkutubi kutoka maktaba ya Mkoa wa Mwanza, Hadija Hassan, alieleza kuwa licha ya kuwekea vitabu vya kutosha watu bado wamekuwa wanasuasua katika usomaji wa vitabu hatua inayosababishia watu kukosa ujuzi.

Ofisa Tarafa wa Wilaya ya Sengerema, Happiness Segera, akizungumza katika Maadhimisho ya Wiki ya Elimu ya Watu Wazima yaliyofanyika wilayani Sengerema aliwaagiza wakurugenzi pamoja na wakuu wa wilaya kuweka mikakati kusimamia uboreshaji wa mazingira ya kujifunzia katika vituo vilivyoko katika maeneo yao.

Alisema maboresho hayo yaambatane na kuweka umeme wa uhakika ili kutatua matatizo ya wanafunzi wa elimu ya watu wazima katika mfumo usio rasmi ili kuwawezesha kufikia malengo yao ikiwa ni pamoja na kujiajiri.




Ofisa Maendeleo ya Jamii wa Manispaa ya Kahama, Robert Kwela, akimtwisha ndoo ya maji mmoja wa wanafunzi wa Shule ya Msingi Kilago, wakati wa ziara ya ukaguzi wa miradi ya maji, Kata ya Kilago juzi, iliyotekelezwa na Shirika la World Vision Tanzania. Wengine ni wananchi na baadhi ya watumishi wa shirika hilo. **PICHA: SHABAN NJIA**

## 'Msiwanyanyapae wenye ulemavu'

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

WADAU wa maendeleo mkoani Shinyanga wamewataka wazazi na walezi mkoani humo kuacha tabia ya kuwanyanyapaa watoto wenye ulemavu na kushindwa kuwapatia haki yao ya elimu.

Meneja Mradi wa Elimu Jumuishi kutoka Shirika la ADD International, Adam Mkaka alibainisha hayo juzi wakati wakikabidhi kompyuta mpakato (Laptop) kwa mashirika ambayo yanajihusisha na utetezi wa haki za watu wenye ulemavu mkoani Shinyanga na Mwanza.

Alisema tafiti zinaonyesha kuwa mikoa ya Kanda ya Ziwa inakabiliwa na tatizo la wazazi na walezi kuwabagua watoto wenye ulemavu katika suala la elimu.

Alisema wengine wanadiriki kuwaficha ndani na kuwaona watoto hao kama mkosi katika familia zao, kuwataka waachane na dhana hizo na kuwapeleka shule.

"Mradi wetu huu wa elimu jumuishi ni kuhakikisha watoto wote wenye ulemavu wanapata haki zao za kielimu na kuacha kubaguliwa ili kutimiza ndoto zao," alisema Mkaka.

Ofisa Ustawi wa Jamii Mkoa wa Shinyanga, Lidya Kwesigabo, alisema serikali itaendelea kushirikiana na wadau wa maendeleo katika kutatua matatizo ambayo yanawakabili watu wenye ulemavu.

Katibu wa Shirika la VODIWATA ambao ni miongoni mwa mashirika yaliyopewa kompyuta mpakato na shirika hilo, Yuel Mnyonge, alisema vifaa hivyo vitaongeza chachu ya utendaji kazi zao.

**"Mradi wetu huu wa elimu jumuishi ni kuhakikisha watoto wote wenye ulemavu wanapata haki zao za kielimu na kuacha kubaguliwa ili kutimiza ndoto zao," alisema Mkaka.**

# Shirika lajenga mradi wa maji kuokoa wajawazito

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

SHIRIKA la World Vision Tanzania limejenga mradi mkubwa wa majisafi na salama katika Kata ya Lyenye Manispaa ya Kahama, kuondoa adha ya upatikanaji maji kwa wajawazito wakati wakujifungua.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa mradi huo, Mwenyekiti anayesimamia mradi huo, Kilago Daudi alisema awali wajawazito walikuwa wakilazimika kubeba ndoo za maji kutoka nyumbani kwao mpaka kituoni.

"Ilikuwa ukifika kituo kabla ya kukaguliwa vifaa vya kujifungulia lazima waangalie kama una ndoo ya maji na usipokuwa nayo ilikubidi mume alete maji, magonjwa ya kipindupindu na kuumwa matumbo yalikuwa mengi kwa kutumia maji ambayo siyo safi na salama," alisema Daudi.

Diwani wa Kata ya Lyenye, Lucas Makulumo, alisema kwa sasa wananchi wanatumia maji yaliyo salama tofauti na awali ya kwenye visima na madimbwi yaliyoko jirani na mashamba ya mpunga.

Aliliomba shirika hilo kupeleka pia huduma hiyo katika shule za msingi na sekondari wilayani humo.

Mratibu wa Mradi wa Kilago-Lyenze, Dominick Mbamba, alisema wamekuwa wakitekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo kulingana na mahitaji ya wananchi wa eneo husika, hivyo jukumu lililobaki ni kuitunza na kutumia vema ili iendelee kuwanufaisha.

Alisema miradi yote inapokamilika humkabidhi Mkurugenzi wa Halmashauri kwa hatua nyingine za uendelezaji na kuwashauri kuhakikisha wanatenga bajeti na kupeleka huduma ya maji katika shule za msingi na sekondari zisizokuwa na huduma ya maji ili kuwanusuru wanafunzi na magonjwa.

Kaimu Mkurugenzi wa Manispaa ya Kahama, Robert Kwela, alisema mwaka ujao wa fedha watahakikisha wanatenga fedha kwa ajili ya kupeleka huduma ya maji katika shule za msingi na sekondari ambazo hazina huduma na kuwataka wananchi kusimamia na kuitunza miradi hiyo isiharibike.

## HABARI KIMATAIFA

# Liz Truss ajiuzulu uwaziri mkuu, kaongoza Uingereza siku 45

**LONDON, Uingereza**

BAADA ya kukalia kiti cha uwaziri mkuu wa Uingereza kwa siku 45 pekee, Liz Truss ametangaza kujiuzulu nafasi hiyo baada ya kuibuka mgogoro ndani ya chama chake.

Katika taarifa yake kwa vyombo vya habari nje ya ofisi yake namba 10, Truss alisema aliingia ofisini hapo wakati wa machafuko makubwa ya kiuchumi na kimataifa. Alisema kutokana na hali iliyopo ndani ya chama chake hawezi kutoa mamlaka aliyochaguliwa na wajumbe Tory na anajiuzulu.

Liz Truss aliendelea kusema kwamba alikutana na mwenyekiti wa Kamati ya 1922, Sir Graham Brady jana na kukubaliana kutakuwa na uchaguzi wa viongozi ndani ya wiki ijayo, na atasalia kama waziri mkuu hadi mrithi wake atakapochaguliwa.

Kabla ya kuchukua hatua hiyo, siku mbili mfululizo Liz Truss, alikuwa katika shinikizo kali la kutakiwa kujiuzulu kutoka kwa wabunge wa chama chake wakiishutumu serikali yake kwa kukiaibisha chama hicho kwa kukielekeza katika mgogoro.

Waziri wa mambo ya ndani, Suella Braverman alijiuzulu juzi jioni na kuwa wa pili kuondoka katika baraza la Liz Truss.

Awali Waziri wa Fedha, Kwasi Kwarteng aliondolewa katika wadhifa wake siku tano zilizopita.

Kwarteng, mshirika wa karibu kisiasa wa Truss aliponzwa na bajeti ndogo aliyoitangaza, ambayo iliitumbukiza Uingereza katika mgogoro wa kifedha na kukosolewa vikali kutoka ndani na nje ya Uingereza.

Kikao cha juzi cha bunge cha maswali na majibu kwa waziri mkuu Liz Truss, kilizidisha shinikizo kwa kiongozi huyo ambaye amedumu kwa miezi miwili katika nafasi hiyo.

Kura kurejeshwa kwa utaratibu wenye utata wa kuchimbwa gesi chini ya miamba, inayoungwa mkono na waziri mkuu lakini inapingwa vikali na chama cha upinzani cha Labour na wabunge wengi wa chama tawala cha Conservative ndio ilikuwa kiini cha mzozo huo.

Liz Truss asema hang'oki mtu

Awali, Truss ambaye alitetereshwa na hatua ya waziri wake mpya wa fedha kufuta mipango yote ya uchumi iliyokuwa ahadi za kampeni ya serikali yake, alijitutumua bungeni pale upinzani ulipohoji ikiwa sera zake zimeshindwa, na yeye pia anapaswa kufungasha virago.

Truss aliwajibu kwamba hawezi kung'oka kwa sababu naye anajua kupigana.

"Bwana Spika, mimi ni mpambanaji, siendi kokote. Maamuzi yangu ni kwa maslahi ya taifa, kuhakikisha tunao utengamano kiuchumi." Alijibu kwa ukali.

Wabunge wa Conservative walitishiwa kufukuzwa uanachama iwapo wangeungana na upinzani kuipitisha kura ya kutokuwa na imani, huku mnadhimu mkuu wa chama hicho tawala akisema kura hiyo ingechukuliwa kama ya imani kwa serikali, kwa maana kwamba kama kura hiyo ingepita, waziri mkuu Liz Truss angeondoka.

Hatua ya mwisho Conservative chenye wingi wa viti bungeni kilishinda, lakini namna wabunge wa walivyoshinikizwa iliacha mgawanyiko.

Kulikuwepo madai ya baadhi ya wabunge, kuwa mabavu yalitumika kuwashinikiza wahafidhina kumuunga mkono waziri mkuu.

Hali hiyo iliwafanya baadhi ya wabunge wa muda mrefu wa chama hicho kusema wamepoteza imani na mwelekeo wa chama chao, na kutaka waziri mkuu atimuliwe.

Mmoja wa wabunge hao ni Gary Streeter, ambaye kupitia mtandao wa twitter alisema kuwa hata ikiwa wataweza kumbakiza Liz Truss, chama cha Conservative kitahitaji muujiza kuweza kurejesha nidhamu na kuiongoza ipasavyo Uingereza.

Shinikizo dhidi ya waziri mkuu huyo limeendelea hadi jana baada ya mbunge mwingine wa chama chake, Sheryll Murray kuarifu kuwa amewasilisha kwenye kile kiitwacho kamati ya 1922, barua yake ya kutokuwa na imani na uongozi wa Liz Truss.

Kamati hiyo ndio yenye dhamana ya kuweka utaratibu wa kuwabadilisha viongozi wa chama cha Conservative.

***DW***

# Russia yahamishia mitambo mizito Ukraine

**WASHINGTON, Marekani**

GAZETI la Marekani la New York Times, limedai Russia imehamisha sehemu kubwa ya kikosi chake nchini Syria na mifumo ya makombora ya kupambana na ndege ya S-300 na kukipeleka Ukraine.

Madai hayo yanatokana na vyanzo mbalimbali vya nchi za Magharibi na Israel, ambavyo vinaeleza uamuzi huo ni katika kuhimili mapambano yanayoendelea katika uwanja wa vita dhidi ya wanajeshi wa Ukraine ambao wanapata mafanikio.

Wanadiplomasia wawili wa nchi za Magharibi na ofisa mmoja mkuu wa kijeshi wa Israel waliliambia gazeti hilo, kwa sharti la kutotajwa jina, kwamba Russia imeondoa vikosi viwili kutoka Syria, ambao ni wanajeshi 1,600.

Lakini jarida hilo linaona muhimu zaidi ni kwamba Russia inasemekana kupeleka mifumo hiyo ya kutungua ndege Ukraine.

"Hofu kwamba S-300 inaweza kutumika dhidi ya ndege za Israeli imekuwa sababu kuu kwa nini Israeli hadi sasa imekataa ombi la Ukraine la silaha," gazeti hilo liliandika.

Ripoti ambazo hazijathibitishwa rasmi kwamba Russia inahamisha au inajiandaa kuhamisha sehemu ya kikosi chake cha nchini Syria hadi Ukraine zilionekana mara kwa mara wakati wa vita kwa mwezi Mei na Septemba.

Ukraine yajiandaa kukatika umeme

Wakati huo huo, Ukraine inadhibiti matumizi ya umeme kama sehemu ya kujibu mashambulizi ya Russia kwenye miundombinu ya nishati ambayo yamezua hofu kuhusu jinsi nchi hiyo ilivyokumbwa na vita itakavyojimudu wakati wa msimu wa baridi kali.

Kampuni ya kitaifa ya nishati Ukrenergo, iliwaambia raia wa nchi hiyo kuchaji simu na betri, na kuhakikisha wana tochi tayari, kabla ya kuanza kukatwa kwa umeme kuanzia jana kwa muda wa masaa manne.

***BBC***


**MAMLAKA YA VITAMBULISHO VYA TAIFA**

## TAARIFA KWA UMMA

**UFAFANUZI KUHUSU PICHA YA KITAMBULISHO INAYOSAMBAZWA KWENYE MITANDAO YA KIJAMII YA MTU MWENYE ASILI YA CHINA.**

***Dar es Salaam; Oktoba 20, 2022.***

Kumekuwa na picha ya Kitambulisho cha Taifa cha mtu mmoja mwenye asili ya China aitwaye ZHU JIN FENG kilichotolewa na Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA) ambayo inasambaa katika mitandao ya Kijamii na kuzua maswali na hisia tofauti kuhusu uhalali wa Kitambulisho hicho kwa mtu huyo.

Awali ya yote, ifahamike kuwa Kitambulisho cha Taifa hutolewa kwa makundi matatu ambayo ni Raia (Citizens), Wageni wakaazi (Legal residents) na Wakimbizi (Refugees) wanaoishi kihalali nchini na wanaotambuliwa na Serikali na Shirika la Umoja wa Mataifa la kuhudumia Wakimbizi (UNHCR).

Katika kundi la Raia (Citizens) kuna makundi pia ya wanaopaswa kupata Vitambulisho vya Taifa ambayo ni wenye Uraia wa kuzaliwa, Uraia wa Kurithi na Uraia wa Tajnisi . Kundi hili la Uraia wa Tajnisi ni kwa raia wa nchi nyingine yeyote ile walioomba uraia wa Tanzania na kukidhi vigezo vya kupewa Uraia huu kwa mujibu wa sheria.

Hivyo basi, tunapenda kuujulisha Umma kuwa Kitambulisho cha Bw. FENG ambacho kimekuwa kikisambazwa katika mitandao ya Kijamii ni Kitambulisho halali cha raia wa Tanzania alichokipata kupitia Uraia wa Tajnisi kama ilivyoelezwa hapo juu katika aina za Uraia baada ya kukidhi vigezo vyote ikiwa ni pamoja na kuukana Uraia wake wa China na baada ya kufuata taratibu zote kwa mujibu wa Sheria ya Usajili na Utambuzi wa watu nchini.

Aidha, katika Kitambulisho hicho kuna picha ndogo ya kichwa cha mtoto iliyojitokeza kidogo juu kushoto. Picha hiyo si sehemu ya Kitambulisho hicho bali imepachikwa na waliofanya hivyo kwa njia ya photo editing ili kuonyesha hisia za kushangaa pengine kwa kudhani si Kitambulisho halali kwa mtu huyo na hasa kwa kuzingatia kuwa ni mwenye asili ya China.

Tunapenda kuwahakikishia wananchi kwamba Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa inatekeleza majukumu yake kwa makini na kwa mujibu wa sheria ya Mwaka 1986 na marejeo yake ya mwaka 2012, pamoja na Kanuni za Usajili na Utambuzi za mwaka 2014. Pamoja na Kusajili na kutambua watu wanaoishi nchini, Mamlaka ina jukumu pia la kutoa Vitambulisho vya Taifa kwa raia, wageni wakaazi na wakimbizi wanaoishi nchini kihalali

**Geofrey Tengeneza**
**Msemaji wa Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa**

217106402

# H-BABA AMTETEA HARMONIZE

**Na Mwandishi Wetu**

MSANII wa muziki wa Bongofleva, H-Baba ambaye hivi karibuni alionekana kuwa kinyume na aliyekuwa bosi wake kwenye Lebo ya Konde Gang, Harmonize, amemtetea huku akimuumbua mtangazaji maarufu wa radio, Mwijaku.


H-Baba amtetea Harmonize dhidi ya matamshi ya Mwijaku aliingia katika sebule yake na kumkuta Paula Kajala akimkanda kifuani.

H Baba amesema Mwijaku hajaonyesha tabia nzuri kwa kuingia kwenye sebule za watu na kuanza kutoa mambo ya ndani mwa watu na kuyaweka wazi kwa umma.

Harmonize kwa sasa yupo katika mapenzi na Kajala ambaye ni mama wa Paula.

Anasema katika hilo anamtetea Harmonize kwa vile mambo ambayo wanafaa kuchafuana ni ya nje tu na wala si ya ndani ambayo yanapaswa kubaki kuwa siri za watu husika wenyewe.

Aidha H Baba amekanusha madai huenda Mwijaku ametumwa na Diamond ili kumchafulia jina Harmonize na kusema hana namba ya Diamond.




## FILAMU YA NYARA YAPENYA NETFLIX

**Na Mwandishi Wetu**

FILAMU ya Nyara kutoka Tanzania imefanikiwa kuingia kwenye Netflix Global ambapo itaweza kuonekana duniani kote.

Nyara ni filamu ambayo imetayarishwa hapa nchini huku waigizaji na waandaji wakiwa ni Watanzania.

"Tuna furaha kuwatangazia, ile filamu yetu pendwa ya mapigano ya Nyara sasa inapatikana Netflix duniani kote," ilisema taarifa ya waandaaji wa filamu hiyo, Wanene Studios.

"Ni filamu ambayo imeandaliwa nchini Tanzania uanzia kuanzia Waigizaji na timu nzima ya waandaaji, na tunajivunia sana kwa kila mmoja ambaye aliweza kushiriki katika kuandaa filamu hii. Shukrani zetu kwa Okada Media, wasambazaji wetu wakuu," iliongeza taarifa hiyo.

"Ilikuwa ni safari ndefu sana lakini Mungu Ametenda. Tumefanikiwa. Hongereni sana Waigizaji wote na timu nzima ya waandaaji. Tanzania Wanene Studios ."

## VACANCIES ANNOUNCEMENT -READVERTISED

Air Tanzania Company Limited (ATCL) is expanding its network to meet the needs of its Business Strategy which focus on sustaining the recorded achievements and remain an airline of choice that meets and exceeds customers' expectations in line of its mission of provision of reliable, safe and high-quality services. Therefore, applications are invited from qualified Tanzanians to fill the positions mentioned below:

**1. POSITION: AVIATION SECURITY ASSISTANT II (2 POSTS)**

**1.1 QUALIFICATIONS**

- Must be a holder of an Advanced Secondary School Certificate or a Diploma preferably in Law plus training/certification on military/militia or its equivalent qualifications from recognized iinstitution.
- Must have Aviation Security Screener Training
- Training in Cargo and Mail Security, Airport Security or Security Quality Control will be an added advantage.

**1.2 RESPONSIBILITIES:**

- Ensure proper access control of staff, authorized persons and vehicles to aircrafts
- Conduct aircraft security searches and checks as appropriate
- Ensure that security personnel from outsourced security service providers are appropriately deployed and supervised to ensure for security of aircrafts, passengers, baggage, cargo and mail.
- Ensure Revenue Integrity.
- Report and record all incidents in the OB for management follow up
- Brief and debrief outsourced security on security matters to ensure they understand and implement the instructions.
- Ensure safe and secure handling and carriage of firearms in compliance with company security program
- Prepare daily shift security operations report to ensure that there is proper follow up and action on any issues arising in course of duty.
- Ensure safe custody and accountability of Lost and Found property until reclaimed by the rightful owner or otherwise disposed off according to company policy.
- Act as duty shift in-charge
- Perform any other official duty as may be assigned by your Supervisor

**2. TERMS AND CONDITIONS:**

Five (5) years contract with attractive remuneration and Fringe Benefits as per ATCL Salary structure and Incentive Scheme.

**3. MODE OF APPLICATION:**

Interested applicants must submit a dully signed letter for consideration of the applications attached with the following:

i. A detailed curriculum vitae (CV);
ii. Certified copies of all certificates (including Secondary School and birth certificate), and other relevant certificates and licenses. (Tanzanian applicants who have studied outside Tanzania should have their certificates approved by relevant authorities i.e Tanzania Commission for Universities (TCU) or National Examination Council- NECTA))
iii. Two recent passport size photographs;
iv. Names and addresses of at least two reputable referees;
v. Applicant's reliable contact address, email address and telephone numbers.
vi. The applicant must indicate willingness to work upcountry when need be.

Note: Misrepresentation of facts and qualifications during application shall warrant legal consequences. Previous applicants may re-apply.

**4. CLOSING DATES:**

Applicants should reach the undersigned within 14 days from the first date of this announcement: -

**MANAGING DIRECTOR & CHIEF EXECUTIVE OFFICER**
**AIR TANZANIA COMPANY LIMITED,**
**P.O. BOX 543,**
**DAR ES SALAAM**

217106102

**Welcomes you, to where you can Fly**

# KAGERE, PLUIJM WAAHIDI KUIMALIZA KAGERA SUGAR

**Shufaa Lyimo na Hadija Mngwai**

MSHAMBULIAJI wa Singida Big Stars, Meddie Kagere, amesema amejipanga vyema kuhakikisha timu hiyo inapata ushindi katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Ihefu FC itakayochezwa Jumatatu kwenye Uwanja wa CCM Liti, mkoani Singida.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kagere alisema lengo kuhitaji ushindi katika mechi hiyo ni kuendelea kujiimarisha kwenye msimamo wa ligi hiyo ya juu na inayotoa mwakilishi wa nchi katika mashindano ya kimataifa.

Kagere alisema kila mchezaji anafahamu umuhimu na faida ya kupata ushindi kwenye uwanja wa nyumbani, hivyo wamejipanga kuonyesha kiwango bora na kuwafurahisha mashabiki wao.

"Nimejipanga kuhakikisha tunapambana na kupata ushindi katika mchezo wetu ujao, timu yangu inahitaji kujituma zaidi baada ya kupoteza mchezo uliopita, kwa upande wangu sijakata tamaa," alisema Kagere.

Aliongeza ligi ya msimu huu ina ushindani sana kwa sababu kila timu ilijiandaa vizuri na zimejipanga kupata pointi tatu iwe nyumbani au ugenini.

"Ushindani msimu huu ni mkubwa, kila timu imejipanga vizuri kuhakikisha haishuki daraja, hali hii inazidisha ushindani, sisi pia tumejipanga kumaliza katika nafasi ya juu," Kagere alisema.

Aliongeza anashukuru anapata ushirikiano mzuri kutoka kwa mashabiki wa timu hiyo tangu alipojiunga nayo.

Naye Kocha Mkuu wa Singida Big Stars, Hans van Pluijm, alitaja sababu iliyosababisha timu yake kupoteza mechi ni mastraika kushindwa kutumia vyema nafasi za kufunga walizopata. Pluijm alisema wamekuwa wakitengeneza nafasi nyingi lakini nyota wake wanashindwa kuzitumia na kusababisha kupoteza ushindi.

"Kupoteza michezo miwili mfululizo kunatokana na kushindwa kufunga wakati tunatengeneza nafasi nyingi, ukifanya kosa moja wapinzani wanalitumia kwa kushambulia na kufunga. Nitahakikisha mchezo unaofuata dhidi ya Kagera Sugar tunapata matokeo mazuri," alisema Pluijm.





Wanariadha wakichuana katika mbio za mita 1,500 katika Tamasha la Tanzanite lililofanyika kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam jana. Salma Charles alishika nafasi ya kwanza katika umbali huo baada ya kutumia saa 4:40: 04. **PICHA: SAADA AKIDA**

# Azam FC yaitangazia vita KMC

**Na Shufaa Lyimo**

TUNAZITAKA pointi tatu, hayo ni maneno ya makocha, Thierry Hitimana wa KMC FC na Kally Ongala wa Azam, kuelekea mechi yao ya Ligi Kuu Tanzania Bara itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam.

Katika mchezo huo KMC wanashuka dimbani wakiwa na kumbukumbu ya kuifunga Mtibwa Sugar mabao 2-0 huku Azam FC ikiwa na machungu ya kuondolewa katika mashindano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika na Al Akhdar ya Libya.

Hitimana alisema wachezaji wake wote wana morali ya hali ya juu kuelekea katika mchezo huo.

"Lengo letu ni kupata pointi tatu katika mchezo huu, tunawaheshimu wapinzani wetu na tunafahamu hivi karibuni wametolewa kwenye mashindano ya kimataifa, tunajua hautakuwa mchezo rahisi," alisema Hitimana.

Naye Ongala, alisema wachezaji wake wapo katika hali nzuri na wale ambao walikuwa majeruhi hali zao zinaendelea kuimarika.

Ongala alisema wamejipanga kuhakikisha wanamaliza unyonge dhidi ya KMC FC kwa kuhakikisha wanaondoka na pointi zote tatu muhimu katika mechi hiyo.

# Zimamoto yazidi kutakata Zanzibar

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

ZIMAMOTO imeendelea kufanya vizuri baada ya kuichapa Black Sailor mabao 3-2 katika mechi ya Ligi Kuu Zanzibar iliyochezwa kwenye Uwanja wa Amaan, juzi jioni.

Matokeo hayo yameifanya Zimamoto kufikisha pointi 14 huku ikizidi kuzamisha jahazi la Black Sailor ambayo imepoteza mechi saba mpaka sasa katika msimu huu unaoendelea.

Kocha Mkuu wa Zimamoto, Mohamed Ali Hilali, alisema mipango ya timu yake ni kuhakikisha wanashinda kila mchezo ili kujiweka kwenye mbio za kuwania ubingwa wa ligi hiyo ya juu Zanzibar.

Kocha huyo alisema awali timu hiyo haikuanza vyema msimu katika michezo yake minne ya mwanzo lakini hivi sasa imeimarika na imeshinda mechi tatu mfululizo.

Aliongeza malengo yake ni kumaliza mzunguko wa kwanza wakiwa kileleni mwa ligi hiyo inayotoa tiketi ya kushiriki mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

# Balozi Royal Tour aandaa matembezi

**Na Mwandishi Wetu**

MSANII wa muziki wa bongofleva, Masoud Masandae, ameandaa matembezi maalumu yatakayofanyika kesho kwa ajili ya kuunga juhudi zinazofanywa na Rais Samia Suluhu Hassan katika filamu ya Tanzania Royal Tour, imefahamika.

Masandae alisema maandamano hayo yatafanyika kuanzia kwenye Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Mwalimu Julius Nyerere hadi katika Taasisi ya Saratani ya Ocean Road.

"Katika matembezi hayo nitagawa mafuta maalumu ya kuzuia jua (Sun-skin lotion), kwa ndugu zetu wenye ulemavu wa ngozi, walioathirika na kansa ya ngozi ambao wanatibia katika hospitali hiyo," alisema msanii huyo ambaye ni mlemavu wa ngozi.

Aliongeza ameamua kujitokeza kuitangaza filamu hiyo kwa sababu ina umuhimu mkubwa kwa taifa na dunia.

"Mimi nimejitolea kuwa balozi wa kuitangaza filamu hii, matembezi yangu haya ni sehemu ya kuhamasisha watu kuitizama filamu lakini pia kuchangamkia fursa zinazokuja ndani na nje ya nchi," msanii huyo alisema.

## ZISIKUPITE

### OSIMHEN ATAJWA CHELSEA
KLABU ya Chelsea ina mpango wa kusajili mshambuliaji mpya katika msimu ujao wa joto na mchezaji wa kimataifa wa Napoli mwenye umri wa miaka 23, Victor Osimhen ametajwa kivutio zaidi huku wakifikiria wachezaji wengine pia. ***(90 Min)***

### BELLINGHAM AZIDI KUWINDWA
KIUNGO wa kati wa Borussia Dortmund, Jude Bellingham mwenye umri wa miaka 19, ameibuka kama mchezaji mwingine anayelengwa zaidi na Chelsea. ***(Evening Standard)***

### ENDRICK AGEUKA LULU
ARSENAL inaweza kushindana na Barcelona na Real Madrid katika mbio za kumsajili mshambuliaji wa Palmeiras, Endrick mwenye umri wa miaka 16, ambaye amepewa jina la "Pele ajaye". ***(FourFourTwo)***

### HAG BADO AJIFIKIRIA
KOCHA wa Manchester United, Erik ten Hag anachelewesha uamuzi kuhusiana na hatima ya mkataba wa kipa wa Timu ya Taifa ya Hispania, David de Gea, mwenye umri wa miaka 31. ***(Guardian)***

### GAKPO AIWAZA UNITED
WINGA wa PSV Eindhoven, Cody Gakpo, mwenye umri wa miaka 23 amesema uhamisho wa kwenda Manchester United ulishindikana msimu wa joto, huku Leeds United na Southampton pia zikimhitaji mchezaji huyo wa kimataifa wa Uholanzi kabla ya kuamua kusalia na klabuni hapo. ***(Times)***

### BARCA YAMTAKA DALOT
KLABU ya Barcelona inafuatilia hali ya beki wa kulia wa Manchester United na Timu ya Taifa ya Ureno, Diogo Dalot mwenye umri wa miaka 23, ambaye mkataba wake utakamilika msimu ujao wa joto. ***(Mundo Deportivo)***

### UNITED KUTOSAJILI JANUARI
MKURUGENZI wa soka wa Manchester United, John Murtough, amezima matumaini ya uhamisho wa Januari kwa kusisitiza Mashetani Wekundu hao wanafikiria zaidi dirisha lijalo la joto. ***(Telegraph)***

### TRAORE AITAMANI HISPANIA
WINGA wa Wolves, Adama Traore mwenye umri wa miaka 26, amesema anatumaini siku moja atarejea kucheza katika nchi yake ya Hispania. ***(AS)***

### GOMEZ ANUKIA ENGLAND
KOCHA wa Timu ya Taifa ya England, Gareth Southgate atafuatilia kiwango cha mchezo cha beki wa kati wa Liverpool, Joe Gomez mwenye umri wa miaka 25, kabla ya kutaja kikosi chake kitakachokwenda kwenye fainali za Kombe la Dunia huko Qatar. ***(Times)***

### CARRICK MAMBO SAFI
KIUNGO wa kati wa zamani wa Manchester United na England, Michael Carrick mwenye umri wa miaka 41, anatarajiwa kuteuliwa kuwa kocha mpya wa Middlesbrough baada ya kuafikiana na klabu hiyo inayoshiriki Ligi ya Championship. ***(Mail)***

### ZAHA KUPEWA MKATABA
KOCHA wa Crystal Palace, Patrick Vieira amesema timu hiyo ipo kwenye mazungumzo ya kuongeza mkataba wa mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Ivory Coast, Wilfried Zaha mwenye umri wa miaka 29. ***(Metro)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# TEN HAG AFUNGUKA 'ATADILI' NA RONALDO

●●● Ni baada ya Mreno huyo kuonyesha kitendo cha utovu wa nidhamu dakika chache...

**MANCHESTER, England**

KOCHA wa Manchester United, Erik ten Hag amesema "nitadili na" Cristiano Ronaldo baada ya mchezaji huyo ambaye hakutumika kuondoka uwanjani dakika chache kabla ya ushindi dhidi ya Tottenham Hotspurs, hapo juzi.

Ronaldo mwenye umri wa miaka 37, aliondoka dakika ya 89, muda mfupi baada ya Ten Hag kuwaingiza Christian Eriksen na Anthony Elanga.

"Nitalishughulikia hilo kesho (leo), sio leo (juzi). Sasa tunasherehekea ushindi huu," alisema Ten Hag.

"Nimemwona, lakini sijazungumza naye."

Licha ya United walikuwa wamebadilisha wachezaji watatu pekee kati ya watano walioruhusiwa katika mechi ya nyumbani iliyomalizika kwa ushindi wa mabao 2-0, Ronaldo aliamua kuondoka katika benchi mapema pale pale kwenye Uwanja wa Old Trafford.

Hili lilitokea siku tatu baada ya kuonyesha kutofurahishwa na kubadilishwa kwenye mchezo dhidi ya Newcastle Jumapili.

Baada ya suluhu, Ten Hag alisema "hana tatizo" na majibu hasi ya Ronaldo, lakini akaongeza Mreno huyo lazima aonyeshe kiwango.

Mshambuliaji zamani wa Timu ya Taifa ya England, Gary Lineker alisema tabia ya Ronaldo sio ya kufurahisha.

"Samahani, hiyo haikubaliki - ni mbaya sana," alisema Lineker.

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,042,0

MECHI KALI

AC AJACCIO
VERSUS
PARIS ST GERMAIN

1 | 9.98
X | 5.08
2 | 1.29

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.

tigo pesa
vodacom m-pesa
airtel money

SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#

GBT:0249 18+
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA:
0764115588, 0677115588
0685115588

@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



# ZIDANE ASEMA BENZEMA STRAIKA BORA UFARANSA

**PARIS, Ufaransa**

ZINEDINE Zidane amekiri, Karim Benzema ndio mshambuliaji bora zaidi wa Ufaransa.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 34 alitunukiwa tuzo ya Ballon d'Or ya 2022 Jumatatu usiku baada ya msimu mzuri akiwa na Real Madrid, msimu ambao ulimshuhudia akifunga mabao 44 na kutoa asisti 15 katika mechi 46 na kushinda LaLiga na Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Benzema alifunga hat-trick dhidi ya Paris Saint-Germain na magoli muhimu dhidi ya Manchester City katika hatua ya mtoano wa Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Mafanikio ya Ballon d'Or yalimfanya Benzema kuwa mchezaji wa kwanza wa Ufaransa kushinda taji hilo tangu alipochukua Zidane mwaka 1998.

Pia ni mchezaji wa tano wa Ufaransa kushinda tuzo hiyo baada ya Michel Platini, Jean-Pierre Papin na Raymond Kopa.

Katika mahojiano maalum na jarida la L'Equipe la Ufaransa, Zidane alisema Benzema ndio mshambuliaji bora zaidi wa Ufaransa.

Pia alikiri kwamba anamchukulia mshambuliaji huyo wa zamani wa Lyon kuwa mshambuliaji bora zaidi kuwahi kutokea nchini Ufaransa. Zidane pia alizungumzia mchango wa Benzema katika kazi yake kama kocha na alizungumzia kuhusu uthabiti wake wa ajabu katika miaka michache iliyopita.

# Conte : Spurs inahitaji kuimarika

**LONDON, England**

ANTONIO Conte amekiri Tottenham Hotspurs lazima ifanye vyema katika mechi kubwa baada ya kuchapwa mabao 2-0 na Manchester United hapo Jumatano.

Mabao ya Fred na Bruno Fernandes yaliiwezesha United kuondoka na pointi zote tatu katika mchezo huo.

Spurs wameanza vyema msimu huu na bado wanashika nafasi ya tatu kwenye msimamo, kwa pointi sawa na Manchester City wanaoshika nafasi ya pili na watatu mbele ya Chelsea walio katika nafasi ya nne.

Hata hivyo, akizungumza na Amazon Prime, Conte alisema timu yake inapaswa kujipanga zaidi.

"Tunajitahidi. Tulipambana dhidi ya Chelsea, tulipambana dhidi ya Arsenal, tulijitahidi leo (juzi) dhidi ya United."

Spurs walipiga mashuti 28 langoni mwao kutoka kwa wenyeji, yakiwamo 19 katika kipindi cha kwanza.

"United walistahili kushinda, walicheza mchezo mzuri sana," alisema Conte.



026,796/-

SUPA JACKPOT
MECHI WIKI HII
BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 22/10/22 | 17:00 | Everton vs Crystal Palace | 2.46 | 3.19 | 2.89 |
| 02. 22/10/22 | 17:00 | Sunderland vs Burnley | 2.88 | 3.23 | 2.45 |
| 03. 22/10/22 | 17:00 | Sheffield Utd vs Norwich City | 2.55 | 3.25 | 2.75 |
| 04. 22/10/22 | 17:00 | Millwall vs West Bromwich | 2.78 | 3.23 | 2.53 |
| 05. 22/10/22 | 17:00 | Reading vs Bristol City | 2.40 | 3.24 | 2.94 |
| 06. 22/10/22 | 20:00 | Niort vs Dijon | 2.73 | 3.18 | 2.68 |
| 07. 22/10/22 | 21:30 | Arminia Bielefeld vs St. Pauli | 2.89 | 3.44 | 2.33 |
| 08. 23/10/22 | 14:30 | Karlsruher SC vs Fortuna Dusseldorf | 2.34 | 3.43 | 2.89 |
| 09. 23/10/22 | 16:00 | Wolverhampton vs Leicester | 2.25 | 3.38 | 3.08 |
| 10. 23/10/22 | 16:00 | Clermont Foot vs Brest | 2.41 | 3.27 | 2.87 |
| 11. 23/10/22 | 16:00 | Troyes vs Lorient | 2.42 | 3.37 | 2.78 |
| 12. 23/10/22 | 17:15 | Betis vs Atletico Madrid | 3.08 | 3.23 | 2.32 |
| 13. 23/10/22 | 17:30 | CS Maritimo vs FC Arouca | 2.59 | 3.24 | 2.69 |
| 14. 23/10/22 | 19:30 | Girona vs Osasuna | 2.58 | 3.08 | 2.83 |
| 15. 23/10/22 | 20:00 | GD Chaves vs Gil Vicente | 2.45 | 3.34 | 2.79 |
| 16. 23/10/22 | 21:45 | Lille vs Monaco | 2.46 | 3.52 | 2.63 |
| 17. 23/10/22 | 21:45 | Roma vs Napoli | 2.83 | 3.47 | 2.36 |

MECHI ZA USHINDI
"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE
"2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

IJUMAA - 21/10/2022

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:30 | 1202 | Peykan FC vs Havadar | 2.61 | 2.57 | 3.05 |
| 14:45 | 4886 | Lion City Sailors vs Young Lions | 1.04 | 10.71 | 21.42 |
| 14:45 | 5234 | Geylang Int. vs Albirex Niigata (SIN) | 5.25 | 5.25 | 1.39 |
| 15:00 | 3131 | Chiangrai Utd vs Nakhon Ratchasima | 1.62 | 3.75 | 4.67 |
| 15:55 | 1667 | Masfoot Sports Club vs AL Arabi | 4.36 | 3.73 | 1.66 |
| 16:00 | 1043 | Kagera Sugar vs Singida BS FC | 2.32 | 2.63 | 3.46 |
| 16:00 | 1842 | Ahi Nazareth vs Hapoel Afula | 3.25 | 3.25 | 2.20 |
| 16:00 | 2154 | Ironi Hasharon vs Hapoel Petah Tikva | 3.00 | 2.90 | 2.55 |
| 16:00 | 4737 | KMC vs Azam | 3.16 | 2.77 | 2.37 |
| 16:00 | 5620 | Police FC Rwanda vs Etincelles | 1.91 | 3.06 | 3.98 |
| 16:30 | 2346 | Esteghlal Tehran vs Aluminium Arak | 1.82 | 2.91 | 4.86 |
| 16:30 | 4413 | Gol Gohar vs Zob Ahan | 1.95 | 2.83 | 4.29 |
| 17:00 | 2119 | USM Khenchela vs MC Alger | 2.96 | 2.58 | 2.67 |
| 17:00 | 3660 | Chennaiyin FC vs FC Goa | 2.82 | 3.36 | 2.23 |
| 17:00 | 3941 | Ararat Armenia vs Ararat Yerevan | 1.55 | 3.70 | 5.45 |
| 17:00 | 4212 | ASO Chlef vs RC Arbaa | 2.09 | 2.97 | 3.50 |
| 17:00 | 4501 | El Bayadh vs Paradou AC | 2.13 | 2.73 | 3.80 |
| 17:00 | 4823 | CS Constantine vs US Biskra | 1.55 | 3.34 | 6.40 |
| 17:00 | 5588 | USM Alger vs JS Saoura | 1.55 | 3.40 | 6.21 |
| 17:00 | 5738 | CR Belouizdad vs MC Magra | 1.19 | 5.26 | 14.61 |
| 18:00 | 4344 | Shirak Gyumri vs Pyunik Yerevan | 5.25 | 3.74 | 1.56 |
| 19:00 | 2590 | JS Kabylie vs ES Setif | 2.62 | 2.62 | 2.96 |
| 19:00 | 3645 | Olympiakos Nicosia vs Apollon Limassol | 4.71 | 3.70 | 1.70 |
| 19:00 | 4155 | AS Kigali vs APR FC | 3.30 | 2.85 | 2.40 |
| 19:00 | 5096 | Hajduk Split vs Dinamo Zagreb | 2.82 | 3.30 | 2.26 |
| 19:10 | 4005 | FC Liefering vs Rapid Vienna II | 1.91 | 3.85 | 3.16 |
| 19:30 | 1521 | SV Darmstadt vs Holstein Kiel | 1.66 | 3.82 | 4.66 |
| 19:30 | 5394 | Hansa vs Kaiserslautern | 2.97 | 3.32 | 2.26 |
| 20:00 | 1801 | Sonderjyske vs Hillerod | 1.34 | 4.76 | 6.99 |
| 20:00 | 2371 | Odense vs Lyngby | 2.07 | 3.43 | 3.33 |
| 20:00 | 2749 | Antalyaspor vs Istanbulspor | 1.70 | 3.73 | 4.57 |
| 20:30 | 1396 | Nancy vs Saint Brieuc | 1.89 | 3.35 | 3.89 |
| 20:30 | 1754 | Le Puy vs Avranches | 2.15 | 3.25 | 3.20 |
| 20:30 | 1995 | Bastia Borgo vs Chateauroux | 3.95 | 3.35 | 1.87 |
| 20:30 | 2019 | Le Mans vs FC Martigues | 2.09 | 3.35 | 3.25 |
| 20:30 | 4999 | Rapid Bucuresti vs Farul Constanta | 2.57 | 3.02 | 2.77 |
| 21:15 | 3297 | Lausanne-Sport vs FC Thun | 1.76 | 3.85 | 3.66 |
| 21:30 | 2800 | Hibernian vs St Johnstone | 1.58 | 3.78 | 5.58 |
| 21:30 | 5483 | Mainz vs FC Koln | 2.17 | 3.42 | 3.07 |
| 21:45 | 1302 | UCD Dublin vs Drogheda Utd | 2.78 | 3.26 | 2.31 |
| 21:45 | 2240 | Cercle Brugge vs Charleroi | 2.10 | 3.44 | 3.24 |
| 21:45 | 2256 | Dundalk FC vs Sligo Rovers | 1.96 | 3.21 | 3.60 |
| 21:45 | 3440 | Shamrock Rovers vs St Patricks | 1.79 | 3.45 | 3.98 |
| 21:45 | 4213 | Juventus vs Empoli | 1.45 | 4.19 | 6.51 |
| 21:45 | 5097 | Bohemians FC vs Finn Harps | 1.58 | 3.81 | 4.88 |
| 21:45 | 5571 | Derry City vs Shelbourne | 1.42 | 4.09 | 6.62 |
| 22:00 | 3740 | AC Ajaccio vs Paris St Germain | 9.89 | 5.03 | 1.29 |
| 22:00 | 4388 | Ipswich vs Derby | 1.71 | 3.68 | 4.47 |
| 22:00 | 5099 | Granada vs Zaragoza | 2.00 | 3.08 | 3.93 |
| 22:15 | 5114 | Porto vs Benfica | 2.27 | 3.28 | 3.03 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# MOROCCO MATUMAINI KIBAO AKIIKARIBISHA NIGERIA U-23

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Timu ya Soka ya Vijana ya Tanzania ya umri chini ya miaka 23, Hemed Morocco, amesema kikosi chake kiko tayari kuelekea mechi ya kusaka tiketi ya kushiriki Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON U-23) dhidi ya Nigeria itakayocheza kesho kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Tanzania ilisonga mbele katika mashindano hayo baada ya kuiondoa Sudan Kusini.

Akizungumza na gazeti hili jana, Morocco alisema ameridhishwa na kiwango cha wachezaji wake baada ya sasa kuonekana wameanza kupata muunganiko kutokana na aina ya mazoezi waliyokuwa wanafanya.

Morocco alisema pia ushindani wa wachezaji unakifanya kikosi hicho kiimarike zaidi na kila mchezaji ana morali ya juu kuhakikisha wanapata matokeo bora katika mechi hiyo ya kwanza.

"Timu imeimarika na pia inaonekana kucheza kwa mfumo rasmi, tunajua tunakutana na timu ngumu, timu yenye upinzani, tunashukuru tumepata mazoezi sahihi kuelekea mechi hiyo, tunachosubiri ni muda wa mechi," Morocco alisema.

Kocha huyo alisema anaendelea kukisuka kikosi chake katika mazoezi ya mwisho yatakayofanyika leo na imani yake kubwa ni kufanya vizuri na kujiweka kwenye nafasi nzuri ya kusonga mbele.

"Tunawaheshimu wapinzani wetu, tunafanyia kazi mapungufu yetu na kwenye ubora wao ili tuzidi kuimarika, Nigeria wako vizuri lakini na sisi tumejiandaa kwa ajili ya kutafuta ushindi hapa nyumbani, haitakuwa mechi rahisi kwa kila upande," alisema Morocco.

Mkuu wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Clifford Ndimbo, aliliambia gazeti hili maandalizi kuelekea mechi hiyo yamekamilika na wadau wanaombwa kujitokeza kuishangilia timu yao.

Ndimbo aliwataja waamuzi watakaocheza mchezo wanatoka Djibouti ambao wataongozwa na Souleiman Djama, Liban Abdoulrazak Ahmed, Rachid Wais Bouraleh huku mwamuzi wa akiba atakuwa ni Saddam Houssein Mansour wakati Mganda, Mike Letti, ndiye Kamishna.



Wachezaji wa Timu ya Soka ya Taifa ya Vijana wa umri chini ya miaka 23 wakifanya mazoezi kwa ajili ya kuwakabili Nigeria katika mechi kusaka tiketi ya kucheza fainali za Kombe la Afrika (AFCON U-23), itakayochezwa kesho kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam. **PICHA: TFF**

# Shime: Tutaivaa

INATOKA UK. 32

Mungu kwa matokeo mazuri wanayopata na kesho wataendelea kupambana ili kupata ushindi.

Luhala alisema wanafahamu wameingia hatua ya mtoano, hivyo watacheza kwa kiwango cha juu kwa malengo ya kusaka ushindi.

"Sisi kwetu tunaifananisha na mechi ya fainali, ukiingia fainali basi mawazo yanakupeleka katika ushindi, ndio tutakavyoingia, kwetu kila mechi ni muhimu, tunaziheshimu timu zote tunazokutana nazo, tunaamini huu ni mwaka wetu, tunataka kuendelea kumpa furaha Rais, Samia Suluhu Hassan," nahodha huyo alisema.

Robo fainali nyingine ya michuano hiyo itakayochezwa kesho itawakutanisha Marekani dhidi ya Nigeria.

# Yanga: Furaha yetu

INATOKA UK. 32

inakuwa kubwa. Naamini kikosi nilichonacho nikiri itakuwa mechi kubwa, ngumu na yenye ushindani, haijalishi matokeo yaliyopita ya timu yoyote ile. Kwa kawaida mechi hii huwa ina shughuli, niseme tu najiandaa vizuri na hiyo shughuli ya Jumapili, vijana wenyewe wanaelewa mechi hii ina uzito gani na wanatakiwa wafanye nini na hata mashabiki wetu wana matumaini makubwa," Mgunda alisema.

Kocha huyo aliongeza maandalizi yote muhimu yamekamilika na kilichobakia ni kuwaaminisha wachezaji wake wanaweza kama walivyofanya kwenye michezo ya kimataifa iliyopita.

Mara ya mwisho timu hizo zilikutana Agosti 13, mwaka huu katika mechi ya Ngao ya Jamii ambapo Yanga walipata ushindi wa mabao 2-1.

Simba yenye pointi 13 sawa na Yanga, ndio kinara wa ligi hiyo lakini ikiwa na moto baada ya kufanikiwa kutinga hatua ya makundi kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

# Michezo

Ijumaa Oktoba 21, 2022

Nipashe




UKURASA 29

## Ten Hag afunguka 'atadili' na Ronaldo

# Yanga: Furaha yetu ni kumfunga Simba

●●●Mgunda naye atamba ataicheza vyema 'ngoma' ya Jumapili na...

**Adam Fungamwango na Saada Akida**

WAKATI Yanga ikitamba wanasikia raha sana wanapomfunga mtani wao Simba, Kaimu Kocha Mkuu wa Wekundu wa Msimbazi, Juma Mgunda, amesema kikosi chake kiko tayari kwa mchezo huo wa Ligi Kuu Tanzania Bara utakaochezwa keshokutwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Akizungumza jijini, Kocha Msaidizi wa Yanga, Cedric Kaze, alisema wanahitaji kushinda mechi hiyo ili kurudisha mioyo iliyovunjika ya mashabiki wao baada ya kutolewa katika mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Kaze alisema ana imani Yanga itafanya vizuri katika mechi hiyo kwa sababu inawafahamu vyema wapinzani wao ambao waliwafunga pia katika mchezo uliopita.

"Tulichofanya kwanza ni kuwaweka sawa wachezaji kisaikolojia baada ya kupoteza mchezo wa Ligi ya Mabingwa Afrika. Haikuwa rahisi kwa sababu tuliwekeza nguvu nyingi, inabidi watoke kwenye hali hiyo ya masikitiko kwa sababu imeshatokea, sasa akili zielekezwe kwenye mchezo wa 'dabi' ambao mashabiki wanataka kuona timu inarudi kwenye njia nzuri na kuwasahaulisha kilichotokea. Inabidi tuingie katika mchezo huo kwa nguvu nyingi kutafuta pointi tatu," alisema Kaze.

Aliongeza ushindi pekee ndio utawaweka kwenye nafasi nzuri kuelekea mechi za Ligi Kuu zinazofuata pamoja na mchezo wa hatua ya mtoano wa Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya Club Africain ya Tunisia utakaochezwa Novemba 2, mwaka huu hapa nchini.

Ofisa Habari wa Yanga, Ally Kamwe, aliliambia gazeti hili kupata matokeo chanya dhidi ya Simba ni moja ya malengo ambayo wamejiwekea na kuongeza kikosi chao kimejiandaa kuendeleza furaha hapo Jumapili.

Kamwe alisema ubingwa wa Ligi Kuu huwa na raha zaidi pale unapomfunga mtani wako na wao ndio kitu wanachohakikisha hawakosei.

Naye Mgunda, ambaye itakuwa ni 'dabi' yake ya kwanza tangu ajiunge na Simba alikiri mechi hiyo itakuwa ngumu, lakini kikosi chake kiko kamili kwa ajili ya kupambana.

Mgunda alisema kikosi chake kiko tayari kumaliza 'ubabe' dhidi ya watani zao na kujiimarisha kwenye msimamo wa ligi hiyo inayodhaminiwa na Benki ya NBC.

"Nikiri hii itakuwa 'dabi' yangu ya kwanza nikiwa Kocha wa Simba, changamoto ya mechi hizi hakuna mtu asiyejua timu hizi zinapokutana basi heka heka

INAENDELEA UK. 31



Kocha Mkuu wa Yanga, Nasreddine Nabi (kushoto), akimwelekeza jambo winga wa timu hiyo, Jesus Moloko katika mazoezi kuelekea mechi dhidi ya watani wa jadi, Simba itakayochezwa kesho kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam. **PICHA: MTANDAO**

## Shime: Tutaivaa Colombia kikatili

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Timu ya Soka ya Taifa ya Wasichana wa umri chini ya miaka 17 (Serengeti Girls), Bakari Shime, amesema kikosi chake kimedhamiria kuendelea kuipeperusha vyema bendera ya Tanzania katika fainali za Kombe la Dunia (U-17) zinazofanyika nchini India.

Serengeti Girls inatarajia kuivaa Colombia katika mechi ya hatua ya robo fainali ya Kombe la Dunia itakayochezwa kesho kwenye Uwanja wa Pandit Jawaharial Nehru, Goa.

Shime alisema wachezaji wake wanaendelea vizuri na mazoezi na tayari ameyafanyia kazi madhaifu aliyoyabaini katika mechi zilizopita ili wafanye vyema kwenye mchezo wa kesho.

Kocha huyo alisema ameziangalia mechi zote ambazo Colombia wamecheza, hivyo amejiandaa kuingia tofauti kwa lengo la kuwashangaza wapinzani hao.

Alisema mechi hiyo itakuwa na ushindani mkubwa kwa sababu timu zote mbili zinahitaji kusonga mbele katika michuano hiyo inayoandaliwa na Shirikisho la Soka Duniani (FIFA).

Alisema wamejipanga kucheza kwa tahadhari na nidhamu ili kujiondoa katika presha ya kuruhusu mashambulizi ya mara kwa mara ambayo yanaweza kuwaondoa mchezoni.

"Tunaendelea na maandalizi kwa ajili ya mechi yetu ya Jumamosi, tumefanyia kazi mapungufu yetu yaliyojitokeza katika mchezo uliopita na kuingia kwa tahadhari kubwa ili kufanikiwa kusonga katika hatua inayofuata, bado tunaamini tunaweza kufanya vyema zaidi," Shime aliongeza.

Kocha huyo wa zamani wa Serengeti Boys, JKT Mgambo ya Tanga alisema anaendelea kuwapongeza wachezaji wake kwa hatua waliyofikia wakiwa wanashiriki kwa mara ya kwanza michuano hiyo kama nchi.

"Ushindani ni mkubwa sana na tuko makini, ninaimani na vijana wangu watapambana na kufuata maelekezo yote niliyowapa mazoezini, watatakiwa kuyahamisha katika mechi, hii itatusaidia na kutuweka salama, katika soka hakuna timu ndogo, Colombia nao wataingia wakifahamu wanakutana na timu iliyowaondoa mataifa makubwa," Shime alisisitiza.

Nahodha wa Serengeti Girls, Noela Luhala, aliliambia gazeti hili wanamshukuru

INAENDELEA UK. 31

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >